# Nipashe

Jumatatu Desemba 30 , 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580114
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710






## Serikali yavunja mkataba machinjio wa mabilioni

UKURASA 3

# Mafuriko yasomba makaburi, nyumba

**PIA** yakata mawasiliano ya barabara, TMA yaonya mvua kubwa zaja mikoa 11...*Endelea ukurasa wa 2*



Wazee wa kimila wa kabila la Kisukuma wakimvisha nguo za jadi pamoja na kumkabidhi mkuki na kigoda Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, ambaye jina la kichifu aliitwa Malonja, baada ya kuwasili katika ofisi ya Kanda ya Victoria jijini Mwanza. **PICHA: ROSE JACOB**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MRITHI WA FARU FAUSTA APATIKANA**

KUFUATIA kifo cha aliyekuwa faru mwenye umri mkubwa zaidi duniani, Fausta, Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), imemtangaza faru Vicky...

**UKURASA WA 5**

**MAJALIWA AWAPA KIBARUA MA-RC UJENZI MADARASA**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa nchini kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa na kukamilika kwa wakati...

## CCM SASA YAKUSANYA MAONI YA ILANI 2020

UKURASA 3

# Mwimbaji injili akiri kumuua mkewe

UKURASA 2


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

**MICHEZO** GOLIKIPA KMC ABAINISHA UZOEFU UMEIBEBA SIMBA UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Mvua yasomba makaburi, nyumba

Na Waandishi Wetu

MVUA zinazoendelea kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini zimeanza kuleta madhara baada ya nyumba 57 na makaburi saba kusombwa na maji wilayani Mvomero, mkoani Morogoro.

Aidha, usafiri wa mabasi ya abiria na magari ya mizigo katika barabara ya Rujewa hadi Madibira wilayani Mbarali mkoani Mbeya, umesitishwa kwa muda usiojulikana kutokana na barabara hiyo kuharibiwa na mafuriko ya mvua zinazoendelea kunyesha wilayani humo.

Wiki iliyopita Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitangaza baadhi ya mikoa ikiwamo Morogoro kuwa na mvua nyingi zinazoweza kuleta uharibifu.

Tukio la Mvomero lilitokea juzi katika Kijiji cha Kilimanjaro, Kata ya Sungaji, wilayani Mvomero baada ya nyumba hizo zilizopo katika eneo hatarishi zipatazo 57 kati ya 180, kuzingirwa na maji yakiwamo makaburi saba yaliyopo katika eneo hilo.

Akizungumzia tukio hilo, Diwani wa Kata ya Sungaji, Deogratius Daniel, alisema mvua hiyo iliyoanza kunyesha Alhamisi iliyopita na kuendelea imesababisha uharibifu huo wa nyumba na makaburi na baadhi ya wananchi kukosa makazi na kuhifadhiwa na majirani.

Alisema kuwa chanzo cha nyumba na makaburi hayo kusombwa na maji ni kutokana na Mto Mbulumi unaopita katika eneo la kijiji hicho, kuhama mkondo wake baada ya kutokea mmomonyoko wa ardhi.

Hata hivyo, diwani huyo alisema kufuatia makaburi hayo kusombwa na maji baadhi ya ndugu wenye makaburi mengine 14 walilazimika kuyahamisha katika eneo lingine ili kuepusha kusombwa na maji.

Mmoja wa waathirika wa tukio hilo, Rehema Hassani, alisema mvua zimesababisha nyumba yake kusombwa na maji na kuiomba serikali kuwapatia msaada wa haraka ikiwamo chakula pamoja na sehemu ya kujifadhi kwa muda kwa kuwa hivi sasa analazimika kuishi kwa msaada wa majirani.

Naye Ofisa kutoka Bonde la Wami Ruvu ambalo linasimamia maji ya mto huo, Mhandisi Elibariki Mmasi, alisema maji ya mto huo yamepoteza mwelekeo wake kutokana na mmomonyoko wa ardhi na kuwataka wakazi hao kuwa na subira wakati suala hilo likishughukiwa kwa ajili ya kurudisha mto huo katika mkondo wake wa kawaida.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Msifwaki Haule, baada ya kutembelea eneo hilo alisema baada ya kutokea uharibifu huo tayari wameshafikisha suala hilo katika

INAENDELEA UK. 8



Mkazi wa jijini Dar es Salaam wakitoa mabati juzi kwenye mto, eneo la Mabibo Relini, baada ya kuzolewa na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Zaidi ya madumu 5,000 ya mafuta yakamatwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huu, limekamata madumu 5,260 ya lita 20 za mafuta ambayo yaliingia nchini kwa magendo kupitia bandari bubu.

Hayo yamebainishwa juzi mjini Kibaha na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alipokuwa akitoa taarifa ya matukio yaliyotokea mwaka huu kwa waandishi wa habari.

Alisema, kukamatwa kwa madumu hayo kumetokana na operesheni za mara kwa mara, zilizofanywa na jeshi hilo kukomesha uhalifu.

Kamanda Wankyo alisema, pia zipo balo 16 za khanga, matairi ya pikipiki 175 na mafuta ya diseli lita 320 na watuhumiwa 23 walifikishwa mahakamani.

Kadhalika alisema, katika kipindi hicho, wahamiaji haramu 197, walikamatwa kwa makosa ya kuishi nchini bila kibali na kufikishwa mahakamani.

Alieleza kuwa, wahamiaji haramu hao waliokamatwa ni kutoka katika mataifa mbalimbali ambayo ni pamoja na Somali (18), Ethiopia (174), Kenya (2) Burundi (2) na Uganda (2).

Katika hatua nyingine, Jeshi hilo la Polisi limekamata pombe ya moshi lita 2,117 na milimita 500 na mitambo 15.

Kamanda Wankyo alisema, watuhumiwa 150 waliokamatwa, walifikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kamanda huyo alisema, operesheni mbalimbali zinaendelea katika mkoa huo kukomesha uhalifu na wananchi kuishi kwa amani.

# Mwimbaji injili akiri kumuua mkewe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MTUHUMIWA wa mauaji ya mkewe kwa kumpiga na shoka ambaye ni mwimbaji wa nyimbo za injili, Mosses Pallangyo (28), hatimaye amekamatwa na polisi akiwa mafichoni kuelekea nchini Kenya na kukiri mauaji hayo kwa madai kuwa shetani alimpitia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye Kituo cha Polisi cha Usa River, wilayani Arumeru, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Desemba 28, mwaka huu majira ya saa 11:30 jioni katika Kijiji cha Ekibushing, Kata ya Oltrument, Tarafa ya Muklati wilayani Arumeru.

"Mtuhumiwa huyu alikuwa amejificha wakati akitafuta njia ya kwenda mafichoni nchini Kenya, lakini sisi polisi kupitia kamati maalum ya kikosi kabambe ambacho yumo hadi Mkuu wa Wilaya hii, Jerry Muro, tulimtafuta na njia iliyofanikisha tumkamate ya 'Dog Style' yaani ya mbwa," alisema.

Alisema tangu kutokea kwa tukio hilo Desemba 25, mwaka huu majira ya mchana, katika Kijiji cha Kilinga, Tarafa ya Songolo wilayani humo, kikosi hicho hakijalala kilingia katika kazi ya kumsaka usiku na mchana hadi walipomkamata.

"Tulipomkamata alikiri kumuua mkewe na kusema ni shetani alimwingilia, ambaye mimi hili watu wa imani watusaidie maana sijui jinsi ya kumpeleleza shetani," alisema.

Alimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kwa kujaza mafuta magari yote ya polisi ili kazi ya kumtafuta isikwame.

Kamanda Shana alisema pia Muro amenunua pikipiki nne za Jeshi la Polisi ambazo zipo njiani kupelekwa Arusha kwa ajili ya kukabidhi.

Aliomba wananchi kuepuka kujichukulia hatua mkononi kwa sababu serikali haitamuacha salama.

"Kwa wale wanaotaka kumuona mtuhumiwa ndani ya siku mbili au tatu wafike mahakamani watamwona muuaji huyu," alisema.

Rais wa nyimbo za injili Tanzania, Dk. Donald Kisanga, alishukuru jeshi hilo na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kwa kufanikiwa kumtia mbaroni mtuhumiwa huyo ambaye ameua mwimbaji mwenzao pia.

"Lakini sisi kama waimbaji tunajipanga tukifahamu siku ya mazishi tutashiriki mazishi hayo kikamilifu na nawaomba waimbaji wenzangu tuwe watulivu katika kipindi hiki tuachie vyombo vya dola vifanye kazi yake na tuachane na mazungumzo yasio sahihi," alisema.

## HABARI KITAIFA



Madaktari wa mifugo na wanyamapori wakiufanyia uchunguzi mwili wa faru 'Fausta' ambaye alikuwa na umri mkubwa duniani alikufa mwishoni mwa wiki katika Hifadhi ya Ngorongoro Crater. **PICHA: MARC NKWAME**

# Mrithi wa faru Fausta apatikana

**Na Marc Nkwame,**

**NGORONGORO**

KUFUATIA kifo cha aliyekuwa faru mwenye umri mkubwa zaidi duniani, Fausta, Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), imemtangaza faru Vicky kuwa mnyama wa jamii hiyo mwenye umri mkubwa zaidi nchini kwa sasa.

Fausta aliyekufa akiwa chini ya uangalizi maalum ndani ya Bonde la Ngorongoro, na miaka zaidi ya 57, ameacha rekodi ya kuwa faru mweusi mwenye umri mkubwa kuliko wote duniani. Faru Vicky anakadiriwa kuwa na miaka 49 kwa sasa, na hivyo kuwa 'mgombea' pekee wa nafasi ya bibi wa kreta kwa sasa.

"Mara nyingi faru wanapozeeka, hupoteza uwezo wa kujilinda dhidi ya wanyama wengine kama fisi na simba, kwa hiyo ni muhimu kwa wahifadhi kuhakikisha usalama wa wanyama hawa adimu na wachache duniani," alibainisha Kamishna wa Uhifadhi katika Mamlaka ya Ngorongoro, Dk. Freddy Manongi.

Alisema kwa sababu faru Fausta alikuwa akiishi ndani ya jengo maalum, Mamlaka ya Ngorongoro inafikiria pia kumhamishia faru Vicky' ndani ya nyumba ya 'marehemu' Fausta ili kumsaidia na yeye katika kipindi chake cha uzee.

Naibu Waziri wa Utalii, Costantine Kanyasu, alisema baada ya faru Fausta kufariki, wizara itashirikiana na wahifadhi pamoja na wataalamu wengine kuangalia jinsi ya kuuhifadhi mwili wa aliyekuwa faru mkubwa kuliko wote ulimwenguni.

"Fausta ameishi maisha yake yote katika Hifadhi ya Ngorongoro mpaka umauti ulipomkuta usiku wa Ijumaa, Desemba 27, saa mbili unusu usiku," baadhi ya askari wanyamapori katika bonde la Ngorongoro walibainisha.

"Huyu ndiye alikuwa faru mzee zaidi duniani, hiyo ni historia kwa Tanzania...tunahisi kifo chake ni cha kawaida kutokana na umri wake mkubwa. Madaktari wapo njiani watatueleza hasa sababu ya kifo chake baada ya kufanya vipimo," aliongeza Dk. Manongi.

Faru Fausta licha ya umri wake mkubwa hakuwahi kuzaa na hiyo inaelezwa kuwa huenda ikawa ni moja ya sababu ya kuishi kwake kwa muda mrefu.

Faru wanakadiriwa kufikisha umri wa miaka 35 mpaka 40 wakiwa porini na huishi zaidi ya hapo wakiwa chini ya ulinzi maalumu.

Faru mwingine mweusi na jike aliyeishi porini kama Fausta na aliyefahamika kwa umri wake mkubwa ni Solio, wa nchini Kenya ambaye hata hivyo hajafikia umri wa 'Vicky' (49) na aliachwa mbali na Fausta (57), Solio alikuwa akiishi nchini Kenya na kufa akiwa na umri wa miaka 42 mwaka 2016.

# Serikali yavunja mkataba mauzo mali za machinjio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imevunja mkataba wa mauzo ya mali za machinjio ya Dodoma (TMCL) kati yake na kampuni ya NICOL uliosainiwa mwaka 2008, huku ikiitaka kampuni hiyo kulipa zaidi ya Sh. bilioni 14.96 za madeni ya TMCL na mapunjo katika biashara ya machinjio kwa serikali.

Sambamba na hilo, vyombo vya ulinzi na usalama vimeagizwa kuwachukulia hatua za kisheria watendaji wote wa NICOL, NARCO na TMCL waliohusika na ubadhirifu wa mali za TMCL na kuisababishia hasara serikali tangu mwaka 2008.

Hatua hiyo ilifikiwa jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, katika kikao cha wadau kujadili namna ya kunusuru machinjio hiyo.

Mpina alisema mkataba huo umevunjwa kwa kuzingatia ibara ya 7 na 13 ya mkataba wa mauzo ya mali na hivyo kuanzia sasa machinjio hiyo itakuwa chini ya serikali.

"NICOL ilipe serikali Sh. 9,712,127,660 ambazo serikali ilipunjwa katika biashara ya machinjio na pia NICOL ilipe madeni yote inayodaiwa kampuni ya ubia TMCL kiasi cha Sh. 5,248,084,000," alisema.

Aidha, aliitaka kampuni ya NARCO ijiondoe katika kampuni ya Ubia TMCL ndani ya siku 60 kuanzia jana.

"Huduma za uchinjaji zitaendelea kutolewa kama kawaida katika kipindi cha mpito chini ya usimamizi wa serikali wakati mchakato wa kumpata mwekezaji mahiri wa mpito na wa kudumu unaendelea," alieleza.

Mpina alisema serikali imejipambanua kuwa ya viwanda na wanyonge haitakubali hujuma na ufisadi uliokuwa ukifanyika katika machinjio hayo kuendelea.

"Aidha, nataka niwahakikishie kuwa waliohusika na wizi na ubadhirifu hawatapona, tunajua kuwa hata mishahara ya wafanyakazi nayo ilifanyiwa ufisadi na kuleta usumbufu mkubwa," alisema na kuendelea:

"Pia tunatambua mahitaji ya uchinjaji mifugo na kusafirisha nyama nje ya nchi ambapo kusimama kwa machinjio hii kulisababisha wafugaji na vijana wengi kukosa ajira na masoko ya uhakika."

Aliwaomba wadau wote walioathirika kwa namna moja au nyingine na uendeshaji wa machinjio hiyo waipe muda serikali kushughulikia changamoto zilizopo.

"Katika kipindi cha muda mfupi machinjio ya Dodoma itafufuliwa na kupanuliwa na kuwa ya kisasa zaidi," alisema.

Akizungumzia baadhi ya kasoro zilizobainika, alisema NICOL tangu ikabidhiwe mali hizo kwa kipindi cha miaka 11 haijawahi kutoa gawio kwa serikali.

Pia alisema nchi imepoteza ajira, fedha za kigeni, biashara na masoko ya mazao ya mifugo baada ya kiwanda kufungiwa kuuza mazao ya mifugo katika nchi za Falme za Kiarabu (UAE).

"Aidha, kampuni 10 zilisimama kusafirisha na kufanyabiashara ya nyama baada ya kiwanda kufungiwa, ambapo kwa mwezi mauzo ya nyama nje ya nchi katika machinjio yalikuwa yamefikia tani 192 sawa na mbuzi 24,000 kwa mwezi, pia kiwango cha uchinjaji ng'ombe kushuka kutoka wastani wa ng'ombe 120 hadi 50 kwa siku," alisema.


COMPANY NO 138904423

**EXTRACT OF THE RESOLUTIONS OF AN EXTRA-ORDINARY GENERAL MEETING OF THE MEMBERS OF WILD EXISTANCE SAFARIS LIMITED HELD AT THE REGISTERED OFFICES ON THE 27 DECEMBER 2019;**
**THE FOLLOWING RESOLUTIONS WERE DULY PASSED;**

**SPECIAL RESOLUTION**

At an Extra-Ordinary General Meeting the Shareholders of **WILD EXISTANCE SAFARIS LIMITED,** presided over by **STEPHEN ARTHUR ATTWELL** as chairperson by special resolution resolved the following:-

1) That the Company be wound up voluntarily effective from 27th December 2019.

2) That **Cyprian Herbert Mwaimu of Next Level Attorneys, Plot No. 7 & 8, Sikh Union Road, P.O. Box 1203, Arusha-Tanzania** be appointed as the liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing assets of the Company.

**We, the undersigned authorized representatives of the shareholders of the Company, hereby certify the foregoing to be a true and bona fide resolution passed by the Company on the 27th day of December 2019.**

Name: Stephen Arthur Attwell
Signature:
Designation: DIRECTOR
Date: 27th December 2019

Name: SAMWEL SIFAEL MATURO
Signature:
Designation: DIRECTOR
Date: 27th December 2019

115568902


# CCM yaanza kukusanya maoni Ilani 2020-2025

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeanza kukusanya maoni ya wananchi ya namna ya kuboresha maisha yao, ili yaingizwe kwenye Ilani ya uchaguzi ya 2020-2025.

Aidha, kamati za siasa za wilaya na mikoa zimeagizwa kuyakusanya maoni hayo na kuyafikisha makao makuu kwa ajili ya mchakato unaofuata.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ofisa Habari wa Ofisi ya Katibu Mkuu wa CCM, Said Said Nguya, agizo hilo limetolewa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ally, kwa lengo la kutengeneza ilani jumuishi.

Alisema moja ya maelekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM ni kuzitaka kamati za siasa za wilaya na mikoa kuwasilisha maoni ya wananchi wote katika kuboresha maisha yao.

Alisema maoni hayo yataingia kwenye mwelekeo wa Sera za CCM 2020 - 2030 na Ilani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 na kwamba mwisho wa kuwasilisha maoni hayo ni Januari, 2020.

Dk. Bashiru akiwa katika kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kagera kilichojumuisha wajumbe wa kamati za siasa na Sekretariet za Wilaya ya Bukoba Mjini, Vijijini na Misenyi, alisisitiza umuhimu wa wanachama wake kushiriki mchakato huo utakaokuwa na manufaa kwenye maisha yao.

"Wananchi wote wakiwamo walimu, madaktari, wafanyabiashara, wakulima na hata wale wa vyama vya upinzani, kwani CCM kwa namna inavyoendelea kutekeleza matakwa ya wananchi ni vema mawazo ya wanachama wa vyama hivyo nayo yakajumuishwa mapema kwa utekelezaji," alisema.

RIPOTI MAALUM -3

# Hivi ndivyo ilivyo rushwa ngono wasomi vyuo vikuu

Na Sanula Athanas

## ■Takukuru: Atakayenasa mhujumu uchumi
## ■Wanafunzi wakiri ‘kuwatega’ walimu

**SEHEMU ya pili ya mtiririko wa ripoti hii kuhusu kashfa ya rushwa ya ngono vyuoni, iliwasilisha ushuhuda wa pande zote zinazoguswa na tuhuma hizo, kila upande ukitoa uhalisia wa namna unavyoguswa. Endelea na sehemu ya mwisho kujua kwa kina yaliyojificha katika kashfa hiyo...**

GEORGE Mnali, Mwenyekiti wa TAHLISO, anageuza kichwa na kuwanyoshea kidole wanafunzi wenzake kwamba nao ni sehemu ya mzizi wa matatizo, akifichua siri ya kulazimisha uhusiano wa kimapenzi na wahadhiri wao.

Mnali anaeleza chanzo na mwenendo huo kwamba zaidi upo kwa wanafunzi anaowaita wazembe wa kujisomea, ambao wamekuwa wakijenga mazingira ya urafiki wa kimapenzi na wahadhiri, ili wapate msaada wa alama za bure za kufaulu kwenye baadhi ya masomo.

“Wakati mwingine siyo kwamba walimu wanalazimisha, ila ni baadhi ya wanafunzi wanawalazimisha walimu. Unakuta mwanafunzi anaona somo ni gumu, hivyo anaamua ‘kumtega’ mwalimu kimapenzi kwa lengo la kuepuka kufeli somo hilo.

“Kwa hiyo, hili suala la rushwa ya ngono ni suala la kuviziana pande zote. Nasema hivyo kwa sababu mwanafunzi wa kike akiona somo haliwezi, hata kama mwalimu hana mpango naye, anaweza kutumia mbinu ya ‘kumtega’ kimapenzi ili kumnasa mwalimu ampe alama za ufaulu,” anaeleza.

Pia, kuna sura nyingine inayosimuliwa na Seleman Juma, mhitimu wa shahada ya sanaa UDSM, anayeanika mtazamo mwingine wa kashfa hiyo kupitia uzoefu binafsi na ushuhuda wa kipindi chake cha masomo.

Anataja maeneo matatu anayodai kuwapo kasoro kubwa katika kusababisha rushwa hiyo, yakijumuisha ufanyaji na usimamizi wa utafiti, kazi za nyumbani wanazopewa wanafunzi na uwezeshaji katika upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi.

Juma, ambaye wakati wa masomo yake ya chuo kikuu alikuwa Naibu Waziri wa Mikopo wa Serikali ya Wanafunzi UDSM (Daruso), anaeleza kadhia ya baadhi ya wanafunzi kuendekeza rushwa pindi wanapopewa kazi za kufanya nyumbani.

Anasema hatua ya kwanza wanayochukua, ni kuwafuata wenzao wenye uelewa wa juu kimasomo na kuwaomba msaada wa kuwafanyia kazi hiyo, ambayo malipo ya maelewano yao yanajumuisha rushwa ya fedha au ngono.

“Kama uko vizuri darasani, mabinti wanakufuata uwasaidie kufanya ‘assignment and home work’ (kazi za nyumbani) zinazotolewa na wahadhiri, watakuletea vitabu, chakula na hata kukupatia fedha, lakini baadhi yao wanakuja kwa mitego ili uwatumie kimwili.

“Kwenye hizi ‘assignments’ kuna shida nyingine ya baadhi ya wahadhiri kuzitumia kuwanasa mabinti. Kuna mabinti ambao wanamalizana na wahadhiri huko wanakojua wao, darasani huwaoni, kazi za nyumbani mnazopewa hawafanyi, lakini kwenye matokeo ya mwisho ya kozi wana ‘A’ kibao,” anasimulia.

Vivyo hivyo katika utafiti, Juma anasema wapo wanafunzi wameendekeza tabia ya uvivu na kutafuta urahisi katika taaluma kwa kufanyiwa utafiti na watu wengine, wakiwamo wanafunzi wenzao kwa malipo ya fedha au ngono.

Anasema wahadhiri nao hawako mbali na mchakato huo wakitumia udhaifu na upungufu wa wanafunzi wao katika ufanyaji utafiti, wakigeuza kuwa mtego wa kutimiza malengo yao kwa mabadilishano ya aina hiyo ya rushwa.

Juma pia anaibua lingine lililojificha katika aina hiyo ya kashfa ambalo ni suala la upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi.

Anasema waligundua kwamba, baadhi ya wanafunzi wanaotafuta mkopo, wanakuwa tayari kwa lolote, ikiwamo kuwekeza katika aina hiyo ya rushwa kwa mhusika anayeratibu na kuwezesha upatikanaji wa mikopo, awatumie.

“Binti anakufuata umsaidie kufuatilia HESLB (Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu) mkopo wake au rufani yake ya kupewa mkopo. Anapoona majibu yanachelewa, anakufuata kwa mitego ya kingono, akiamini ukishakuwa na uhusiano naye wa karibu namna hiyo, atafanikisha suala lake,” anasimulia.

### UHUJUMU UCHUMI

Mnano Novemba 26 mwaka huu, katika wasilisho lake kuhusu maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Intelijensia wa Takukuru, Emmanuel Kiyabo, alisema hivi sasa rushwa inayohusu ngono nchini ni kubwa kuliko ya fedha.

Katika maadhimisho hayo yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa), Mtandao wa Wanawake (WFT), Takukuru na Jeshi la Polisi, Kiyabo alisema asilimia 28 ya wanawake wanaofanya biashara ndogo na wanafunzi wa vyuo wanatumikishwa kwa rushwa ya ngono.

Mwanasheria wa Takukuru, Imani Nitume, anatafsiri Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007, akirejea kifungu cha 25 kinachoainisha kwa upana maana hiyo kwamba:

“Mtu yeyote ambaye kwa kutumia nafasi yake au mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake, anadai au analazimisha upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria, atakuwa ametenda kosa.”

Mwanasheria huyo anaendelea kueleza kwamba, Takukuru imepiga hatua zaidi katika kuunga mkono juhudi za kumlinda mwanamke duniani dhidi ya unyanyasaji, udhalilishaji na kutambua umuhimu wake.

Anasema Machi 8 mwaka huu, taasisi hiyo iliyoanzishwa mwaka 1991 (kipindi hicho ikiitwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (Takuru) na baadaye mwaka 2007 kuitwa Takukuru), ilitoa tamko la kumtetea mwanamke dhidi madhila hayo ikiwamo kupambana na rushwa ya ngono.

Nitume anasema tamko hilo liliienda sambamba na uanzishwaji wa dawati maalum la kushughulikia rushwa ya ngono katika ofisi zote za taasisi hiyo.

Anaendelea kueleza kwamba, kulingana na marekebisho ya kisheria ya mwaka 2016, Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984 na marejeo yake ya mwaka 2002, ilifanyiwa mabadiliko na kufanya rushwa ya ngono nayo kuangukia kwenye jinai ya uhujumu uchumi.

“Kwa sasa rushwa ya ngono ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu yake siyo faini tena, ila ni kifungo cha mpaka miaka 20,” mwanasheria huyo anatahadharisha.

Mkuu wa Uelimishaji wa Takukuru, Asseri Mandari, anaeleza walivyojipanga dhidi ya aina hiyo rushwa, akidokeza mkakati mmojawapo wameanzisha kampeni wanayoiita ‘Vunja Ukimya Ondoa Rushwa ya Ngono’, inayolenga kutokomeza ukatili huo wa kijinsia.

Anaeleza mbinu wanayotumia katika kampeni hiyo, ni kama kilichoasisiwa Udom, kuanzisha vilabu vya wapinga rushwa katika maeneo mbalimbali, ambavyo vina wajibu wa kuelimisha na kutoa taarifa kwa kila kinachostahili.

Wakati kuna hatua hiyo inayoanikwa na Takukuru, ni mwezi mmoja baada ya taarifa ya mwanasheria wa taasisi hiyo, mwezi Aprili kwenye mkutano wa Bunge la Bajeti, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Goodluck Mlinga, aliibua kashfa nyingine dhidi ya wahadhiri.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, kuna lindi la malalamiko yanayoelekezwa kwa wahadhiri vyuoni wanaowafelisha wanafunzi wa kike kwa makusudi, pindi wanaponyimwa rushwa ya ngono.

Mbunge huyo alidai kuwa na majina ya wanataaluma husika na alianika msimamo wake kwamba alikuwa tayari kuyakabidhi kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako.

### USTAWI WA JAMII

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, naye amejitokeza katika sakata hilo, akikemea ukatili wa kijinsia vyuo vikuu, akinyosha kidole mahsusi kwa rushwa ya ngono.

Dk. Jingu mwenye dhamana na Maendeleo ya Jamii wizarani kwake, analalamika ukatili wa kijinsia umeshamiri katika vyuo vya elimu ya juu, anakokiri kuripotiwa malalamiko ya kuwapo wahadhiri wanaotumia mamlaka yao kuwalazimisha wanafunzi kushiriki nao ngono kwa mbadala wa ufaulu wa mitihani.

Katika namna ya kipekee, Dk. Jingu anasema ni kashfa isiyoishia kwa wanafunzi pekee, bali inawakumba hata wafanyakazi wa vyuo na anaweka msimamo wake kwamba: “Hili siyo sawa, tunatakiwa kulikemea kwa nguvu zote.”

Anasema kitaifa hatua inayochukuliwa ni kwamba, serikali hivi sasa inatekeleza mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Maelekezo yake kwa wakuu wa vyuo ni watekeleze agizo la Waziri mwenye dhamana na Ustawi wa Jamii na Afya, Ummy Mwalimu, la kuunga mkono mpango mkakati wa Takukuru, wa kuunda madawati ya jinsia vyuoni, ili kujengea jamii yao mazingira yaliyo salama dhidi ya rushwa.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo.

# Waziri Biteko ampa ofisa madini siku 7 kutoa leseni

**Na Renatus Masuguliko,** CHATO

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ametoa siku saba kuanzia jana kwa ofisa madini, mkazi wa Geita, Daniel Mapunda, kutoa leseni ya viwanda vidogo 278 vya kuchenjulia dhahabu ambavyo havijapata kutokana na kile alichodai kuwapo kwa urasimu katika mchakato wa utoaji leseni hizo.

Agizo hilo amelitoa juzi wakati akizindua soko la dhahabu la Buseresere, wilayani Chato, mkoani Geita, ambalo litatoa huduma kwa wachimbaji na litakuwa na wanunuzi 10 ambalo ukarabati wa jengo lake umegharimu zaidi ya Sh. milioni 68 huku Halmashauri ya Wilaya ya Chato ikichangia Sh. milioni 11.

Biteko alisema hadi sasa kuna maeneo ya kuchenjulia dhahabu 278 mkoani Geita hayajapatiwa leseni kwa ajili ya shughuli hiyo, licha ya kuwa tayari kwa kufanya kazi huku wamiliki wake wakiwekeza fedha nyingi katika miradi hiyo.

"Kuna migogoro ya kawaida inayodaiwa kuchangia uwapo wa ucheleweshaji wa kutolewa kwa leseni kwa wamiliki hao...itafutiwe ufumbuzi mara moja na kisha wawe wamepewa leseni ndani ya siku saba kwa hili sitokuwa na mjadala," alisema Waziri Biteko.

Pia amepiga marufuku tabia ya wachimbaji au wanaokwenda kuuza dhahabu kwenye masoko kunyanyaswa ikiwamo kukamatwa na kuhojiwa wanakoyapata madini ya dhahabu na badala yake waruhusiwe kuyauza na serikali kukata tozo zake.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wachimbaji wakilalamikia kunyanyaswa wanapopeleka dhahabu kwenye soko kwa kuulizwa walipoyatoa hatua ambayo inaweza kuwafanya baadhi ya wachimbaji kuamua kuiuza kwa njia za panya na serikali kupoteza mapato. "Mtu anapoleta dhahabu sokoni kuuza asinyanyaswe kwa kuulizwa maswali ameipata wapi dhahabau hiyo, hata kama atakuwa ameipata kutoka nje ya nchi kinachotakiwa asaidiwe kukamilisha taratibu zote na kisha auze dhahabu yake na siyo kuwapa vitisho, hii sitaki kuisikia," alisema Waziri Biteko.

Kufunguliwa kwa soko la dhahabu la Chato, kunafanya idadi ya masoko ya dhahabau mkoani Geita kufikia nane likiwamo soko kuu la dhahabu la Geita mjini na kwa mujibu wa ripoti ya mkoa, kiwango cha mapato ya serikali kinachotokana na biashara ya dhahabu kwa serikali kimepanda kutoka Sh. bilioni moja kwa mwezi hadi kufikia wastani wa Sh. bilioni tatu kwa mwezi.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala Mkoa wa Geita, Dennis Bandisa, mafanikio hayo yametokana na uanzishwaji wa masoko ya dhahabu mkoani hapo na mchakato wa kufungua masoko mengine kwa ngazi ya wilaya unaendelea ili kuwasogezea huduma karibu wananchi.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, wakikata utepe kuashiria kuzindua mfumo wa kidigitali utakaowezesha ndege kutua salama katika Kiwanja cha Ndege Mpanda, mkoani Katavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM awapa kibarua ma-RC ujenzi madarasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa nchini kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa na kukamilika kwa wakati ili wanafunzi wote waliochagulia kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 waanze masomo kwa pamoja.

Amesema lengo la serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaanza kusoma kwa pamoja kwa sababu wakipishana muda wa kuanza masomo baadhi yao wanashindwa kufanya vizuri.

Alitoa agizo hilo jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015/2020 kwenye mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Ruangwa.

Jumla ya watahiniwa 933,369 sawa na asilimia 98.55 ya waliosajiliwa, walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2019 na kati yao watahiniwa 759,737 wamefaulu ambao ni sawa na asilimia 81.50.

Kati yao wasichana ni 395,738 ambao ni sawa na asilimia 80.87 na wavulana ni 363,999 sawa na asilimia 82.20. Mwaka 2018 watahiniwa waliofaulu walikuwa asilimia 77.72, na kufanya ongezeko la ufaulu kuwa asilimia 3.78.

"Wakuu wa mikoa hakikisheni vyumba vya madarasa vinakamilika ili wanafunzi wote waliofaulu waanze masomo kwa pamoja. Kitendo cha wanafunzi kupishana kuanza masomo kinawafanya waliochelewa kutofanya vizuri katika mitihani yao."

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwasisitiza viongozi hao kusimamia vizuri elimu kwa watoto wa kike na kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika kuwakatisha masomo iwe kwa kuwaoa, kuwaozesha au kuwapa ujauzito.

Alisema serikali imeweka sheria kali

INAENDELEA UK. 8




Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mwaka 2019 ulikuwa mzuri kwa Taifa Stars

**KWANZA** kabisa tunapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama hadi siku ya leo.

Ikiwa imebakia siku moja ili kumaliza mwaka 2019, wadau wa soka nchini Tanzania hawataweza kuusahau kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia timu yake ya Taifa (Taifa Stars).

Timu hii ambayo wakati huo ilikuwa chini ya Mnigeria Emmanuel Amunike, ilionekana kama imekata tamaa ya kufanya vema katika safari ya kufuzu kushiriki katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2019), ambazo zilifanyika Juni mwaka huu nchini Misri. Ni mwaka ambao Tanzania iliweka rekodi kubwa ya kushiriki fainali hizo ikiwa imepita miaka 39 tangu iliposhiriki kwa mara ya mwisho mwaka 1980, ikiongozwa na nahodha wake Leodegar Tenga, ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Hata kama Taifa Stars haikufanya vema katika fainali hizo ikiwa imepangwa kundi moja pamoja na mabingwa wa michuano hiyo Algeria, Senegal na majirani zao Harambee Stars ya Kenya, lakini kitendo cha kushiriki fainali hizo ni mafanikio.

Wapo wachezaji na makocha mbalimbali wamepita katika kikosi hicho cha Taifa Stars, ambao walishindwa kufikia hatua hiyo, lakini kwa mwaka huu, timu hiyo ilifaulu na kupeperusha bendera ya Tanzania pamoja na wimbo wake wa taifa kuimbwa kwenye fainali hizo.

Ikionekana kuwa na nafasi finyu baada ya kufungwa na Lesotho, ndio timu pekee iliyozoa pointi nyingi kutoka kwa Uganda (timu iliyoonekana) ngumu katika kundi lao wakati wa kusaka tiketi, ilianza kwa kuishangaza Uganda baada ya kutoka nao sare tasa jijini Kampala na kuipa kichapo cha bila huruma cha magoli 3-0 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Na katika kuthibitisha au kuonyesha Taifa Stars haikubahatisha katika kukiandaa kikosi chake, ikiwa bila nyota wake wanaocheza soka nje ya Tanzania, iliweza pia kukata tiketi ya kushiriki kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), fainali ambazo zitachezwa Aprili mwakani nchini Cameroon.Kwa mara nyingine, Taifa Stars, ambayo sasa inanolewa na Kocha Mkuu Mrundi Etienne Ndayiragije, iliweza kuifunga Sudan nyumbani kwao na kukata tiketi ya kucheza CHAN kwa mara ya pili, mara ya mwisho Tanzania ilishiriki fainali hizo mwaka 2008.

Ili mafanikio haya yaweze kudumu, huu ni wakati wa kila mdau wa soka kushiriki kikamilifu katika kuifanya Taifa Stars iweze kuwa timu yenye ushindani na si kusindikiza timu nyingine.

Mafanikio ya timu hiyo yanaanzia katika ngazi za familia kwa kuwa wepesi kusaidia kuendelea vijana ambao mwisho wa siku, huvaa jezi ya Taifa Stars katika mashindano mbalimbali.

Huu ni wakati wa kutoa ushirikiano na kuwaunga mkono makocha na klabu zetu mbalimbali ili ziweze kutimiza malengo yao, kufanya kazi kwa weledi na kuacha kusubiri kusema viongozi hawafai pale Taifa Stars inapopata matokeo mabaya.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na serikali haiwezi kuipa matokeo chanya Taifa Stars, kama wadau wengine watajiweka pembeni wakati wa maandalizi.


Nipashe inakumbusha kuwa ni muhimu wadau wote wakashiriki kuanzia hatua ya maandalizi, ili mwisho wa siku, kama ni kucheza au kulia, iwe ni kwa pamoja.

Mwaka huu pia Tanzania iliweza kushiriki na kuwa mwenyeji wa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wa umri chini ya miaka 17 (Afcon 2019). Hii ni rekodi nyingine ambayo Watanzania tunatakiwa kujivunia, tunaamini nguvu ambazo zilitumika kufikia hapa, ziendelezwe ili mwaka ujao wa 2020 pia uwe wa mafanikio zaidi.

Katika mpira hakuna miujiza, endapo maandalizi sahihi yatafanyika, timu za Tanzania zitaendelea kufanya vema katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

## Lililotokea Uwanja wa Sokoine liwe funzo

**GUMZO** kubwa lililowaacha watu hoi wiki iliyopita ni Uwanja wa Sokoine Mbeya kutumiwa kwenye tamasha la muziki, kiasi cha kushindwa kuchezwa kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Prisons dhidi ya Yanga.

Kutokana na uharibifu huo, mechi hiyo ilihamishiwa kwenye Uwanja wa CCM Samora mjini Iringa na Yanga iliondoka na pointi tatu baada ya kushinda bao 1-0.

Picha zilizopigwa baada ya tamasha hilo zilionyesha uwanja umeharibika kiasi cha kuwasikitisha wadau wa soka.

Hakukuwa na nyasi zaidi kuonekana kama bonde au jangwa. Meneja wa uwanja naye alipoulizwa, majibu yake yalionyesha kuwa na yeye kukerekwa na jambo hilo, lakini akionekana kama vile hakushirikishwa.

Cha kujiuliza ni nani aliyeruhusu tamasha la muziki, tena la bure kufanyika kwenye uwanja huo ambayo ulitengenezwa sehemu ya kuchezea 'pitch' miaka michache iliyopita na kuwa moja ya viwanja vizuri nchini?

Inawezekana labda waandaaji wa tamasha walilipa pesa. Lakini thamani ya kuutengeneza uwanja huo unaweza kuwa chini kuliko gharama za malipo ya tamasha hilo? Hili mimi siamini.

Tayari Bodi ya Ligi imeufungia uwanja huo. Nimewaelewa Bodi ya Ligi. Si kwamba wameusimamisha mpaka pale utakapokuwa umetengenezwa, la hasha.

Ni kwamba imeufungia kabisa na hata ukishatengenezwa na kuwa tayari kuchezeka, itabidi uongozi na wamilikiwa wa uwanja mkoani Mbeya waandike barua ya kuomba radhi kwa kilichotokea kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi ili kuomba ufunguliwe na kutumika kwa michezo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Steven Mguto, alikaririwa akisema kuwa anasikitika kwa tukio hilo ambalo linaonekana kama uongozi wa uwanja umeonyesha dharau kwani ulitambua kabisa kuwa kesho yake kulikuwa na mechi, lakini ukaruhusu tamasha la muziki ambalo liliruhusu watu kuingia uwanjani, wakikanyaga nyasi na kucheza, kiasi cha kutoacha hata nyasi moja, lilipomalizika.

Mguto alisema kuwa inaonyesha kuwa uongozi haukuona umuhimu wa mechi hiyo zaidi ya umuhimu wa tamasha kwa sababu ratiba ya mechi hiyo ilifahamika tangu zamani, hivyo akasema wanaufungia hadi viongozi waone umuhimu wa uwanja huo kuchezewa mechi za Ligi Kuu.

Binafsi ninaipongeza Bodi ya Ligi kwa kuufungia uwanja huo na nadhani hii itakuwa ni fundisho kwa viwanja vingine.

Ni kweli inawezekana viwanja vingi mikoani havipati pesa nyingi kwenye mechi za mpira wa miguu, labda zikicheza Simba na Yanga, lakini pamoja na hayo haiondoi ukweli kuwa hivyo ni viwanja vya soka na si kumbi za burudani, ndiyo maana vina magoli.

Matamasha kama haya yalitakiwa yapelekwe kwenye viwanja vya wazi, lakini nadhani viongozi wa viwanja hivi huamua kuchukua pesa za matamasha kwa sababu zinakuwa nyingi kuliko zile za mechi ya mpira, lakini madhara yake ndiyo haya, unapotokea uharibifu hasara inakuwa kubwa kuliko kilichoingia.

Ukiachilia mbali Uwanja wa Sokoine hautopata tena mapato yatokanayo na soka, labda uongozi uendelee sasa kukodisha matamasha, lakini mashabiki wa Mbeya watakosa mechi mbalimbali za Ligi Kuu kwenye uwanja huo, nadhani hata na baadhi ya mechi za Ligi Daraja la Kwanza.

Kuna wafanyabiashara ndogo ndogo ambao walikuwa wakiuza jezi, vyakula, vinywaji, na hata wale wa usafiri kama bodaboda, bajaji na mabasi madogo wakati timu za mikoani zikifika Mbeya, lakini kwa sasa hawatoweza tena kufanya hivyo na hajulikani tena hali itatengemaa lini.

Timu za Mbeya City na Prisons na mashabiki wao itabidi waingie gharama zisizo za lazima za kwenda kucheza mechi nje ya mkoa huo kwa uzembe wa watu wachache tu.


Sina uhakika kama ratiba ya ligi nayo itakwenda sawa sawa, kwani Uwanja wa Samora pia hutumiwa na Lipuli, hivyo timu zingine mbili kwenda kutumia uwanja huo huo ni lazima kuwe na marekebisho ya ratiba pia.

Wakati wakazi wa Mbeya wakiteseka kwa kutopata burudani ya soka licha ya kuwa na timu mbili za Ligi Kuu, hili liwe fundisho kwa viongozi wa viwanja vingine nchini Tanzania kutokubali kuruhusu kuharibika kutokana na kutumika kwa mambo mengine ambayo yako nje ya kusudio la kujengwa kwa viwanja hivyo ambavyo kiasili vimetengenezwa kwa ajili ya kuchezwa soka tu.

MJADALA

# Hongera TFF kwa kubadilisha kanuni za usajili, lakini...

**Na Adam Fungamwango**




HATIMAYE Shirikisho la Soka Nchini (TFF) limebadilisha kanuni zake za usajili ambazo zilikuwa zikitumika kwa miaka mingi tangu enzi za (FAT) na sasa mchezaji atakayesajiliwa kipindi cha dirisha dogo hatosubiri hadi dirisha lifungwe na kamati ikae ndipo apate leseni ya kucheza, badala yake ataanza kucheza mara tu usajili utakapokamilika.

Mwenyekiti wa Sheria na Hadhi ya Wachezaji, Elias Mwanjala, alitangaza hivyo Jumamosi iliyopita wakati kukiwa na mkanganyiko kutoka kwa baadhi ya mashabiki wa soka kuhusu usajili wa msimu huu.

Kanuni ya usajili ya miaka yote ni kwamba wachezaji waliosajiliwa au kuhamishwa kuanzia Desemba 15 kipindi cha dirisha dogo kinachomalizika Januari 15 mwakani, wangeanza kutumia hadi siku ambapo dirisha litafungwa na kutolewa wiki moja ya pingamizi ambayo nayo ikiisha ndipo kamati hiyo inakaa kuchambua, mchezaji yupi amehamishwa kihalali na yupi usajili wake una matatizo.

Wale ambao wamesajiliwa kihalali huruhusiwa na wale ambao bado usajili una utata wanasimamishwa kwanza mpaka taratibu zote zifuatwe, kama vile timu kwa timu kumalizana kama kulikuwa na utata kwenye uhamisho.

Hali hii ilisababisha wachezaji wanaosajiliwa kipindi hiki kuisubiri kamati hiyo kwa muda mrefu kabla ya kuanza kuzitumikia klabu zao mpya.

Pia ilikuwa ikizua malalamiko kwani tayari klabu zimeshasajili wachezaji wapya ambao wanaona ndiyo watakaoziba mapengo, lakini wanalazimika kwanza kusubiri hadi kamati ikae.

Safari hii hali si hivyo, kwani mchezaji anaposajiliwa tu, kama timu zitamalizana na hakuna tatizo, mchezaji anaanza kuitumikia mara moja bila kusubiri.

Nianze kuipongeza TFF na Kamati yake ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kwa kubadilisha kanuni hiyo ili kuendana na wakati uliopo.

Ilikuwa inashangaza kuona kwa miaka ya karibuni usajili unafanyika kwa njia ya mtandao, lakini bado wachezaji wanakuwa wanasubiria hadi kamati ikae, kiasi kwamba kunakuwa hakuna tena umuhimu mtandao, badala yake inakuwa kama ule ule wa kizamani tu.

Kwa sasa Tanzania imeingia kwenye mfumo wa kisasa ambapo uhamisho ukifanyika, basi hakuna tena kusubiri. Hiyo ni hatua kubwa kwenda kwenye maendeleo ya soka.

Hata hivyo kuna angalizo kuwa isije ikawa mfumo huu umepitishwa kwa sababu ya kuinufaisha klabu fulani kwa sababu imesajili wachezaji muhimu wanaotakiwa kuwahi mechi fulani, hivyo ikawa haina maana yoyote ile.

Yanga imesajili wachezaji wengi kipindi hiki cha dirisha dogo na kwa utaratibu wa zamani, isingeweza kuwatumia kwenye mechi dhidi ya watani zao Simba inayotarajiwa kuchezwa hapo Januari 4 mwakani.

Kabla hata Mwanjala hajatangaza utaratibu huo mpya, tayari Ofisa mmoja wa Yanga alitangaza kuwa wachezaji hao wapya watachezea timu hiyo kwenye mechi dhidi ya Simba.

Sikuelewa kama alikuwa akisema bila kujua utaratibu ukoje, au tayari alishaambiwa na kamati hiyo kuwa utaratibu umeshabadilishwa.

Na siku chache baadaye ndipo Mwanjala akatangaza kanuni hiyo. Sina maana kwamba utaratibu huo ni mbaya, la hasha. Kama nilivyotangulia kueleza hapo juu kuwa ndiyo kwenda na wakati, ila shaka yangu isiwe tu imewekwa kwa sababu ya kuwarahisishia wachezaji hao kuwahi mechi hiyo ya watani na msimu ujao tukarejea tena kwenye mfumo wetu ule ule wa kusubiri kamati ikae.

Mara nyingi sheria au kanuni zilibadilishwa au kuwekwa kwa ajili ya kuinufaisha timu fulani huwa haidumu kwa sababu jambo lililokusudiwa likipita, inakuwa haina tena umuhimu, badala yake watu wanarejea kule walikotoka.

Msimu wa Ligi Kuu 2014/15, Simba ilinufaika na kanuni ya kuchagua mechi kama mchezaji akiwa na kadi tatu za njano, ambapo ilimchezesha Ibrahim Ajibu kwenye mechi ya Februari 28, 2015 dhidi ya Prisons, ikashinda mabao 5-0.

Hii ni baada ya kubainisha kuwa alicheza akiwa na kadi tatu za njano, lakini ufafanuzi wa (TFF) ukaja kuwa ipo kanuni kwa mchezaji kuchagua mechi ya kucheza na ipi ya kuitumikia kadi hiyo na cha ajabu ni kwamba klabu ya Simba pekee ndiyo ilikuwa inaijua kanuni hiyo.

Maajabu mengine yakaja kuwa baada ya hapo hakuna tena klabu iliyotumia kanuni hiyo na hata msimu ujao ikaondolewa hadi leo hii. Kwa maana hiyo ni kwamba utaratibu wa kanuni ya usajili wa dirisha dogo mchezaji kutosubiri kamati uwe endelevu na msimu ujao na inayofuata pia, tusije tena tukasikia vinginevyo kama ile kanuni ya Ajibu.



# Wananchi Ludewa wasubiri MV Mbeya II

**Na Elizabeth Zaya,**
LUDEWA

WANANCHI wanaoishi katika vijiji 10 vilivyoko katika mwambao wa Ziwa Nyasa, Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe wamesema wanaisubiri kwa hamu meli kubwa ya abiria MV Mbeya II, kutokana na jiografia ya eneo hilo kuzungukwa na milima na hivyo kutofikika kwa urahisi kwa njia ya barabara.

Meli hiyo ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo, inatarajia kuanza kufanya safari zake katika bandari zinazopitia vijiji hivyo kuanzia Januari mwakani ili kuwaondolea wananchi adha ya kukosekana kwa usafiri wa uhakika.

Wakizungumza na waandishi wa habari waliotembelea moja ya vijiji hivyo wananchi wa kijiji cha Lupingu walipongeza serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kwa kurudisha usafiri wa meli katika kijiji hicho baada ya zaidi ya miaka 15 ya kutokuwa na usafiri wa meli.Mwenyekiti wa kijiji hicho, Ignas Kopea, alisema meli hiyo ina umuhimu mkubwa kwa vijiji vyao kwa sababu biashara zao nyingi zinategemea usafiri wa maji kutokana na kuzungukwa na milima ya Livingstone ambayo haipitiki kwa njia ya barabara.

Alitaja vijiji vingine vinavyotegemea usafiri wa maji pekee kuwa ni pamoja na Nkwambili, Nsisi, Lifuma, Makonde, Kilondo, Nsele, Chachale, Zumbila, Nkanda na Nndoa.

Alisema kutokuwapo kwa meli kubwa kumechangia changamoto kubwa ya usafiri inayowalazimu watumie maboti madogo ambayo si salama kutokana na ziwa hilo kuwa na mawimbi makubwa.

"Tumekuwa tukipoteza watu, mali na vyombo vya usafiri kutokana na kuzama kwa maboti kwa sababu ziwa hili linachafuka sana mara kwa mara na safari zake hazitabiriki, unapanda likiwa shwari, lakini ukifika katikati linachafuka," alisema Kopea.

Alisema licha ya vijiji hivyo kuwa katika Wilaya ya Ludewa, lakini biashara zake nyingi wanafanya Kyela mkoani Mbeya kutokana na kufikika kwa njia ya maji.

"Ukitaka kwenda Ludewa utalazimika kutumia bodaboda na utalipa kati ya Sh. 12,000 hadi Sh. 15,000 kwenda tu na huwezi kubeba mizigo mikubwa. Ndiyo maana tegemeo letu kubwa ni meli ambayo itatusaidia kubeba mizigo mikubwa kama hii MV Mbeya II," alisema Mwenyekiti huyo.

Kopea alisema kurudi kwa usafiri wa meli kutawasaidia kukuza biashara zao ambazo kubwa ni uzalishaji wa dagaa.

"Tunamshukuru sana Rais wetu John Magufuli kwa kuwa vijiji hivi vilikuwa shimoni na sasa ametutoa huko tunakwenda kuongeza biashara zetu na kukuza uchumi wa vijiji vyetu na taifa kwa ujumla," alisema Kopea. Marko Ngwezi, mkazi wa kijiji hicho aliishukuru TPA kwa ujio wa meli hiyo na kutaka ianze kazi mapema mwakani kama ambavyo imepangwa ili kuondoa adha ya usafiri katika vijiji hivyo.

Meli ya MV Mbeya II imejengwa na serikali ya awamu ya tano kwa gharama ya zaidi Sh bilioni tisa ili kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo baada ya kuharibika kwa meli za MV Songea na MV Iringa, huku meli moja ya MV Mbeya ikizama na kuacha wananchi wanaozunguka ziwa hilo pasipo usafiri wa uhakika.

Kwa mujibu wa TPA, meli hiyo ya Mbeya II imekamilika kwa asilimia 98 na ipo katika majaribio ya mwisho ya kujiridhisha na ubora ili ianze kazi rasmi miezi ya mwanzoni mwa mwaka kesho.



Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Ally Possi (wa kwanza kulia), akikagua hali ya jengo ndani lililokuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika, ambalo kwa sasa linafanyiwa ukarabati alipotembelea Ofisi ya Mratibu wa Programu ya Ukombozi wa Bara hilo, mwishoni mwa wiki Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Utamaduni, Christopher Mhongole, anayemwakilisha Mratibu wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. **PICHA: MAELEZO**

# PM awapa kibarua ma-RC ujenzi madarasa

**INATOKA UK. 5**

ya kumlinda mtoto wa kike lengo likiwa ni kumwezesha amalize masomo yake ili aweze kujikwamua kiuchumi na aondokane na utegemezi na kupiga marufuku kuwakatisha masomo.

"Watoto wa kike wanatakiwa kuheshimiwa katika jamii na serikali itatoa adhabu kali ya kifungo cha miaka 30 jela kwa mtu atakayekatisha elimu ya mtoto wa kike iwe kwa kumuoa au kumpa ujauzito."

Pia alisema serikali inataka kuona idadi kubwa ya watoto wa kike wanatimiza malengo yao kielimu, hivyo ni lazima wakaondolewa vishawishi kwa kuboresha mazingira yao ya kujifunzia ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya mabweni.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu ameishukuru serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwamo na Wilaya ya Ruangwa, ambayo imepewa Sh. bilioni 38 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Aliupongeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kubuni mradi wa kimkakati wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao na pembejeo linalojengwa katika kijiji cha Lipande. Ujenzi huo unagharimu Sh bilioni 5.45.

Ghala hilo ambalo limeanza kutumika, lina uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 litaiwezesha halmashauri kujiongezea mapato ya ndani na kusaidia kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu na wafadhili. Pia litapunguza gharama za usafirishaji wa korosho walizokuwa wanatozwa wakulima wakati wa kusafirisha mazao.

Amesema katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano miradi mingi ya kimkakati imetekelezwa nchini ambayo ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), upanuzi wa bandari za Mtwara, Dar es Salaam na Tanga, uboreshwaji wa viwanja vya ndege, ununuzi wa rada na ununuzi wa ndege mpya. Pia alisema serikali ya awamu ya tano tangu ilipoingia madarakani mwaka 2015, kipaumbele chake kilikuwa ni kukuza kiwango cha uchumi kutoka cha chini kwenda cha kati ifikapo mwaka 2025 kupitia sekta ya viwanda.

# Mvua yasomba makaburi, nyumba

**INATOKA UK. 2**

ofisi inayoshughulikia maafa ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya utekelezaji zaidi.

**TUKIO LA MBEYA**

Barabara ya Rujewa hadi Madibira wilayani Mbarali mkoani Mbeya, yenye urefu wa kilometa 80 ni tegemeo kubwa kwa wakazi wa Mji wa Rujwa na Madibira na vijiji vinavyopakana na barabara hiyo ambayo inatajwa kuwa ni mhilimi mkuu wa kiuchumi kwa wakazi wa maeneo hayo.

Akizungumzia athari hizo Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, alisema jana kuwa barabara hiyo imeharibiwa vibaya kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mfululizo ambazo pia zimeharibu makazi ya watu kwa baadhi ya vijiji.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, mabasi yote ya abiria na magari ya mizigo yatalazimika kupita katika mji wa Mafinga mkoani Iringa ili kupeleka mizigo na abiria katika mji wa Rujewa na Madibira.

"Kutokana na uharibifu wa barabara hiyo, serikali tumeagiza mabasi yote ya abiria na magari ya mizigo kupitia katika mji wa Mafinga mkoani Iringa kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Alisema kuwa hadi kufikia jana jumla ya nyumba 10 zilikuwa zimeanguka ingawa hakuna kifo cha mtu kilichoripotiwa katika mafuriko hayo ambayo yameathiri miundombinu ya barabara hiyo ambayo ni tegemeo kwa uchumi kwa wakazi hao.

Alisema mpaka sasa serikali inaendelea kufanya tathmini ya athari za barabara hiyo na makazi ya watu walioathirika katika mafuriko ambayo kwa kiasi kikubwa yameathiri shughuli za kiuchumi kwa baadhi ya vijiji.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Mbarali walisema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, sasa gharama ya usafiri imefikia Sh. 30,000 kutoka Sh. 5,000 kutokana na kuibuka kwa kundi la vijana wanaoendesha bodabora kuwasafirisha abiria.

Wakati huo huo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetahadhariasha kuwa kutakuwa na mvua kubwa kwenye mikoa 11 nchini, ambayo italeta madhara na wananchi kutakiwa kuchukua hatua za kujikinga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye tovuti ya TMA juu ya utabiri wa hali ya hewa wa saa 24, mvua hizo zitanyesha kwenye mikoa hiyo na athari zinazoweza kutokea ni mafuriko.

Mikoa hiyo ni Ruvuma, Lindi, Mtwara na Kusini mwa mkoa wa Morogoro, pamoja na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe, Rukwa na Kaskazini mwa mkoa wa Morogoro.

**Imeandikwa na Ashton Balaigwa, MOROGORO na Innocent Ng'oko, MBEYA**

HABARI KITAIFA

# Wakulima warejeshewa furaha mbolea

**Na Mwandishi Wetu, KATAVI**

WAKULIMA, viongozi wa serikali na vyama vya ushirika vya msingi maeneo mbalimbali nchini wameendelea kuishukuru kampuni ya uuzaji na usambazaji mbolea na pembejeo za kilimo ya Petrobena East Africa kwa kufanikisha kusambaza mbolea ya kotosha na kwa wakati.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakulima, viongozi wa serikali na vyama vya msingi vya ushirika katika mikoa ya Mbeya, Katavi, Rukwa,

Tabora na Shinyanga wamesema kampuni hiyo imefanikiwa kurejesha matumaini ya wakulima kwa kufikisha mbolea hata kabla ya msimu kuanza.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alipongeza kampuni hiyo kwa kusambaza mbolea ya kutosha na wakati mkoani mwake akisema hiyo ni zawadi kwa wakulima ambao siku za nyuma bidhaa hiyo ilikuwa ni adimu kwao.

"Kila mmoja miongoni anafuraha moyoni mwake baada ya kuona shehena ya kutosha ya mbolea," alisema Homera na kuongeza kuwa kama serikali itahamasisha wakulima kutumia fursa hiyo kuimarisha kilimo.

Aliomba Petrobena East Africa Limited kuendelea kufanya kazi kwa karibu na vyama vya msingi vya ushirika ili kuwafikia wakulima kwa urahisi na kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo na pia kuchagiza maendeleo ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mhandisi MaryPrisca Mahundi, alisema kampuni ya Petrobena imeleta majibu sahihi kwa wakulima wilayani mwake na kuashilia mavuno msimu ujao.

"Wakulima hawatakuwa na sababu ya kusema hawana mbolea kwani imesambazwa kabla hata ya msimu kuanza. Nitoe wito kwa wakulima kuchangamkia shehena ya mbolea ambayo imeshawasili," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Ukonongo wilayani Melele katika Mkoa wa Katavi, Maganga Peter kwa upande wake mbali ya kuishukuru kampuni ya Petrobena, aliitaja kampuni hiyo kama mkombozi wa kweli wa mkulima.

"Kwa zaidi ya miaka kumi nyuma kama chama cha msingi cha ushirika hatujawahi kusambaziwa mbolea shehena nyingi kabla ya msimu kuanza hii ni historia kwetu na kwa niaba ya wanaushirika wote tunapenda kutoa shukrani zetu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, alisema:

"Mnafanya kazi nzuri sana katika kufanikisha azma ya serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025."

Naye Meneja wa Ushirika wilayani Kahama, Albert Chale, alisema "Kampuni ya Petrobena imekuwa karibu sana na wakulima mbali ya kusambaza mbolea ya YARA na pembejeo za kilimo, imekuwa ikileta wataalamu wa kilimo yaaani maofisa ugani kutoa elimu ya matumizi bora ya mboleo."

Mkurugenzi Mtendaji wa Petrobena, Peter Kumalilwa, alisema tangu kampuni yake ianze kujishughulisha na shughuli za kilimo na hasa usambazaji wa mbolea za YARA hapa nchini, wakulima wamekuwa wakifurahishwa huduma zake.

"Sisi kama kampuni tupo mstari wa mbele kuhakikisha tunachagiza maendeleo ya kilimo ili kiweze kufanikisha azma ya kujenga uchumi wa kati na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Kumalilwa.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na wakulima wa zao la tumbaku na pamba katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini jana, kwenye mkutano mkuu wa 24 wa Chama Kikuu cha Ushirika (KACU), Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack na kulia ni Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika (KACU), Emmanuely Charahani. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ma-RC, ma-DC watwishwa zigo ushirika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya nchini, kuhakikisha wanavipitia vyama vya msingi (AMCOS), na kuhakikisha viongozi wake waliochaguliwa wana sifa ya kuwaongoza wakulima wa mazao ya tumbaku na pamba.

Pia alisema, kama watabaini kuwapo kwa baadhi ya vyama vya msingi viongozi wake hawana sifa ya kuwaongoza wakulima hao watoe taarifa kwa mrajisi wa vyama vya ushirika ili kuwajibishwa.

Bashe alitoa agizo hilo katika mkutano mkuu wa 24 wa mwaka 2019 wa Chama Kikuu cha Ushirika (KACU) wilayani Kahama mkoani Shinyanga ambapo alisema viongozi wa vyama vya msingi walio wengi hawana mashamba ya tumbaku wala pamba, na wamechaguliwa kutokana na kuwa wasemaji kwenye maeneo yao.

Aidha, alisema viongozi wa vyama vya msingi wasiokuwa na sifa wamekuwa wakitumia madaraka yao vibaya kiwakandamiza wakulima wa tumbaku na pamba hasa wakati wa urejeshwaji wa fedha za ukopeshwji wa pembejeo na mbegu kutoka kwa kampuni za ununuzi wa mazao hayo.

"Kama wewe sio mkulima hauwezi kuwa kiongozi wa chama cha msingi, tunataka kiongozi AMCOS awe mkulima ambaye anajua changamoto na maumivu anayoyapata mkulima wakati wa kilimo...wakuu wa mikoa na wilaya hakikishe mnahakiki vyama vya msingi kama viongozi wake wanasifa na nafasi zao," alisema Bashe. Bashe alisema, viongozi wa vyama vya msingi vya pamba maeneo mengi viongozi wake wamekula fedha za wakulima na wakulima hajawalipwa na wanadai fedha zao na hiyo ni kwa sababu ya kuchagua viongozi wasiokuwa na sifa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellacka, akitoa taarifa ya kilimo cha tumbaku na pamba mkoani Shinyanga, alisema chama kikuu cha ushirika wilayani Kahama kiweza kuuza tumbaku yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 13.2.

Alisema fedha hizo zimezalishwa ndani ya Wilaya ya Kahama pekee, na kumwomba Bashe ili wakulima wa mpunga na mahindi waingizwe kwenye vyama vya msingi na kuuza mazao yao kwa bei nzuri kama walivyo wakulima wa tumbaku na pamba.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku, Stanley Mnozya, alisema tumbaku bora nchini inatoka Kahama katika Halmashauri ya Ushetu na kuwataka wakulima kuendelea kulima tumbaku bora.

Mrajisi wa Vyama Vikuu vya Ushirika, Benson Ndengenye, aliwataka wakulima wa tumbaku kuhakikisha wanapanda miti na kutumia matawi ya miti katika kukaushia tumbaku na kutengeneza mabani sanifu ya tumbaku.

# Mil. 62/- zatumika upatikanaji haki

**Na Happy Severine,** SIMIYU

ASASI ya Kawiye Social Development Foundation imeeleza kuwa kiasi cha Sh. mil. 62.13 kutoka Shirika la Legal Service Facility(LSF) kimetumika katika mradi wa upatikanaji wa haki mkoani Simiyu.

Akitoa taarifa ya mradi huo jana kwa waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Asasi ya Kawiye, Ezekiel Kasanga, alisema ruzuku hiyo ya fedha imetolewa kusaidia na kurahisisha upatikanaji wa haki ya wananchi wanaonyimwa haki zao.

Kasanga alisema asasi yake imejikita katika kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa matatizo ya kila siku ili kuwawezesha jamii kutumia vyombo vya haki na kujiepusha kujichukulia sheria mkononi.

Alisema mbali na ruzuku hiyo iliyotolewa katika kusaidia upatikanaji wa haki, pia imesaidia kutoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria wapya na kuwapatia vitendea kazi vikiwamo vitambulisho, vitabu na machapisho ambayo yatawasaidia kuwajengea uelewa zaidi masuala ya kisheria.

Aidha, Kasanga alitoa rai kwa wasaidizi wa kisheria wapya waliopatiwa mafunzo mkoani Simiyu kufanya kazi kwa uadilifu na kuwasaidia wenye uhitaji wa kisheria hususani wanawake na watoto ili waweze kupata haki zao wanazozikosa.

Naye mwanasheria kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mwanahamisi Kawega, alisema ni vema wasaidizi wa kisheria wa maeneo yote wakafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya serikali kama Polisi, Mahakama pamoja na Takukuru ili wawe na dhumuni moja la kumsaidia mwananchi anayekosa haki yake ya msingi.

Alisema kupitia mafunzo waliyopatiwa wasaidizi wapya wa kisheria, yatasaidia kupunguza kazi ya malalamiko yaliyokuwa yakiwasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.

## Washindi wa kampeni 'Ibuka Kidedea' waagwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imefanya hafla maalumu ya kuwapongeza na kuwaaga wateja walioibuka washindi katika kampeni yake ya Ibuka Kidedea na Akaunti ya NBC Malengo.

Washindi hao wamejishindia safari za kitalii ambapo baadhi watazulu mbuga ya wanyama ya Serengeti na wengine visiwa wa Sychelles.

Kampeni ya Ibuka Kidedea ilizinduliwa Oktoba mwaka huu ikiwa na lengo kuu la kuhamasisha utamaduni wa kuweka akiba kwa wateja, ambapo zawadi mbalimbali zikiwamo bodaboda zimekuwa zikitolewa kwa washindi walioingia kwenye droo maalum inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nichini.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga washindi hao iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa NBC, Elibariki Masuke, aliwashukuru wateja wote waliojitokeza kushiriki kampeni hii tangu kuzinduliwa kwake.

"Ibuka Kidedea imefanyika kwa mafanikio makubwa, tumeshuhudia idadi kubwa ya wateja wetu wakishiriki katika kampeni hii, lakini wateja wanashuhudia kuongezeka kwa amana zao kutokana na faida za kila mwezi.

"Natoa pongezi kwa washidi wetu wote na tunaamini mtaendelea kuwa mabalozi wetu wakati mkifurahia safari hizi katika msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka", kampeni hii bado inaendelea hivyo tunatoa wito kwa wateja wengine kushiriki katika kampeni hii kwa kuendelea kuweka akiba ili kupata nafasi ya kushinda zawadi," aliongeza Masuke.

Naye Meneja Chapa na Mawasiliano wa NBC, David Raymond, alisema ni matumani ya NBC kuwa kampeni hii inatoa hamasa kwa Watanzania kuwa na utamaduni endelevu wa kujiwekea akiba ili kutimiza mahitaji yao ya kifedha, lakini zaidi ni kuwa na uhuru wa kifedha.

Meneja Masoko wa NBC, Alina Kimaryo alisema Ibuka Kidedea imekuwa ikitoa zawadi kila mwezi na hadi sasa jumla ya pikipiki tano zimeshatolewa tangu mwezi Oktoba.

Ili kujishindia pikipiki (bodaboda) mteja anachotakiwa kufanya ni kuweka akiba kwa kiwango kinachoanzia Sh. 100,000 katika akaunti yake ya Malengo, na kwa safari ya Serengeti kiwango kinaanzia Sh. 1,000,000 na kiwango kinachoanzia 50,000,000 kwa safari ya Sychelles.

"Pamoja na zawadi hizi katika kampeni hii, wateja watakaoweka akiba katika akaunti zao za Malengo kwa kiwango kinachoanzia Sh. 1,000,000 wanapata nafasi ya kujishindia pikipiki ya miguu mitatu aina ya Toyo katika droo kubwa ambayo jumla ya pikipiki za kubebea mizigo (Toyo) tatu zitatolewa," alisema.

Mmoja wa washindi aliyejishindia bodaboda, Daudi Patrick Majani, mstaafu na mfanyabiashara anayeishi Tabata Segerea jijini Dar es Salaam, alisema atatumia bodaboda yake kumwingizia kipato na kuitumia kwa usafiri utakaosaidia kuiwezesha biashara yake.

Washindi walioshinda safari ya Serengeti ni Christopher Mgote kutoka Nzega, Makongoro Makongoro kutoka Arusha, Jocelyine Rwechengura na Esther Ndunguru wote kutoka Dar es Salaam. Washindi walioshinda safari ya Sychelles ni Wambura John Wambura kutoka Tarime mkoani Mara, Ramadhan Saidi, Lettice Rutashobya na Sylevester Ambokile wote wa jijini Dar es Salaam.

# Waandikishaji wa daftari la kudumu wahimizwa haki

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KATIBU Tawala Wilaya ya Wete, Mkufu Faki Ali amewataka waandikishaji wasaidizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwaorodhesha wananchi wote ambao wana sifa ya kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura bila kujali itikadi zao.

Alisema kuandikishwa katika daftari hilo ni haki ya kila mwananchi ambae anazo sifa zote za kuandikishwa kuwa mpigakura na kuchagua kiongozi anayemtaka. Mkufu aliyasema hayo alipokuwa akifungua semina ya siku mbili kwa waandikishaji wasaidizi wa NEC.

Alisema uandikishaji huo ni uboreshaji wa daftari la wapigakura ambao umefanywa na NEC ili kuwapa fursa wananchi wote ambao hawajaorodheshwa katika daftari hilo, pamoja na kuhakiki taarifa zote za wananchi ambao wamehama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Uboreshwaji huo wa daftari ni kuwapatia wananchi wote ambao hawajaandikishwa, lakini hata wale ambao wamepoteza stakabazi zao (vitambulisho) kuwa ni rahisi kupata vingine na wale ambao wamehama kutoka eneo moja kwenda nyingine nao pia kubadilishiwa eneo," alisema Mkufu.

Katibu huyo aliwataka kuwa na moyo wa kujitolea na kuwa na uzalendo wa nchi yao bila ya kujali muda ambao watautumia wakati wakiwa kazini.

"Kazi za uchaguzi ni kazi ngumu sana tena unatakiwa uwe mstahimilivu, uweze kujituma na kujitolea, lakini pia inatulazimu tufuate sheria na taratibu ambazo zimewekwa na Tume ya Uchaguzi," alisema Mkufu. Aliwataka waandikishaji hao kuelewa wajibu wao na kutoa maelekezo mazuri kwa wananchi pale ambapo zinaweza kutokezea kasoro.

"Lakini niwaombe wote ambao wamefanikiwa kuingia katika zoezi hili, kuwa wasikivu na kufuata maelekezo yote ambayo yatatolewa na wasimamizi wao," alisema Mkufu.

Naye Ofisa Mwandikishaji Wilaya ya Wete, Issa Juma Hamad, aliwahakikishia wananchi wote wa wilaya hiyo kuwa hakuna mwananchi ambaye atakosa haki yake kwa kisingizio kisichokuwa na misingi.




Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (katikati), akimkabidhi tiketi ya ndege mmoja wa washindi wa kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo, Jocelyne Rwechungura, aliyejishindia safari ya kwenda Sychelles wakati wa hafla ya kuwaaga washindi hao iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja Masoko wa benki hiyo, Alina Maria Kimaryo. **MPIGAPICHA WETU**

# Uwanja wa Ndege Mpanda wapata mfumo wa kisasa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MAMLAKA ya usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imezindua mfumo wa kisasa wa GNSS RNAV katika viwanja vya ndege vya Mpanda mkoani Katavi unaoiwezesha ndege kuruka na kutua kwa usalama zaidi.

Mfumo huo ulizinduliwa juzi na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, na kusema kuwa safari za anga zitaongezeka ndani ya mkoa huo kutoka siku moja kwa wiki hadi kufikia siku tatu kwa wiki.

Alisema mfumo huo unaimarisha chombo pamoja na usalama wa abiria, pia humwezesha rubani kupima usalama kwa kutumia mitambo badala ya kupima kwa macho.

"Leo tunazindua huu mfumo wa RNAV katika viwanja vya ndege hapa Mpanda, nina imani mfumo huu utasaidia sana kumwezesha rubani kupima usalama kwa kutumia mitambo na sio macho... pia utaongeza siku za kusafiri kwa abiria itakuwa Jumanne, Alhamisi na Jumamosi," alisema Kamwelwe.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, alisema mfumo huo ulianza kufanyiwa kazi Novemba 2019 na uligharimu kiasi cha Sh. milioni 25 hadi kukamilika na kuanza juzi.

"Mfumo huo ulianza kutekelezwa Novemba mwaka huu na leo (juzi) umekamilika, lakini ulitugharimu kiasi cha Sh. milioni 25 tu... tungetumia wataalamu kutoka nje nadhani angezidisha fedha hiyo," alisema Johari.

Alisema mfumo huu wa RNAV tayari uko kwenye viwanja vikubwa nchini kama JNIA, KIA, AAKIA (Zanzibar), Mwanza, Songwe, Dodoma, Tabora, Kigoma, Bukoba, Chato na Iringa.

Usafiri wa anga ndani ya mkoa wa Katavi ulianza rasmi Oktoba 26, mwaka huu kwa safari za kutoka Mpanda kwenda jijini Dar es Salaam.

# Wazazi, walezi wabanwa chakula shuleni

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, amesema ataanza kuwachukulia sheria kali, wazazi na walezi wanaokwepa kuchangia chakula shuleni.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akiongea na wazazi kwenye mkutano wa kujadili maendeleo ya sekta ya elimu uliofanyika Kata ya Endabash.

Alisema ni kosa kisheria kwa sababu wanachangia kuumiza watoto waliopo shuleni.

"Sasa nasema kuanzia sasa serikali hatutawaacha, tutafuatilia kwa karibu na tutawachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaokwepa kuchangia chakula shuleni, kwa kisingizio cha serikali tunafanya kila kitu," alisema.

Mahongo alisema Rais John Magufuli alikuja na mpango endelevu wa elimu bure, ili watoto wengi nchini kupata elimu, lakini suala la chakula shuleni bado ni jukumu la mzazi au mlezi.

Alisema suala hilo limeonekana kuwa na changamoto zinazosababishwa na wazazi na walezi kutowajibika ipasavyo, licha ya waraka wa elimu kuwekwa bayana kwa wazazi au walezi juu ya umuhimu wa kushirikiana na walimu katika kuunda kamati zitakazohudumia wanafunzi kupitia michango ya chakula cha mchana.

Aidha, alisema hajaridhishwa na hali ya upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Endabash, kwani imechangia kwa kiwango kikubwa kuathiri hali ya kitaaluma na ufaulu.

Alisema kutokana na hali hiyo, analazimika kuvalia njuga suala hilo kwa kuwachukulia hatua kali wazazi au walezi watakaoshindwa ama kukaidi maelekezo ya serikali ya kuchangia chakula cha mchana cha wanafunzi.

"Sipo tayari kuona wilaya yangu inashuka kiwango katika ufaulu kwa sababu ya suala la chakula, kwa kutumia sheria ya mtoto 2009, tutahakikisha tunawashughulikia wazazi, walezi ambao wanakwepa majukumu yao," alisema.

Naye Mratibu wa Mradi wa Shirika lisilo la kiserikali la World Vision aliyeshiriki mkutano huo kama mmoja wa wadau wa elimu wilayani humo, Daniel Kirhima, alisema mpaka sasa wamewafikia zaidi ya watoto 1,000 kutoka kata mbalimbali wilayani humo na kutekeleza miradi ya kilimo, maji, afya na elimu, ili kuhakikisha ustawi wawanafunzi unakuwapo shuleni.

"Watoto hawa ni taifa la kesho, wanapokuwa na ustawi bora ni hatua kubwa kwa taifa, kwani tunaamini nyanja mbalimbali zitapata wataalamu wazuri waliojengewa misingi imara toka ngazi za chini," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Emmanuel Mkongo, akiongea na wananchi wa Kata ya Mbuyuni kuzingatia elimu na ushauri toka kwa wataalamu wa afya ili kuwa na afya bora wakati wote. **PICHA: WOINDE SIZZA**

# Wakulima waombewa mazingira ya kukopeshwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI na taasisi za fedha zimeombwa kushirikiana kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha wakulima kukopesheka kwa urahisi, kwa kuweka dhamana mashamba yao, ili kuboresha kilimo chao.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Huduma katika Kijiji cha Kilimatembo Kata ya Rhotia wilayani Karatu, Fabiano Petro, wakati akizungumza na wakulima kijijini hapo alipotembelea shamba darasa na kujifunza mbinu bora za kilimo na changamoto zinazowakabili.

Petro alisema wakulima wengi hususan walioko vijijini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha, kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo, hali inayosababishia kuendelea kulima kimazoea. "Sasa hivi gharama za pembejeo za kilimo zipo juu sana, hali inayosababisha wakulima kushindwa kulima kisasa na kuishia kulima kilimo cha kimazoea, ambacho mwisho wa siku wanaishia kupata hasara, na kutokuwa na hali ya kupenda kilimo," alisema.

Meneja masoko wa kampuni ya kizalendo ya usambazaji na uzalishaji wa mbegu za mahindi katika kampuni ya IFFA, Luhenda Yangole, aliwataka wakulima kuyatumia mashamba darasa yalioandaliwa kama mfano, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima, ili walime kilimo cha kibiashara na kuondokana na kilimo cha mazoea cha kuishia kuhudumia kaya zao.

Yangole alisema changamoto kubwa iliyopo kwa wakulima wengi ni kutofanya kilimo kama biashara kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya mbegu bora za kisasa na matumizi bora ya zana za kilimo.

"Wakulima wengi wanalalamikia changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununulia pembejeo, katika hili sisi tupo tayari kuwakopesha pembejeo kupitia vyama vyao vya ushirika na mtapatiwa kwa bei rahisi, kwani watachukua moja kwa moja kwenye kampuni yetu na kwa kufanya hivyo tunawahakikishia usalama wa mbegu zetu pia," alisema Yangole.

Ofisa Mazao wa Wilaya ya Karatu, Twilumba Ngwale, aliwataka wakulima hao kubadilika na kutumia kanuni bora za kilimo kama wanavyoelekezwa na wataalamu na kutumia mashamba darasa kujifunza na kujua mbegu bora za kilimo zinazowafaa kwenye maeneo yao.

Mmoja wa wakulima katika Kijiji cha Kilimatembo, Jackson Musa, aliziomba kampuni za mbegu kuendelea kuwatembelea wakulima vijijini na kutoa elimu juu ya matumizi bora ya mbegu za kutumia, ili walime kilimo chenye tija na kuondokana na mazoea.

# Madini kinara kwa mapato

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

SEKTA ya madini mkoani Manyara imejisifia kukusanya mapato zaidi ya kiwango walichopangiwa na Wizara ya Madini cha Sh. milioni 75 kwa kipindi cha miezi sita toka kufunguliwa kwa ofisi zao Mjini Babati na kukusanya Sh. milioni 140.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Ofisa Madini mkoani Manyara, Mhandisi Godfrey Nyanda, wakati akizungumza na Nipashe.

Mhandisi Nyanda alisema baada ya kufungua rasmi ofisi hizo ambazo zilipewa jukumu la kusimamia wilaya za Babati, Hanan'g, Mbulu na Kiteto, walipangiwa kukusanya Sh. milioni 75 kwa kipindi cha miezi sita, ili kukamilisha mwaka wa fedha 2018/2019, ambapo walivuka lengo la ukusanyaji.

Aidha, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020 wilaya nne wanazozisimamia zimepangiwa kukusanya Sh. bilioni moja, huku nchi nzima inatakiwa kukusanya Sh. bilioni 470.

"Mpaka sasa kwenye kipindi hiki cha pili cha robo ya mwaka 2019/2020 tumeshakusanya Sh. milioni 230 na tunaamini tutakamilisha kiwango tulichojiwekea," alisema Mhandisi Nyanda.

Alisema baada ya serikali kufanya marekebisho ya sheria ya madini ya mwaka 2010 namba 15 ambayo marekebisho yake yalifanyika mwaka 2017 na kanuni za soko la madini mwaka 2019 yamewarahisishia ukusanyaji wa kodi.

"Kwa sasa mchimbaji ana uhakika wa soko ila zamani mchimbaji aliuza bei yeyote ila sasa tunatoa bei elekezi, lakini zamani uuzwaji wa madini ulikuwa ni holela," alisema.

Kwa mujibu wa Mhandisi Nyanda, kwa sasa serikali inapata kipato kikubwa kwenye sekta ya madini tofauti na zamani, ambapo tangu walifungua ofisi katikati ya bajeti, lakini walikusanya mapato waliyopangiwa Sh. milioni 75 na kuzidi mpaka Sh. milioni 140.

Naye Mwenyekiti wa Wachimbaji wadogo wilayani Babati, Emmanuel Penco, aliishukuru serikali kwa kuwathamini wachimbaji wadogo.

Alisema wachimbaji wadogo siku zote ndio wanagundua madini, ila kwa Babati bado wachimbaji wadogo wako kama yatima, kutokana na kukithiri kwa migogoro.

## Wafagilia agizo la DC fedha za choo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKAZI wa Mijongweni katika Kata ya Mnadani, Wilaya ya Hai, wameeleza kuridhishwa kwao na uamuzi wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, kuagiza kupelekwa leo kiasi cha Sh. milioni saba kijijini hapo kwa ajili ya kujenga choo cha walimu wa Shule ya Msingi Mijongweni.

Jana kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliieleza Nipashe kuwa wamefurahi kwa namna serikali ya wilaya hiyo ilivyolishughulikia jambo hilo.

Ibrahim Amon alisema: "Tunamshukuru DC (Mkuu wa Wilaya) kwa kulitafutia jambo hili ufumbuzi wa kudumu kwa umakini mkubwa, lazima tuseme kweli kwamba kazi anayoifanya tunamuunga mkono na kimsingi ameibadili sana wilaya yetu na kuifanya ipige hatua kimaendeleo."

Kwa upande wake, Zuhura Ally alisema ujenzi wa choo hicho utasaidia kumaliza tatizo hilo la muda mrefu, huku akipongeza serikali kwa kuona changamoto hiyo na kuitatua kwa haraka.

Juzi, DC Sabaya, aliagiza kiasi cha Sh. milioni 42 ambazo ni za Mfuko wa Jimbo la Hai zimegwe Sh. milioni saba na zipelekwe kujenga choo cha walimu wa Shule ya Msingi Mijongweni.

Fedha hizo ni za Mfuko wa Jimbo hilo linaloongozwa na Mbunge wa Hai (Chadema), Freeman Mbowe.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, tayari ameshatoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai, Yohana Sintoo kutoa kiasi hicho cha fedha na kuzipeleka katika shule hiyo leo.

Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Hai kupitia kwa mkurugenzi wake, Yohana Sintoo, imekabidhi mifuko 20 ya saruji kwa ajili ya kuanzisha mchakato huo na ndipo Sabaya alipoingilia kati ili choo hicho kijengwe na kukamilika Januari 2020.

# Mawakala wadaiwa kutoza fedha usajili simu

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

BAADHI ya wananchi wa wilaya za Siha na Hai, wamelalamikia hatua ya mawakala wa kampuni za simu za mkononi kuwatoza fedha wakati wa usajili wa laini zao za simu kwa kutumia alama za vidole ili wasajiliwe kwa haraka.

Kwa nyakati tofauti jana na juzi, tangu Rais John Magufuli atangaze kuongeza siku 20 zaidi za kusajili laini hizo, inadaiwa kuwa baadhi ya mawakala mitaani wenye mashine za kielektroniki zinazotumiwa kusajili, wamegeuza zoezi hilo kuwa fursa ya kujipatia fedha.

Walitoa malalamiko yao wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu ujanja unaofanywa na mawakala hao mitaani kujipatia fedha ili kumsajili mteja kwa haraka. Mmoja wa wananchi hao, John Mmari, mkazi wa Siha, alisema wanashangazwa na jambo hilo kwa kuwa katika matangazo walielezwa kuwa kusajili wa laini ni bure.

"Jana nilikwenda kusajili laini zangu mbili kwa hao watu wanaokaa chini ya miavuli ya kampuni za simu, sasa baada ya kusajiliwa nikaambiwa nitoe Sh. 2,000 kwamba kila laini moja nilipaswa kulipa Sh. 1,000. Nikahoji kwa nini, nikajibiwa kama nataka kusajiliwa bure niende kwenye maduka ya kampuni yaliyopo Moshi Mjini," alisema Mmari.

Desemba 27, mwaka huu, Rais Magufuli akiwa mkoani Geita alitangaza kuongeza siku 20, kuanzia Januari mosi, 2020 hadi 20 kwa wote ambao watashindwa kusajili laini zao katika kipindi cha kuishia Desemba 31, 2019.

Mkazi mwingine wa Kata ya Karansi, Wilaya ya Siha, Elizebert Lukumai, alisema alisajiliwa laini tatu na mawakala hao na alielezwa kwamba kabla ya kujisajiliwa anatakiwa kulipa Sh. 3,000. "Baada ya kusajiliwa tu hizo laini, huyo mhudumu alinitaka nitoe Sh. 3,000 kwa ajili ya gharama ya kusajili laini zangu tatu na akaniambia kama sina pesa niache simu nikatafute au niondoke nazo, lakini hasajili bila kupokea pesa yake. Kwa hiyo ombi letu kwa mamlaka husika walichunguze jambo hili na hasa Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania," alieleza Lukumai.

Kwa upande wake, Angelah Mbaga, mkazi wa Bomang'ombe wilayani Hai, alisema alikwenda kusajili laini zake za simu katika kituo kikuu cha mabasi cha Bomang'ombe, na alipofika aliambiwa atoe Sh. 1,000 ili asajili laini yake.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alipoulizwa kama amewahi kupokea malalamiko ya wananchi wa Siha alisema:

"Kama kuna mwananchi anadaiwa fedha wakati wa kusajili laini kwa alama za vidole atoe taarifa katika Kituo cha Polisi ili aliyemdai pesa aweze kuchukuliwa hatua. Toeni taarifa sehemu husika ili huyo anayewaomba pesa tumjue kwa kuwa usajili ni bure."




Watoto wanaoishi mji wa Hale wilayani Korogwe, wakionyesha samaki ambao wamewavua katika Mto Pangani, ambapo watoto hao wanahatarisha maisha yao kwa kuliwa na mamba katika mto huo. **PICHA NA STEVEN WILLIAM**

# Ubovu wa barabara waiathiri Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

HALI mbaya ya ubovu wa miundombinu ya barabara ya Hedaru katika Wilaya ya Same ambayo inaunganisha vijiji vya milimani vya Gundusine, Makasa na baadhi ya maeneo ya Saweni, inatishia uchumi wa wakazi wa ukanda huo.

Sehemu ya barabara hiyo kutoka Hedaru Mjini kwenda Gundusine ambayo ina urefu wa kilometa 14 inayopita kando kando ya miamba, haijawahi kuchongwa kwa katapila tangu kupatikana kwa Uhuru mwaka 1961.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Gundusine, Kata ya Hedaru waliozungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, wameeleza kuwa ubovu wa barabara hiyo umesababisha kwa sasa kutopitika kwa magari zaidi ya pikipiki za kukodi. Mkazi wa Gundusine, Haidan Mmbaga alisema barabara hiyo haipitiki kirahisi kwa magari kwa sababu ya mawe na wembamba wa barabara, hali ambayo imefanya waendesha pikipiki kuwatoza wananchi kiasi cha Sh. 10,000 kukodi pikipiki kutoka Hedaru hadi Gundusine. "Mawe mengi yamesababisha ubovu wa miundombinu ya barabara hii na ndiyo sababu imeibua adha ya usafiri kutokana na kutokuwapo kwa daladala za kuwasafirisha. Inatuwia vigumu mfano kufuata huduma za afya na mahitaji mengine muhimu katika Mji Mdogo wa Hedaru," alisema Saimon Wehael.

Pia mawasiliano mabovu ya barabara hiyo yanadaiwa kutesa wajawazito na watoto kukaa kwa muda mrefu katika usafiri wa pikipiki kufuata huduma mbalimbali ikiwamo hospitali katika Mji wa Hedaru.

"Kupitia kwa Mkuu wa Wilaya ya Same (Rosemary Senyamule) tunamwomba aliangalie suala hili kwa huruma, hali sio nzuri kwa watumiaji wa barabara hii. Tumepiga kelele kwa mamlaka husika kusaidia kurejesha mawasiliano, lakini mpaka tunafika mwisho wa mwaka hakuna hata matengenezo ya dharura yaliyofanyika. Niwaombe Tarura waliangalie upya suala hili," alisema.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wa kata hiyo wameiomba serikali kutatua tatizo hilo kwa kuwa wanalazimika kutumia gharama kubwa kukodi usafiri wa pikipiki baada ya kukosa mabasi madogo ya kusafirisha abiria.

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, kutoa ufafanuzi kuhusiana na malalamiko ya wananchi hao, alisema amepokea tayari taarifa za wananchi hao na kuanzia wiki ijayo atakwenda kukagua barabara hiyo na kuzungumza na wananchi.

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 30, 2019
Nipashe
Spotika



MOURINHO NA MIPANGO MIPYA KUIBEBA SPURS UK. 20




## ISIKUPITE

Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, amesema kuwa atakapostaafu kucheza kandanda, atajaribu kufanya kazi ya kuigiza filamu. Bado Ronaldo mwenye umri wa miaka 34 na nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno hajatangaza kustaafu, tayari msimu huu akiwa ameshaifungia timu yake mabao 10 katika mechi 14 alizocheza.

# HAKUNA NJIA

Mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling (kushoto), akimtoka golikipa wa Wolves, Rui Patricio, na kwenda kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa mwishoni mwa wiki. City ilifungwa mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

SOKA




# KLABU 5 ZILIZOCHEZA MECHI NYINGI BILA KUFUNGWA EPL

**LONDON, England**

WAKATI Ligi Kuu England ikizidi kuchanja mbuga, hadi sasa klabu ya Liverpool ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi hadi sasa.

Ushindi wao wa hivi karibuni ni dhidi ya Watford, waliposhinda 2-0 na ule dhidi ya Leicester City walioshinda mabao 4-1 hivyo kuifanya Liverpool kufikisha mechi 35 kwenye ligi tangu msimu uliopita bila ya kupoteza.

Mara ya mwisho kupoteza kwenye ligi ilikuwa Januari.

Hata hivyo, vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp si timu ya kwanza kwenye historia ya Ligi Kuu England kucheza mechi kibao bila ya kuonja machungu ya kupoteza.

Makala hii inakuchambulia timu ambazo zilicheza bila kupoteza mchezo.

**Manchester United - Mechi 29**

Timu ya Manchester United ilicheza mechi 29 bila ya kupoteza kwenye ligi katika awamu mbili tofauti. Kwanza ni kwenye ule msimu waliobeba mataji matatu makubwa, ambapo walianzia Krismasi hadi mwisho wa msimu na mwanzo wa msimu mwingine bila ya kupoteza, hadi walipokuja kufungwa Oktoba 1999, kabla ya kurudia rekodi hiyo kuanzia Aprili 2010 na Februari 2011.

**Manchester City - Mechi 30**

Kikosi hiki cha Manchester City kila mmoja aliamini kwamba huenda kingefikia rekodi ya Arsenal ya kucheza msimu wote kwenye Ligi Kuu England bila ya kupoteza mechi, wakati walipocheza mechi 22 bila ya kupoteza msimu wa 2017/18.

Lakini, walikuja kuvurugwa kwa kipigo cha 4-3 kutoka kwa Liverpool, lakini hiyo ilikuwa kabla ya kucheza mechi 30 mfululizo bila ya kupoteza.

**Liverpool - Mechi 35**

Liverpool ndiyo timu ya sasa ambayo imecheza mechi nyingi bila ya kupoteza, ambapo tangu Januari 12 mwaka huu, wamecheza mechi 35 hadi sasa bila kupoteza.

Wamekuwa na rekodi tamu kweli kweli kwenye Ligi Kuu England, ambapo kwa sasa wanaoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 13. Rekodi yao ya kushinda mfululizo ilivurugwa na Manchester United msimu huu.


**Chelsea - Mechi 40**

Wakati Jose Mourinho alipowasili Stamford Bridge mwaka 2004, haraka sana aliibadili timu hiyo na kuwa moto uwanjani, ambapo timu hiyo ikageuka kuwa hatari ndani ya uwanja, ambapo walicheza kwa miezi 12 na wiki tatu bila ya kupoteza mechi yoyote. Rekodi yao hiyo ilikuja kumalizwa na United kwenye msimu wa 2005/06, licha ya kwamba Chelsea ilibeba ubingwa.

**Arsenal - Mechi 49**

Wanaoshika namba moja ni Arsenal, hasa kwenye ule msimu wao ambao walicheza bila ya kupoteza mechi kwenye Ligi Kuu England. Arsenal ilicheza mechi 49 bila ya kupoteza. Arsenal walicheza kutoka Mei 7, 2003 hadi Oktoba 24, 2004 bila ya kupoteza mechi yoyote, hadi hapo waliposhindwa kufikisha mechi ya 50, ambapo walichapwa na United.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi (31), ambaye ni raia wa Argentina, ndiye mchezaji anayevuta mkwanja zaidi duniani. Kwa mwaka anapokea kiasi cha Dola milioni 127 kutokana na mishahara yake na fedha kutoka kwa wadhamini wake.

MICHEZO



Emmanuel Okwi



Haruna

# WACHEZAJI WALIOREJEA KLABU ZAO KAMA NIYONZIMA

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imemrejesha tena kiungo wake za zamani Haruna Niyonzima kuichezea kwa mara ya pili.

Yanga ilimtangaza Niyonzima kwenye kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo akitokea AS Kigali ya nchini Rwanda ambako ndiko nyumbani kwao.

Kurejea kwa Mnyarwanda huyo kunaongeza idadi ya wachezaji ambao wameshawahi kuzitumikia klabu zao nchini, wakaondoka na kurejea tena mara ya pili.

Mara ya kwanza, alijiunga na Yanga mwaka 2011 na kuichezea kwa miaka sita, kabla ya kumtimkia kwa wapinzani wao wa jadi, Simba 2017 na kuitumikia kwa kipindi kimoja cha miaka miwili kabla ya kurudi kwao na kutua AS Kigali kwa kipindi kifupi.

Hawa ni baadhi ya wachezaji waliowahi kuzichezea klabu zao hapa nchini, wakahama na baadaye kurejea kwa mara ya pili kama Niyonzima.

**1. Emmanuel Okwi**

Ni mchezaji aliyejiunga na kuondoka kwenye klabu moja zaidi ya mara moja.

Okwi, raia wa Uganda ameichezea klabu ya Simba mara tatu kwa vipindi tofauti.

Mchezaji huyo kipenzi cha Wanamsimbazi, alijiunga na Simba 2010 akitokea SC Villa na kuichezea kwa miaka mitatu, akahamia Etoile du Sahel 2013, lakini mwaka huo huo, baada ya kuwa na mgogoro na klabu yake, akaenda kuicheza klabu yake ya zamani SC Villa kwa mkopo.

Hata hivyo mwaka huo huo alijiunga na Yanga na kuichezea kwa msimu mmoja hadi 2014, aliporejea kwenye klabu yake pendwa ya Simba.

Okwi anayeweza kucheza nafasi kama mshambuliaji msaidizi au winga, aliichezea kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi 2015, alipoondoka na kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Sweden katika klabu ya Sonderjyske na kuitumikia hadi 2017, aliporejea tena SC Villa, kabla ya kurejea Simba na kuichezea mara ya tatu 2017, hadi mwaka huu alipohamia klabu ya Al Ittihad ya nchini Misri.

**2. Mrisho Ngasa**

Kama ilivyo kwa Okwi, naye ameichezea Yanga kwa vipindi vitatu tofauti.

Ngasa ambaye ni Mtanzania alijiunga na Yanga 2006 akitokea Kagera Sugar na kuitumikia kwa miaka minne, hadi 2010, alipouzwa kwenye klabu ya Azam FC.

Hata hivyo, kabla ya mkataba wake kumalizika, alipelekwa kwa mkopo kwenye klabu ya Simba ambako aliichezea hadi 2013 na baada ya mkataba wake kumalizika, alirejea kwenye klabu ya Yanga.

Huko akakaa kwa miaka miwili hadi 2015, alipokwenda kucheza soka la kulipwa nchini Afrika Kusini, akiitumikia klabu ya Free State Stars kwa msimu mmoja na kutimkia Fanja FC ya Oman 2016 hadi 2017, ambapo alirejea nchini na kujiunga na Mbeya City.

Ngasa ambaye ni winga wa kulia, aliichezea kwa nusu msimu, kwani dirisha dogo alikwenda Ndanda FC kwa mkopo hadi 2018 alipojiunga aliporejea tena Yanga hadi leo hii.

**3. Miraji Athumani**

Ni mchezaji ambaye amekuja juu msimu huu akiwa na klabu ya Simba, lakini wengi hawajui kama anarejea tena kwenye klabu hiyo kwa mara ya pili.

Miraji anayemudu kucheza winga zote za kulia na kushoto, pia mshambuliaji msaidizi, ni mchezaji aliyelelewa kwenye kikosi cha pili cha Simba. Ni mmoja wa wachezaji waliopandishwa kucheza kikosi cha kwanza, lakini kutokana na wakati huo timu kusheheni mastaa, aliondoka na kwenda kwenye klabu ya Toto Africans mwaka 2015.

Aliingia mkataba wa mwaka mmoja na 2016 baada ya msimu kumalizika, aliondoka na kwenda kujiunga na Mwadui FC.

Alikaa kwenye klabu hiyo kwa miaka miwili hadi 2018, alipojiengua na kwenda kujiunga na Lipuli FC kwa mwaka mmoja na ulipomalizika, klabu ya Simba iliamua kumrudisha Msimbazi, hivyo akarejea tena kwa mara ya pili.

**4. Haruna Shamte**

Beki huyo wa kulia, ambaye ana uwezo wa kucheza beki wa kushoto, ni zao la kikosi cha pili cha Simba.

Alianza kuichezea Simba ya wakubwa 2008 hadi 2014 alipoondoka kwenda kujiunga na JKT Ruvu.

Aliicheza klabu hiyo kwa mwaka mmoja na kwenda kujiunga na Mbeya City 2015 hadi 2018 alipoamua kwenda Lipuli FC.

Mwaka huu, Simba imeamua kumrudisha nyumbani na kuwa mmoja wa wachezaji waliorejea kwenye klabu walioichezea kwa mara ya pili.

**5. Shaaban Chilunda**

Shaaban Chilunda ni mmoja wa mastraika hatari nchini. Anaichezea Azam FC. Naye ni mmoja wa wachezaji waliorejea kwenye klabu zao kwa mara ya pili.

Alianzia soka kwenye kikosi cha pili cha Azam FC mwaka 2012 hadi 2016 alipopandishwa kwenye kikosi cha kwanza.

Mwaka 2018 alipelekwa kwenye klabu ya Tenerife ya Hispania hadi 2019 mwanzoni alipopelekwa tena kwa mkopo kwenye klabu ya Izarra pia ya nchini humo.

Katikati ya mwaka huu alirejea nchini na kujiunga tena na klabu yake ya zamani ya Azam FC na anaendelea kuichezea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**6. Hussein Javu**

Ni straika ambaye alianzia soka lake JKT Ruvu. Lakini umaarufu aliupata akiwa kwenye klabu ya Mtibwa Sugar mwaka 2010 hadi mwaka 2003, alipojiunga na Yanga.

Alikaa kwa miaka miwili tu, kabla ya kurejea tena kwenye klabu yake ya zamani Mtibwa Sugar, 2015.


Msimu uliopita alikuwa na kikosi cha Alliance, msimu huu anaichezea Ndanda FC.

**7. Issa Rashid 'Baba Ubaya'**

Ni mchezaji beki wa kushoto wa Mtibwa Sugar. Awali alikuwa akiichezea klabu hiyo kabla ya kutimkia Simba mwaka 2013 ambako alicheza kwa miaka miwili na kurejea tena kwenye klabu yake ya zamani na kuwa mmoja wa wachezaji walioondoka na kurejea kwenye klabu zao za zamani.

## NJE YA UWANJA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kuwa anashindwa kusajili wachezaji raia wa Ufaransa kutokana na gharama ya kuwapata nyota hao kuwa kubwa. Liverpool inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya pointi 21.



## Extra Time



# MAKINDA WA 5 WANAOKIMBIZA ULAYA

**MADRID, Hispania**

SOKO la Ulaya kwa sasa linaonekana kutawaliwa na vijana wengi ambao wanapenya kiurahisi katika vikosi vya kwanza, licha ya umri wao kuwa mdogo.

Wanabeba majukumu uwanjani kama vile ni wachezaji wakongwe. Hapa makala hii inakuchambulia wachezaji makinda watano ambao wanatesa kwa sasa kwenye soka la Ulaya.

**5. Frenkie de Jong**
**Klabu:** Barcelona
**Umri:** 22

"Ni mchezaji kijana ambaye namfananisha na Sergio Busquets kwa uchezaji wake pamoja na pasi zake," hayo yalikuwa ni maneno ya Xavi akimzungumzia De Jong kwamba ndiye anayeweza kurithi mikoba ya Busquets pale Barcelona. Miezi sita baadaye, Frenkie de Jong akatua Camp Nou.

Ulikuwa ni usajili wenye mapinduzi makubwa, kwani aliondoka kiungo mkabaji na kuingia kiungo mkabaji mwingine katika klabu ambayo inatumia mfumo wa mawazo ya Johan Cruyff.

Pamoja na umri wake mdogo, lakini tayari Barcelona wamemwamini na kumpa mikoba ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza. Na yale anayoyafanya ni makubwa, hivyo ni wazi kwamba, safari yake kisoka itakuwa ni ya kuvutia zaidi.

**4. Trent Alexander-Arnold**
**Klabu:** Liverpool
**Umri:** 21

Trent Alexander-Arnold kwa sasa anatamba pale Liverpool katika safu ya ulinzi. Pamoja na umri wake wa miaka 21, Kocha Jurgen Klopp ameonyesha imani kubwa kwake na alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wakati Liverpool ikibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kwa kiwango chake, ni wazi kwamba, wengi wanatabiri safari nzuri kwa Alexander-Arnold itakuwa nzuri zaidi katika kipindi chake cha uchezaji.

**3. Jadon Sancho**
**Klabu:** Borussia Dortmund
**Umri:** 19

Ni 'dogo' kutoka pale Kennington nchini England na aliamua kwenda Ujerumani ili kutimiza ndoto yake ya kucheza soka la kulipwa.

Baada ya kufanya mambo makubwa pale katika Klabu ya Borussia Dortmund msimu uliopita kwa kuwa na 'asisti' nyingi, dunia sasa inalijua jina la Jadon Sancho.

Kwa sasa klabu nyingine zimekuwa zikitajwa kuwania saini yake, lakini ni wazi kwamba, Sancho ameingia kwenye daraja la juu kama mchezaji mkubwa, wakati umri wake ukiwa bado mdogo kabisa.

**2. Matthijs de Ligt**
**Klabu:** Juventus
**Umri:** 20

Huyu alikuwa nahodha wa Ajax wakati ikitwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu ya Uholanzi kwa kipindi cha miaka mitano na akanunuliwa na Juventus kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 75.

Matthijs de Ligt ni mmoja wa mabeki bora zaidi wa kati vijana kwa sasa, licha ya umri wake wa miaka 20. Mchezaji huyo namna anavyopambana uwanjani unaweza kudhani ni beki mkongwe aliyeshinda Kombe la Dunia na ana umri wa miaka 31.

**1. Kylian Mbappé**
**Klabu:** Paris Saint-Germain
**Umri:** 21

Kylian Mbappé kwa sasa ndiye mchezaji anatazaminiwa kuwa mshindi wa Ballon d'Or kwa siku za usoni.

Mabao 39 kutoka kwenye miguu yake katika mechi 43 alizoichezea Paris St Germain wakati wa msimu wa 2018/19 yanathibitisha hili.

Tayari katika umri wake ameshabeba taji la Kombe la Dunia akiwa na kikosi chake cha Ufaransa, maana yake ni kwamba safari yake ya mafanikio kwenye soka ni kubwa na inaonyesha wazi kwamba atakuwa mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi kwa siku chache zijazo.

Wakati dunia ikishuhudia utawala na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kwa kubeba tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa Ulaya na Dunia, sasa ni wazi kwamba wengi wanaamini ndani ya siku za usoni, Mbappe ndiye atakayekuwa mfalme wa tuzo hizo kwa kipindi kirefu.

## Nukuu

"Nimefurahi kuwa na kundi hilo la makocha wenye vipaji. Kutakuwa na mchanganyiko wa wazoefu na wenye mawazo mapya. Pamoja na vipaji hivi vilivyopo hapa, tunaamini tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuirudisha timu kwenye makali yake ya ushindi," **Kocha mpya wa Arsenal, Mikel Arteta alisema siku chache baada ya kujiunga na kikosi hicho.**



"Nia yangu ni kubakia hapa, ninahitaji mwaka mmoja zaidi ili kuongeza utulivu, ninapenda kuwapo hapa ili kuisaidia timu hii iliyoko kwenye janga la kushuka daraja," **mshambuliaji, Mario Balotelli, alisema licha ya Rais wa Brescia inayoshiriki Serie A, Massimo Cellino, kuweka wazi kwamba Mtaliano huyo anaweza kuondoka klabuni hapo katika dirisha dogo la usajili la Januari.**



"Kwa uhakika wale waliohusika watafutwe na kuadhibiwa haraka, katika soka la kisasa timu kama Tottenham Hotspur yenye mashabiki wengi uwanjani pamoja na televisheni na kamera za ulinzi, itawezekana kuwatafuta na kuwaadhibu. Kama sio, lazima kutakuwa na mashahidi uwanjani ambao waliona na kusikia tukio lile. Ni aibu kwamba matukio ya ubaguzi wa rangi bado yapo hadi mwaka 2019. Upuuzi huu hautakoma?" **alisema Antonio Rudiger.**



# Michezo




# BAO LA FRAGA NA MENGINE YALIYOFUNGWA 'USIKU'

**Na Adam Fungamwango**

MBRAZIL Gerson Fraga (pichani) alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC ya Kinondoni kwenye dakika ya tatu ya nyongeza, akiiwezesha Simba kushinda mabao 2-0.

Lilikuwa ni bao la pili kwa mchezaji huyo kwenye klabu ya Simba, lingine alilifunga kwenye mechi ya mashindano ya Kombe la FA, Simba ilipocheza dhidi ya Arusha FC.

Goli la Jumamosi lilikuja wakati kila mmoja akiamini kuwa mechi ingeisha kwa bao 1-0, lililofungwa na Deo Kanda dakika ya 46, lakini mashabiki wa Simba wenye mioyo midogo bado walikuwa hawana imani na kudhani KMC ingeweza kusawazisha kutokana na mashambulizi yao makali ya kushtukiza.

Fraga ameingia kwenye rekodi ya wachezaji waliofunga magoli kwenye dakika ya 90 ya mchezo au dakika za majeruhi ambazo huongezwa kufidia zile zilizopotea.

Pia mechi ya Simba na KMC nayo ingeingia kwenye rekodi ya mechi ambazo magoli yake yamepatikana kwenye dakika za majeruhi.

Mwandishi wa makala haya ameorodhesha magoli yaliyofungwa kwenye dakika hizo kwenye mechi za Ligi Kuu msimu huu.

**1. Mbao 1-1 Alliance (dakika ya 90)**

Ilikuwa ni moja ya mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Agosti 24, mwaka huu, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

Mbao ilianza kupata bao dakika ya 11 na lilionekana kama lingedumu kwa dakika zote 90.

Ilipofikia dakika ya 90, beki wa Mbao, Ibrahim Said, alijifunga mwenyewe dakika hizo za mwisho na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya goli 1-1.

**2. Mtibwa 1-3 Prisons (dakika ya 90+1)**

Mechi ilichezwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro Septemba 25 mwaka huu.

Prisons ilianza kupata mabao yaliyofungwa na Benjamin Asukile na Salum Kimenya, lakini Issa Kajia alipatia Mtibwa Sugar bao la kwanza baadaye.

Mtibwa ikawa inashambulia mfululizo kwa nia ya kusawazisha bao, angalau itoke na pointi moja nyumbani.

Haikuwa hivyo, kwani dakika ya kwanza tu ya nyongeza, Ezekia Mwasindili aliipatia Prisons mabao ya tatu na kuiua Mtibwa nyumbani kwa mabao 3-1.

**3. Ruvu Shooting 1-1 Coastal (dakika ya 90+5)**

Hili ndilo goli lililochelewa zaidi kati ya yote yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa msimu huu.

Lilifungwa dakika ya tano ya nyongeza kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani kwenye mechi kati ya wenyeji, Ruvu Shooting dhidi ya Coastal Union

Wageni walikuwa wametangulia kupata bao dakika ya 60 lililofungwa na Menzi Chilli.

Alikuwa ni Saadat Mohamed aliyeiokoa timu yake na kipigo cha nyumbani wakati mashabiki wote wakiamini kuwa Ruvu ingepoteza, mechi ikaisha 1-1.

**4. Mwadui 1-1 Mbao (dakika ya 90+3)**

Bao la dakika ya 58 liliipeleka Mwadui hadi dakika ya 90 kuongoza kwa bao 1-0 dhidi ya Mbao FC kwenye uwanja wake wa nyumbani, Kambarage mjini Shinyanga Septemba 28, mwaka huu.

Dakika ya tatu ya nyongeza Chilo Nsohela alizima ndoto za Mwadui kutokana na pointi zote tatu nyumbani baada ya kusawazisha bao na kufanya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

**5. Azam 2-1 Namungo FC (dakika ya 90+1)**

Ilikuwa ni Oktoba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex wakati wenyeji wakicheza dhidi ya Namungo FC.

Wageni walitangulia kwa bao la Lucas Kikoti dakika ya 48, lakini Donald Ngoma aliisawazishia Azam dakika ya 61.

Wakati kila mmoja akiamini kuwa ngoma droo, Frank Domayo, alifunga bao la pili dakika ya kwanza ya nyongeza na mechi kumalizika kwa Azam kushinda mabao 2-1.

**6. Mwadui 2-2 JKT Tanzania (dakika ya 90+2)**

Mechi ilichezwa Uwanja wa Mwadui Complex baada ya kuruhusiwa kutumika na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Ilikuwa ni Oktoba 22, Mwadui ilipotoka sare ya bao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania.

Hata baadhi ya taarifa kwenye michezo zilitangaza kuwa JKT Tanzania ilifungwa mabao 2-1, lakini haikuwa hivyo.

Bao la dakika ya pili ya nyongeza lililofungwa na Najim Magulu, liliiokoa na kipigo hicho na kutoka sare ya kibabe ya mabao 2-2, kwani magoli yote mawili yaliingia kwenye dakika za mwisho.

Dakika ya 90, Edward Songo alipachika bao la kwanza kabla ya Magulu kumaliza kazi.

Kabla ya hapo, Mwadui ilikuwa imetangulia kwa mabao mawili yaliyofungwa na Gerald Mathias na Hassan Kapalata.

**7. Mbao 1-2 Mbeya City (dakika ya 90+3)**

Ni mechi ya kukumbukwa iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba Oktoba 28, mwaka huu kati ya Mbao FC dhidi ya Mbeya City.

Mbeya City ilishinda ugenini kwa mabao 2-1, lakini ililazimika kutoka jasho, machozi na damu.

Ilitangulia kwa bao la penalti lililofungwa na Peter Mapunda dakika ya 48. Dakika ya 90, Emmanuel Charles aliisawazishia Mbao bao na kuonekana kama ingeisha kwa sare.

Faulo iliyopigwa na Mapunda dakika ya tatu ya nyongeza ilikwenda moja kwa moja hadi wavuni na kuimaliza Mbao.

**8. Namungo 1-3 Coastal Union (dakika ya 90+4)**

Ni mechi ambayo Namungo ilipoteza nyumbani kwa mabao 3-1 dhidi ya Coastal Union Novemba 22 mwaka huu.

Wakati wenyeji wakihangaika angalau kusawazisha bao kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, beki wa Simba anayeichezea Namungo kwa mkopo, Paul Bukaba alijifunga mwenyewe na kuipatia Coastal bao la tatu dakika ya nne ya nyongeza na kuzima ndoto za kusawazisha.

Awali Namungo ilikuwa nyuma kwa mabao 2-1, ya Mtenje Juma na Deogratius Antony, Renatus Lusajo akiifungia Namungo.

**9. Kagera Sugar 1-3 Mtibwa Sugar (dakika ya 90+3)**

Bao la dakika ya tatu ya nyongeza lililofungwa na Haruna Chanongo liliwezesha Mtibwa Sugar kuichapa Kagera Sugar nyumbani kwao, Kaitaba Novemba 26, mwaka huu.

Lilikuwa ni bao la tatu, lililoivunja nguvu Kagera Sugar iliyokuwa ikishambulia kutaka kusawazisha bao.


Kabla ya hapo, Chanongo alifunga bao dakika ya 78, Juma Nyosso, akijifunga mwenyewe, na Awesu Awesu akiifungia Kagera Sugar bao.

**10. Yanga 1-1 KMC (dakika ya 90+3**

Tayari baadhi ya mashabiki wa Yanga walikuwa wameshatoka nje ya Uwanja wa Uhuru wakijua timu yao imeshapata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 72 lililofungwa na Mrisho Ngasa. Kosa la beki, Kelvin Yondani, dakika za majeruhi kumwangusha, Hassan Kabunda, lilisababisha mkwaju wa penalti uliowekwa wavuni dakika ya tatu ya nyongeza na Abdul Hirally na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

**NAJUA WAJUA**



STRAIKA mpya wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, aliifungia klabu hiyo mabao 42 katika mechi 61 alizoichezea katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi 2012. Pia baada ya kujiunga na LA Galaxy Machi mwaka jana, amefunga magoli 53 katika muda wote aliokuwa hapo.

SOKA




# NYOTA 5 ARTETA

## ANAOTAKIWA KUWAPIGA BEI ARSENAL

**LONDON, England**

BAADA ya Mikel Arteta kuchukua mikoba ya kuinoa Arsenal, mchezo wake wa kwanza ulikuwa dhidi ya Bournemouth kwenye Ligi Kuu England na matokeo yalikuwa ni sare ya kufungana bao 1-1.

Mhispania huyo jana Jumapili alikuwa na mchezo wake wa pili ambao ni 'dabi' ya London wakati Chelsea ilipokwenda kwenye dimba la Emirates kucheza na Arsenal.

Hata hivyo, kama Arteta atataka kumaliza vizuri msimu huu ni lazima aingie sokoni Januari na kuuza nyota wake ambao hawafanyi vizuri na pia kusajili wengine.

Kuna namba kwenye kikosi chake hicho ambazo hazifanyi vizuri na atahitaji kuimarisha kikosi chake.

Hata hivyo, kama atataka kufanya usajili muhimu, ni lazima kwanza awauze wachezaji wake wengine.

Makala hii inakuchambulia wachezaji watano ambao Arteta atalazimika kuwauza kipindi cha dirisha dogo la Januari.

Granit Xhaka

Yupo kwenye mgogoro na mashabiki wake baada ya kile kilichotokea Oktoba mwaka huu kwa kuwaonyesha ishara iliyowaudhi wakati wakimzomea, na ni wazi kwamba Granit Xhaka bado hajasamehewa na mashabiki wa timu hiyo.

Kiungo huyo alipokonywa unahodha wake kwa tabia yake hiyo ya kubishana na mashabiki wakati Arsenal ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 dhidi ya Crystal Palace, tukio ambalo kwa namna yoyote bado limebakia kwenye mioyo yao.

Bila shaka tabia ya Xhaka imemfanya kutokuwa kwenye mioyo ya mashabiki wa Arsenal kwa sasa.

Hata hivyo, kiwango chake nacho hakieleweki tangu atue hapo jijini London, mara zote timu inakuwa haina matokeo mazuri wakati raia huyo wa Uswisi akiwa dimbani.

Hivyo, kwa wakati huu washika bunduki hao watalazimika kumuuza Xhaka kabla ya mambo mengi zaidi hayajatokea.

Imeripotiwa kwamba Hertha Berlin wamefikia makubaliano ya kumsajili na Arsenal watakuwa wamefanya jambo la maana kumuuza kwenda kwa miamba hao wa Bundesliga.

**Shkodran Mustafi**

Ni rahisi kusema kwamba, usajili wa pauni milioni 36 wa kumnunua Shkodran Mustafi ulikuwa mbaya zaidi katika historia ya usajili wa Arsenal.

Kiwango chake tangu kutua hapo kwenye dimba la Emirates hakieleweki. Washikabunduki hao walitakiwa kumuuza wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Arsenal lazima wakubali kwamba hawataweza kurudisha fedha zao walizomnunulia, amekuwa akitajwa kuwaniwa na Valencia na kama Mustafi ataondoka haraka. Arteta atakuwa na nafasi nzuri ya kukijenga kikosi chake upya.

**Calum Chambers**

Calum Chambers sio beki mbaya wa kati, lakini hawezi kuwa bingwa wa Ligi Kuu England kwa ubora wake. Pengine hajawahi kuwa na ubora wa kucheza Ligi ya Ulaya.

Arsenal wanatakiwa kuachana na Mwingereza huyu ambaye amekuwa na timu hiyo tangu mwaka 2014 baada ya kutua hapo akitokea Southampton kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 16.

Wakati alipojiunga nao, Chambers alikuwa bado mdogo na kuonekana kuwa na matarajio nae makubwa. Ni kweli kwamba, amekuwa na kuimarika, lakini ni wazi anatakiwa kucheza katika timu nyingine.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kamwe hajawa kwenye ubora wake. Ni wakati muafaka kwa washika bunduki hao kumuuza na kutafuta wachezaji wengine wa kuimarisha safu yao ya ulinzi.

**Konstantinos Mavropanos**

Kwa kipindi cha misimu yake miwili aliyokuwa mchezaji wa Arsenal, Konstantinos Mavropanos amecheza mechi za maana nne za Ligi Kuu kwa klabu hiyo. Kama ilivyo kwa Chambers, yeye ni mmoja wa wachezaji ambao hatakuwa na msaada wowote kwa kikosi cha washikabunduki hao wa London.

Ni ukweli kwamba, beki huyo wa kati anakosa ubora wa kutoa changamoto kwenye kikosi hicho. Ushindani wa namba kwenye kikosi hicho ni wazi kwamba utamfanya Arteta kuangalia wachezaji wengine na Mavropanos hawezi kuwa msaada.

Kama raia huyo wa Ugiriki atauzwa Januari, fedha ambazo Arsenal watazipata zinaweza kuwasaidia kununua beki bora katika kikosi hicho, kuliko kuendelea kuwa na wachezaji wengi wasio na msaada.

Inatakiwa kuwa wazi kwamba, Arteta anaangalia namna gani ya kukiimarisha kikosi chake. Amerithi kikosi ambacho beki yake ni mbovu, na itamchukua muda wa kubadilisha mambo kabla ya kila kitu kuwa sawa.

**Joe Willock**

Joe Willock ameikumbusha Arsenal mchezaji aliyelelewa na akademi yao, Kieran Gibbs. Sio kwa staili yake ya uchezaji, lakini kwa namna ambavyo makocha wa klabu hiyo walivyomchukulia.

Inaonyesha wazi kwamba, wanaona ni ngumu kwa mchezaji huyo kuwa bora na kujivunia nyota waliomlea wao wenyewe, kwa sababu amekuwa kwenye akademi yao tangu akiwa na umri wa miaka mitano.

Hii ni dunia inayohitaji wachezaji wa daraja la juu kabisa. Lakini kwake inaonyesha kuwa, Arsenal haimhitaji mchezaji aina ya Willock. Ni wazi kwamba hataweza kuwa mchezaji mzuri kwa timu hiyo.

Kwa namna yoyote, Arsenal wanatakiwa kuachana nae na kumuuza katika kipindi cha dirisha dogo la Januari.

NDANI YA 18



YANGA imekuwa timu ya kwanza kupata ushindi dhidi ya Maafande wa Tanzania Prisons katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Bao pekee lililofungwa na Patrick Sibomana liliwapa ushindi Yanga.

Nipashe
Spotika




SOKO la Ulaya kwa sasa linaonekana kutawaliwa na vijana wengi ambao wanapenya kiurahisi katika vikosi vya kwanza, licha ya umri wao kuwa mdogo. Wanabeba majukumu uwanjani kama vile ni wachezaji wakongwe.

Uk. 16-17

# MOURINHO NA MIPANGO MIPYA KUIBEBA SPURS

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, José Mourinho, amekiri kwamba kikosi chake kitaangalia namna ya kutumia fedha nyingi wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari, kwani kwa kufanya hivyo, ndio klabu hiyo itaweza kufanya kazi vizuri.

Spurs kwa kawaida haina heshima kubwa ya kutumia fedha nyingi za kuingiza sokoni kufanya usajili mkubwa.

Hadi sasa wameweka rekodi ya usajili mkubwa zaidi wakati walipomnunua kiungo Mfaransa, Tanguy Ndombele, kwa kiasi cha pauni milioni 54 wakati wa dirisha la majira ya joto.

Lakini kuna kipindi walipita madirisha mawili ya usajili bila kusajili mchezaji yoyote kwenye kikosi chao cha kwanza.

Hata hivyo, kuwasili kwa Mourinho kukaibua uvumi kwamba, atafanya usajili ghali wa wachezaji wanne au watano katika kikosi chake.

Na hii yote ni kwa ajili ya kuhakikisha wanakuwa na kikosi bora chenye ushindani kwenye mashindano yote.

Hii maana yake kwamba, Mourinho anataka kujenga utamaduni mpya ndani ya kikosi hicho kwa kuhakikisha kwamba wanafanya usajili mkubwa kama timu nyingine za Ligi Kuu England.

"Mimi nipo hapa Tottenham Hotspur. Naijua historia ya klabu, najua miradi yake, najua mtazamo wake, najua malengo yake na najua kwamba kwenye soka la usajili tutakwenda kuangalia mambo yanavyotokea na nini kinaweza kufanyika ili kitusaidie wakati wa usajili," anasema Mourinho.

"Kama kuna wachezaji wataondoka, tunahitaji kuzoea hali hiyo na namna ya kukabiliana nayo kwa haraka.

"Lakini hatutakuwa wafalme wa soko, tutaangalia mahitaji muhimu kwa kikosi, hatutaweza kupigana na klabu ambazo zipo tayari kihistoria na falsafa kutumia fedha nyingi. Sisi tutaangalia mahitaji muhimu tu kwa wakati huo."

Kiukweli, Mourinho amezungumzia kiuwazi tu tangu atue hapo malengo yake ya kufanya kazi na kikosi chake cha sasa na aliongeza kuwa anaamini wachezaji waliopo wana uwezo mkubwa wa kubadiilisha mambo.

"Tunahitaji kufanya mambo yetu kwa kutumia akili kubwa, kuwa wabunifu na kuwatumia wachezaji ambao nilionao kwenye kikosi.

"Kwa zaidi ninavyoendelea kufanya kazi, ndivyo ninavyozidi kuwajua zaidi, na zaidi ninavyowaelewa na kuutambua ubora wao pamoja na matatizo waliyonayo.

"Nimekuwa nikisema kwamba, nahitaji muda na huo muda hivi sasa ndio unakuja. Sio kuanzia.

"Lakini Januari, na Februari tutakuwa na muda zaidi wa kujaribu kuimarika kama timu. Najua namna ya kumaliza matatizo ya klabu, lakini kwa asilimia 100 nitachukua vile vitu bora kwa kikosi ambavyo tunataka kuwa navyo na kuendelea kuimarika kama timu.

"Na halafu kuna jambo gumu zaidi tutatakiwa kulifanya, kuhakikisha tunacheza bila kuruhusu bao.

"Tutakachofanya kwanza, ni kuhakikisha tunacheza mechi bila kuruhusu bao na hii maana yake ni kwamba, tutahitaji kuimarisha safu ya ulinzi, kiungo pamoja na ushambuliaji.

"Hili ni jambo ambalo naliona linawezakana kwa haraka tu, maana tukijipanga kama timu na kuangalia wapi pa kumaliza tatizo kwa haraka, naamini haitakuwa ngumu kwetu kucheza mechi bila kuruhusu bao.

"Na hiyo ni lazima kwanza tuue matatizo yote ya timu na kujipanga upya kama kikosi cha ushindani.

"Kitu kigumu ni kufanya hivyo pamoja na wachezaji ambao ni wale wale na wenye tabia zile zile za mwanzo; jambo jingine gumu ni kujenga safu imara ya ulinzi bila kupoteza umahiri wa washambuliaji wetu.

"Lakini naamini hili litawezekana, maana naona wachezaji waliopo ni rahisi kuwabadili falsafa na kuwaongeza wengine wachache ambao tunamahitaji nao."




Simeone

**USILOLIJUA**



TIMU ya Taifa ya Ufaransa maarufu Les Blues ilicheza mechi yake ya kwanza kwenye Uwanja wa Stade de France Januari 28, mwaka 1998 na ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Hispania, mfungaji wa bao hilo pekee alikuwa ni Zinedine Zidane.



# Wananchi walia barabara kufungwa

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

WANANCHI wa baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Chunya na Mkoa wa Tabora wanaotumia barabara ya Mbeya - Tabora, wameiomba serikali kusitisha uamuzi wake wa kuifunga barabara hiyo kutokana na kuvunjika kwa daraja la Mto Lupa na baadhi ya watu kupoteza maisha wakati wanavuka.

Waliiomba serikali kuwaruhusu waendelee kutumia barabara hiyo kwa kuvuka chini kwenye daraja la muda ambalo mkandarasi anayejenga barabara hiyo kuanzia Chunya Mjini mpaka Makongolosi amelitengeneza kwa ajili ya kuvusha mizigo yake na kwamba watachukua tahadhari kwa kusubiri maji yapunguwe.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya kuifunga barabara hiyo na kuamuru magari yote kuzunguka njia ya Mkwajuni wilayani Songwe, wananchi hao walisema njia hiyo mpya itawaumiza kutokana na nauli kupanda.

Mmoja wa wananchi hao, Ernest Daud ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Matundasi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, alisema serikali ilifunga barabara hiyo bila kuwasikiliza maoni yao.

Alisema barabara ya Mkwajuni mbali na kuwa ndefu, pia nako kuna daraja ambalo lina ufa na kuna hatari likakatika na kusababisha maafa hivyo akaomba waendelee kuitumia barabara yao ya zamani.

"Wiki mbili ambazo mkandarasi amepewa ni nyingi sana, hii barabara kwetu ni muhimu hivyo tunaomba serikali impe mkandarasi hata siku tatu atengeneze usiku na mchana kwa dharura maana hiyo ya njia ya Mkwajuni na kwenyewe kuna daraja liko hatarini kukatika," alisema Daud.

Naye Elizabeth Jeremiah mkazi wa Matundasi, alisema wameingiwa na hofu ya kuwasafirisha wagonjwa kutoka katika maeneo yao endapo itatokea wakapewa rufani kwenda Hospitali ya Wilaya ama ya Mkoa.

Alisema wajawazito ndio itakuwa changamoto zaidi, hivyo akaomba serikali iruhusu barabara hiyo kutumika kwa matukio ya dharura ikiwamo ya kuwakimbiza wagonjwa kwenda wilayani.

Alisema kwa barabara ya kuzunguka Mkwajuni ni ndefu sana na kwa sasa wanahofia hata nauli ya kufika Mbeya Mjini itaongezeka kutokana na ongezeko la urefu ambao haukuzoeleka.

Diwani wa Kata ya Matundasi, Kimo Choga, alisema wananchi wa kata zote za Mji Mdogo wa Matundasi wanategemea huduma nyingi Chunya mjini na hivyo kufungwa kwa barabara hiyo kutawaathiri kwa kiwango kikubwa.

"Kuna wananchi wangu wapo hapa jirani tu na mto, lakini wanategemea huduma kwenye maduka ya upande wa pili, sasa mimi nakubaliana na serikali kuifunga badrabara, lakini wiki mbili ni nyingi sana angalau ingekuwa hata wiki moja," alisema Choga.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kuifunga barabara hiyo, aliwataka wananchi wa maeneo hayo kutothubutu kuvuka kwenye maji kama walivyokuwa wanafanya awali kwa maelezo kuwa atawachukulia hatua kali za kisheria.

Alisema magari yote yanatakiwa yapite njia ya Mkwajuni ambayo umbali unaoongezeka ni kilimita 16 pekee na hivyo ni bora wapite huko kuliko kukatarisha maisha kwenye mto huo ambao tayari umeshaleta maafa.

"Sasa nimempa mkandarasi wiki mbili alirejeshe daraja katika hali yake ya awali ili barabara ifunguliwe na asipotekeleza nitamsweka ndani, hatuwezi tukawa tunahangaika wakati daraja wameharibu wenyewe," alisema Chalamila.

Hivi karibuni mmoja wa wananchi waliokuwa wanavuka kwenye mto huo kwa miguu, alisombwa na maji na akapoteza maisha, huku wengine wakinusurika kwa kuokolewa na waogeleaji na hivyo serikali ikaamua kuifunga b



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Chalangwa, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wakiwa wamewabeba watoto wao, wakijiandaa kuingia kwenye chumba cha kupimia watoto, ikiwa ni maudhurio ya kliniki katika kituo cha afya cha kata hiyo. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wamiliki wa shule binafsi wafundwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

WAMILIKI wa shule binafsi nchini wametakiwa kuendesha shule zao kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa na kujiepusha na udanganyifu kwenye mitihani ya kitaifa utakaosababisha kuwa na vijana wasio bora kitaaluma.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari ya Airport ya jijini Mbeya, Nikuswiga Malambugi, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kutokana na hatua yake ya kumzawadia mwanaye bango kubwa lililoleta gumzo kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni lililokuwa likisomeka 'Hongera Ayubu.N.Malambugi kwa kuhitimu na kupata shahada ya kwanza ya elimu Chuo Kikuu cha Dodoma'.

Malambugi alisema ni muhimu wamiliki hao kuwa waaminifu kwenye mitihani na ufundishaji ili kupata vijana ambao watakuwa waaminifu na waadilifu kwa Taifa lao. "Niwasihi wamiliki wenzangu tufanye kazi kwa nidhamu ya hali ya juu na kujali wateja na tusiende kinyume cha taratibu zozote za uendeshaji wa shule hasa zile za kufanya udanganyifu kwenye mitihani, hichi ni kitu ambacho sikipendi na kinaniudhi kwa baadhi ya wamiliki wa shule wachache," alisema.

Alieleza kufanya udanganyifu hakujengi vijana bora bali wanaharibu na kutengeneza picha mbaya ya maisha yao ya baadaye.

"Hii shule ni miongoni mwa shule bora za mfano hapa Mbeya kwenye nidhamu ya mitihani ya kitaifa, Wizara ya Elimu mwaka 2015 ilitutunuku hati kwamba ni shule moja wapo inayoonesha mafanikio kitaaluma na kimiundombinu," alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo inatokana na miongozo na taratibu alizoweka ambazo walimu wanafuata na kuisimamia

Hata hivyo, aliomba serikali kuendelea kuwa karibu na wamiliki wa shule hizo kuwasaidia ikiwamo kutoa ruzuku ili watoe elimu bora kwa vijana wa kitanzania.

"Hata sisi shule binafsi tunakaguliwa ubora wa shule na kutoa miongozo ili kuboresha taaluma, sasa kutokana na shule za serikali kuboreshwa na ufundishaji kuwa wa kiwango kizuri ikilinganishwa na miaka iliyopita, hali inayozifanya shule binafsi kuweka mkazo zaidi ili kumudu soko la ushindani," alisema.

Akizungumzia bango alilompa Ayubu, Malambugi alisema aliamua kumpatia zawadi ya bango kama kumbukumbu kwake na motisha kutokana na kuhitimu masomo yake.

"Ayubu si mtoto wangu wa kwanza kupata shahada, ni mtoto wa tano, hivyo nilitoa zawadi hii kumpa moyo na kuwapa mwamko wa kusoma wenzake ili kufikia hatua mbalimbali za elimu," alisema.

# Shida ya barabara mtihani kwa diwani

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

DIWANI wa a Igurusi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Hawa Kiwele, amesema changamoto ya barabara katika kata yake imekuwa sugu.

Kiwele alisema tatizo hilo limedumu kwa zaidi ya miaka 14 hasa kipande chenye urefu wa kilomita tatu katika Kijiji cha Mapunga ambacho wananchi wameanza kuchimba kwa kutumia jembe la mkono baada ya kuona serikali inasuasua kutengeneza.

Kiwele alisema barabara hiyo awali shida kubwa ilikuwa ni makalavati ambayo yaliyowekwa yalikuwa hayana viwango hivyo maji yakawa yanatwama barabarani na kusababisha isipitike kirahisi.

Alisema awali alikuwa diwani wa viti maalumu, na walikuwa wanaahidiwa kujengewa kwa viwango vizuri, lakini mpaka sasa bado ni tatizo kwa wananchi wake.

"Hata mimi natamani siku moja hii barabara iwe bora ili wananchi wangu wasafiri na kusafirisha vitu vyao bila kukwama sehemu yoyote, kwa sasa kuna sehemu madimbwi yamejaa barabarani na magari yakiingia yanakwama," alisema Kiwele.

Nao baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walisema barabara hiyo ni muhimu kwao na ndiyo wanayoitegemea kwa ajili ya kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kupeleka nyumbani na kupeleka kwenye masoko.

Yorodani Mbaye, alisema awali waliahidiwa kuwa serikali ingejenga barabara hiyo, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea zaidi ya kibao kuwekwa karibu na barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) ambapo barabara hiyo inajengwa na serikali.

Alisema waliwahi kuletewa makatapila na serikali yakachimba kidogo na kuacha kwa maelezo kuwa bajeti ilikuwa imeisha na hivyo hayajatokea tena ndio maana wakaamua kuichimba kwa jembe la mkono.

"Tunaiomba serikali itusaidie maana imekuwa ikituahidi kwa muda mrefu, kwa sasa kuna baadhi ya maeneo hata pikipiki hazipiti na hivyo ni vigumu kusafirisha hata wagonjwa kwa dharura," alisema Mbaye.

Naye Neema Msanzala alisema kutokana na makorongo yaliyopo katika eneo hilo, baadhi ya wajawazito wamekuwa wakikwama na kujifungulia katika eneo hilo baada ya pikipiki kushindwa kupita.



# Elimu ya rushwa kwa shule za msingi, vyuo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) mkoani Dodoma, imepanga kuanza kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo na shule za msingi jinsi ya kuepukana na rushwa ya ngono katika maeneo yao ya kazi.

Aidha, Takukuru Dodoma imeweka mikakati ya kutumia klabu za wapingarushwa zilizopo vyuoni na shuleni ili kuhakikisha wanasaidia kuibua na kutokomeza rushwa ya ngono katika maeneo waliopo.

Akizungumza na gazeti hili, Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema moja ya mikakati iliojiwekea kupambana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi shuleni na vyuoni ni kuanza kutoa elimu kwa walimu wa vyuo na shule ili wasaidie kutoa elimu kwa wanafunzi wao.

"Kupitia kampeni ya Vunja Ukimya Kataa Rushwa ya Ngono Takukuru Dodoma tutaitumia vema kuwaelimisha walimu wa msingi na vyuo ili nao wasaidie kuwafundisha wanafunzi kuhusu madhara ya rushwa ya ngono, "alisema Kibwengo.

Alisema wanaamini elimu itakayotolewa itakuwa msaada mkubwa na kuhakikisha matukio mengi kuripotiwa ili yafanyiwe kazi.

Kutokana na hilo, alisema wao Takukuru wamejipanga kuhakikisha mwakani wanafanikisha kampeni hiyo kwa vitendo ikiwamo kutoa mafunzo ili kuhakikisha wanapata elimu kuhusiana na rushwa ya ngono vyuoni na shuleni.

Alisema lengo lao ni kuona rushwa ya ngono inatokomezwa kama mkakati uliowekwa wa kuhakikisha rushwa na ukatili wa kijinsia unatokomezwa.

Alisema Takukuru Mkoa wa Dodoma imedhamiria kutilia mkazo kampeni ya vunja ukimya ili kupata vijana ambao wataelewa suala la rushwa na kusaidia kuvunja ukimya ambao wengi wa waathirika wa matukio hayo huogopa kusema.

Kibwengo alisema watu wenye mamlaka waache kutumia nafasi zao kuomba rushwa ya ngono, na kuongeza kuwa ana imani kampeni hiyo itafanikiwa na kuibua matukio ya rushwa ya ngono ambayo yamejificha.

Akizungumzia kuhusu kampeni ya 'Vunja Ukimya', alisema wamejipanga kuanzia mwakani kuitangaza ili iweze kufahamika na kutumiwa na jamii ili kutoa taarifa dhidi ya utokomezwaji na upambanaji wa rushwa ya ngono.

Alisema kampeni hiyo ni muhimu sana kila mmoja kuifahamu hivyo wao kama Takukuru wana kila sababu ya kuitangaza ili jamii ijue na kuifanyia kazi.

Alisema wengi wa jamii hawajui kampeni hiyo hivyo kupitia klabu za wapinga rushwa watawatumia kuelimisha jamii juu ya suala la kukataa rushwa ya ngono.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Dodoma, wakizima moto kwenye vibanda vilivyokuwa vikiteketea vya wafanyabiashara wadogo katika soko la Sabasaba jijini humo jana. **PICHA PETER MKWAVILA.**

# Ombi kuwasaka vigogo wa Viguta

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

ALIYEKUWA Meneja wa Umoja wa Vikoba Tanzania (VIGUTA) akiwawakilisha wananchi wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Hilda Kadunda, ameiomba serikali kutumia vyombo vyake kuwasaka vigogo wa Viguta Taifa na kuwafilisi mali zao kwa tuhuma za kuwatapeli wananchi.

Kiongozi huyo ambaye ni Diwani wa Viti Maalum CCM Kata ya Loje wilayani Chamwino, amesema kuwa shirika hilo limewasababishia hasara wananchi wengi ambao walijiunga nalo.

Akizungumza na vyombo vya habari wilayani Chamwino mkoani hapa, Hilda alisema kuwa Viguta waliingia kwa sura ya kuonekana kama wakombozi kwa wananchi wa hali ya chini kwa ahadi kuwa watawajengea nyumba kwa bei nafuu na wale wote ambao ni wanachama watalipa kidogo kidogo, lakini wameshindwa kufanya hivyo.

Alisema kuwa Viguta waliwashawishi wananchi kuwa watajengewa nyumba kwa bei nafuu kulingana na thamani halisi ya nyumba au kiwanja kwa kulipia asilimia kumi na kuendelea kulipa kidogo kidogo kwa muda miaka mitano.

Hilda alisema kuwa Viguta hawakuweza kutimiza mikataba yao kwa wananchi matokeo yake viongozi wake wamewakimbia wananchi na kuwaachia mzigo ambao walikuwa wakiwasimamia wananchi katika kujiunga na Viguta katika maeneo yao.

Akielezea alishawishika kujiunga na Viguta na kuwa msimamizi wa wananchi kutokana na Viguta walivyojitambulisha na kujiaminisha mbele ya Bunge kwa ushawishi mkubwa kuwa wanaweza kuwa wakombozi kwa wananchi wa kipato cha chini.

"Viguta waliingia Chamwino kama sehemu ya wakombozi wa wanyonge na kila mmoja aliamini kuwa atafaidika kupitia kwao na ukizingatia walijitambulisha hadi bungeni kwa maana kama watu wamepitia mhimili mkubwa kama huo kwa kawaida hauwezi kuwa na shaka nao," alisema na kuongeza kuwa:

"Kutokana na imani hiyo, watu walihamasishwa na wakahamasika na walikuwa wakijaza fomu ya maombi ambapo walikuwa wakilipia Sh. 15, 000 na kulingana na thamani ya nyumba au kiwanja walikuwa wakilipia asilimia 10 na baada ya kukamilika kwa nyumba waliahidiwa kulipa kidogo kwa miaka mitano," alisema.

Aidha, alisema cha kushangaza Viguta hawakuweza kutimiza walichokiahidi kwa wananchi, na walikuwa wakikusanya fedha kutoka kwa wanachama na zote zilipitia kwenye akaunti zao, lakini mwisho viongozi wote wameingia mitini na kuacha vurugu kubwa kwa waliokuwa wasimamizi.

## Vijana waaswa kuchangamkia fursa kujiajiri

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Maendeleo ya Vijana mkoani Dodoma (DOYODO), Rajabu Nh'unga, amewataka vijana kuzitambua fursa mbalimbali zilizopo kwenye maeneo yao ili kujiajiri.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na vijana wa skauti mkoani hapa walipotembelea ofisi za taasisi hiyo zilizopo jijini hapa.

"Doyodo ni Taasisi yenu, hivyo wakati wowote mnakaribishwa kufika hapa kupata ushauri au kujadiliana ili kuhakikisha tunajikwamua kiuchumi kundi letu la vijana," alisema.

Nh'unga aliwataka vijana nchini kutambua na kuchangamkia fursa zilizopo kwenye maeneo yao ili kujiajiri katika sekta hizo na kuacha kutegemea kuajiriwa.

Hata hivyo, aliwapongeza vijana hao wa skauti nchini kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kujitolea katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ya taifa.

Alisema lengo la kikao hicho ilikiwa ni kuimarisha ushirikiano na mshikamano wenye tija kwa taasisi hiyo na vijana hao wa skauti ili kuwajengea uwezo wa kujiendeleza kiuchumi.

Aliongeza kuwa vijana hao wanafanyakazi za kujitolea lakini wanatakiwa kuongeza bidii ya kujitafutia uchumi kwa kubuni miradi mbalimbali ya kujiajiri.

Kadhalika, aliwataka kuzitumia changamoto zilizopo za kundi la vijana zilizopo kwenye maeneo yao kama fursa ili kuondokana na malalamiko kudai hakuna kazi. Mwenyekiti wa Jukwaa la Skauti Dodoma, Ibrahimu Mwinyimvua, alisema walifika hapo kuwasilisha ripoti ya utendaji wa Mwaka 2019 pamoja na kuelezea kazi za Jukwaa hilo.

Mwinyimvua alisema sababu za kuwasilisha taarifa hapo ni kuwashirikisha taasisi hiyo kazi wanazofanya katika jamii pamoja na za kitaifa.

Alisema skauti mkoani hapa wamekuwa wakishiriki katika kazi za ujenzi wa taifa pamoja na usafi wa mazingira na kuelimisha vijana wengine ili kufanyakazi.

Alibainisha kuwa wataendelea kuonyesha nidhamu ya hali ya juu katika jamii ili kuwavuta wengine kujiunga na kundi hilo la kujitolea.





# Akihamasisha kikundi Saccos kuwa benki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi, Ahmada Yahya Abdulwakil, amesema ushirika wa akiba na mikopo Meli Nne Saccos, una nafasi kubwa ya kujiinua na kuwa benki kamili.

Akifungua mkutano mkuu wa 10 wa ushirika huo uliofanyika mjini hapa, Yahya alisema kutokana na maendeleo yaliyofikiwa, Meli Nne Saccos ndiye baba wa vyama vya ushirika kote nchini.

Alisema ushirika huo ni mfano wa kuigwa, kwa kuwa umjijengea heshima kubwa mbele ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia maadili na uaminifu kwa wanachama wake.

Alisema kutunisha mtaji wa Saccos hiyo na kufikia zaidi ya shilingi bilioni mbili, si jambo dogo na inafurahisha kuona hadi sasa ushirika huo haujafilisika. "Kwa sheria mpya ya vyama vya ushirika, si muda mrefu mnaweza kufikia hadhi ya benki kamili mtakapofikisha mtaji wa shilingi bilioni tatu, jambo ambalo ninaamini kwa mlivyojipanga mnaweza," alisema. Alieleza kuwa, hali hiyo pia ilimvutia Waziri Mkuu wa Tanzania, Majaliwa Kassim, alipomwakilisha Rais John Magufuli siku ya ufunguzi wa ukumbi wa Saccos hiyo.

Aliwataka wanachama wa ushirika huo, kuhakikisha wanachagua viongozi wenye uwezo na uadilifu ili waendelee kuipeleka mbele Saccos yao, ambayo imekuwa tegemeo kubwa kwao katika kujiletea maendeleo na kupambana na umaskini. Mwakilishi huyo pia alikabidhi gari aina ya Noah yenye thamani ya Sh. milioni 12 kwa mwenyekiti wake Ussi Chimbeni, ambayo ushirika huo umenunua hivi karibuni kwa ajili ya kurahisisha utendaji wa shughuli zake.

Naye Mrajis wa Vyama vya Ushirika Zanzibar, Khamis Daud Simba, alisema pamoja na mafanikio tangu kuasisiwa kwake, ushirika huo unapaswa kuongeza bidii na kufanya kazi kwa teknolojia ya kisasa ili kudhibiti taarifa na kuwahudumia wanachama wake wapatao 1,500.

Aliwakumbusha viongozi wa Saccos hiyo wana wajibu wa kujiendesha kwa kufuata sera, sheria na kanuni zilizowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuepuka malalamiko ya wanachama na kuzorota kwa ushirika wao na hatimaye kufa.

Alisema miongoni mwa mambo makubwa ambayo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ni kusimamia kuundwa kwa sheria mpya ya vyama vya ushirika namba 15 ya mwaka 2018, na kuitia saini Desemba 31, 2018.

"Baada ya kusainiwa kwa sheria hii, Wawakilishi walishauri wanaushirika wapewe mwaka mmoja kuizoea kabla kuanza kutumika rasmi, muda huo umekwisha mwezi huu, na juzi tu Waziri Moudline Castico ameisaini," alisema.

Aliwataka viongozi wabadilike na pia wanachama wasisite kuuliza pale wanapoona mambo hayaendi kwa mujibu wa matarajio na mahitaji ya sheria inayosimamia vyama vya ushirika pamoja na sera yake.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Saccos hiyo, Njuma Ali Juma, alisema ushirika huo uliundwa na kupata usajili Desemba 23, 2005 ukiwa na wanachama 150, na sasa wamefikia 1,500, wanawake 957 na wanaume ni 554.

Alisema Saccos hiyo ina vikundi 19 vinavyojishughulisha na shughuli mbalimbali za maendeleo, huku akiba za wanachama zikifikia Sh. 1,203,020,500, amana ni Sh. milioni 57, wakati hisa ni Sh. 60,720,600.

Mkutano huo pia unafanya uchaguzi mkuu wa kuwapata viongozi watakaoshika hatamu kwa kipindi kijacho cha miaka minne, Januari 4, 2020.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akihutubia waumini wa dini ya Kiislamu kwenye Maulidi ya Uzawa wa Nabii Muhammad (SAW) yaliyoandaliwa na uongozi wa Msikiti wa Majumat Islamia uliopo Temeke jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

# Aiasa Tume Haki za Binadamu kusimamia sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalim, ameitaka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kuendelea kusimamia majukumu yao kwa ufanisi kama sheria na mwongozo unavyoelekeza.

Akizungumza na ujumbe kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, mjini hapa, alisema ina majukumu ya kuendeleza na kusimamia masuala ya haki na utawala bora nchini, hivyo ni vyema kusimamia kwa uadilifu.

Khamis aliahidi kuwa Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano wa pamoja na tume hiyo.

Vile vile, alisema wizara itahakikisha taratibu na miongozo inafuatwa katika kusimamia demokrasia, utawala bora na haki za binadamu chini ya utawala wa sheria.

"Katiba na Sheria kwa upande mmoja, na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa upande mwingine ni watoto pacha hivyo ni lazima waungane pamoja kama walivyo ili tuweze kusimamia vyema majukumu ya nchi na kuendeleza amani na mshikamano wa nchi yetu," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alisema jukumu kubwa la tume hiyo ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Alisema katika kutekeleza jukumu hilo, tume inayo mamlaka ya kupokea malalamiko kwa njia mbalimbali na kuanzisha uchunguzi wake endapo itaona kuna uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Alimhakikishia waziri huyo kuwa Tume itafanya kazi kwa uadilifu na kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia taratibu na kufuata katiba na sheria za nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mohamed Khamis Hamad, alisema masuala ya haki za binadamu ni sehemu muhimu inayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria.

# Muungano wajivunia maendeleo kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajivunia maendeleo makubwa ya kiuchumi yaliyopatikana Bara na Zanzibar kutokana na sababu kubwa ya uwapo wa amani na utulivu.

Alisema amani na utulivu huo unawapa wananchi kuwajibika ipasavyo katika harakati zao za kila siku.

Kadhalika alisema kikundi au mtu yeyote atakayejaribu kuhatarisha amani na utulivu huo, mshikamano wa jamii na umoja wa wananchi ni adui na inapaswa kupambana naye.

Balozi Seif Ali Iddi alisema hayo katika hafla ya Maulidi ya uzawa wa kiongozi wa Dini ya Kiislamu Mtume Muhammad (SAW) yaliyofanyika, jijini Dar es Salaam.

Alisema Watanzania wote wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nguvu zake zilizowezesha kupatikana kwa neema ya amani inayoendelea kusimamiwa vyema na viongozi wake wakuu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Di. Ali Mohamed Shein.

Balozi Iddi alisema, juhudi za viongozi hao katika usimamizi wa ujenzi wa taifa chini ya kivuli cha amani, ziko wazi zikionekana kuipaisha Tanzania katika heshima kimataifa. Alisema, viongozi wa aina hiyo waliojitolea nguvu na nafsi zao kwa wale wanaowaongoza, kamwe hawatakosa upinzani na maadui ambao daima hawatakuwa tayari kuridhia juhudi hizo za kuing'arisha dola la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aliwataka waumini hao waliohudhuria Maulidi kila mmoja abebe dhima ya kuwa mchunga mwenzake dhidi ya kupiga vita vitendo viovu.

Alisema vitendo vya udhalilishaji ikiwamo ubakaji, kutelekezwa kwa watoto na talaka zisizofuata utaratibu wa Kiislamu, vinakwenda kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu pamoja na mwenendo mzima wa kiongozi mkuu wa waumini wa dini ya Kiislamu.

Aliwakumbusha wananchi kwamba mwaka 2019 unamalizika na kuingia mwaka 2020 wakielewa kuwa ndio mwaka wa uchaguzi mkuu kwa Watanzania wote ambao ni haki ya kidemokrasia ya kila mwananchi kwa kuchagua au kuchaguliwa.

Balozi Iddi aliwataka wajiandae vyema na uchaguzi huo, huku wakifuata maelekezo ya tume zote mbili za uchaguzi NEC na ZEC wakiweka dhamira moyoni mwao ya kuhakikisha uchaguzi unafanyika na kumalizika kwa salama, huru na haki.

Alisema ni vyema wakati wa kampeni utakapowadia wafuasi na viongozi wa vyama vya siasa wakazingatia kampeni za kistaarabu zitakazoepuka matusi na vurugu ili hatimaye kura zipigwe kwa salama.

Naye Mufti Mkuu wa Tanzania Sheikh Aboubakar Zubeir Ali, alisema Waislamu wakati wote lazima waige kigezo na mwenendo wa Nabii Muhammad (SAW) wa ufasaha uliopambwa na ucheshi katika muda wa maisha yake aliyoishi ya kila siku.

# Wanunuzi korosho Mkuranga kupewa upendeleo

**Na Futuna Seleman,**
MKURANGA

SERIKALI imesema wanunuzi wote wa zao la korosho Mkuranga watapewa vibali maalum vya kusafirisha korosho ambazo ziko chini ya daraja la mwisho ambalo ni daraja la tatu.

Aidha, wanunuzi wengine watawekewa mazingira mazuri kwa sababu wana maghala makubwa kuendelea kuzichambua na kuzikausha ili kuzinyanyua daraja kutoka daraja la tatu kwenda la pili na nyingine kwenda daraja la kwanza kwa lengo la kuendelea kulinda taswira ya nchi.Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba, alipokagua maghala ya korosho Mwanambaya na Mkuranga ili kujiridhisha na kuzipima korosho hizo baada ya kutokea sintofahamu na kutoaminiana baina ya wataalamu wake na wakulima wa korosho Mkuranga, waliolalamikia korosho zao kushuka bei kwa madai kuwa zimeshuka kiwango.

Alisema ziara yake Mkuranga inalenga kujiridhisha na ubora wa korosho kwa kuzipima baada ya kutokea sintofahamu hiyo ambapo ikamlazimu kuambatana na wataalamu wake Bodi ya Korosho uongozi wa Mkoa wa Pwani ili kujiridhisha.

"Kama tunavyofahamu korosho haitaki maji mengi na korosho ikidondoka inatakiwa ianikwe, sasa kutokana na mvua nyingi korosho imeshuka kiwango hivyo kumezuka sintofahamu," alisema.

Alisema korosho nyingi zimepata maji na hazijakauka vizuri, hivyo ubora umeshuka.

"Tutaendelea kulinda taswira ya kiwango çha ubora wa korosho yetu duniani kwa kila mtu duniani, mnunuzi yeyote duniani anafahamu korosho ya Tanzania ni ya daraja la kwanza na la pili... lazima sifa hiyo ya taswira tutaendelea kuilinda ili tusichafuke kuonekana kwamba Tanzania tunazalisha korosho iliyo kiwango cha chini sana," alisema na kuongeza:

"Nawahakikishia wakulima, korosho zao zitauzwa, zitanunulika kutokana na viwango vya ubora vilivyopo na makubaliano ya bei kati yao na wanunuzi wenye nia na dhamira ya kununua korosho hiyo na nitakutana na wanunuzi wote wa korosho Tanzania kuwahakikishia tunawapa vibali vya kusafirisha korosho zenye ubora chini ya kiwango daraja la tatu." Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alisisitiza korosho zote za Mkoa wa Pwani zitauzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Aliwatoa hofu wakulima wa zao hilo kuwa siwao peke yao kupata korosho daraja la tatu kwani hata mikoa ya kusini zipo.

Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega ambaye ni Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, alionyesha kukerwa na hatua ya baadhi ya wakulima wa zao hilo, majina yao kutoonekana katika orodha ya waliopeleka korosho zao ghalani hali inayoweza kusababisha upotevu wa mali zao.

Baadhi ya wakulima walilalamikia ucheleweshwaji wa pembejeo umechangia korosho zao kuharibika ikiwamo uchache wa magunia licha ya kuwapo kwa changamoto ya mvua.




Mwonekano wa barabara za juu zinazojengwa Ubungo jijini Dar es Salaam, ambazo zikikamilika zinatarajia kupunguza msongamano wa magari jijini humo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkulo: Sina mpango kugombea ubunge

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Waziri wa Fedha katika serikali ya awamu ya nne, Mustafa Mkulo, amesema hana mpango wa kugombea ubunge katika Jimbo la Kilosa mkoani Morogoro, kwa kuwa ameshawatumikia wananchi vya kutosha.

Mkulo ambaye alikuwa ni Mbunge wa Jimbo la Kilosa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Morogoro huku akitoa salamu za mwaka mpya wa 2020.

Alisema hajabadilisha maamuzi yake ya kutogombea nafasi ya ubunge na kushangazwa na baadhi ya watu kudai anataka kugombea tena nafasi hiyo, na kwamba hajalifikiria suala hilo kwa kuwa ametumikia vya kutosha.

"Kuna watu wamekuwa wakidai nataka kugombea tena ubunge Kilosa... hizi ni habari za uongo, sina mpango wa kugombea ubunge sehemu yoyote ile hapa nchini," alisema Mkulo.

Mkulo alisema bado anajivunia katika miaka 10 ya ubunge Jimbo la Kilosa kwa kutekeleza ilani ya chama kwa kipindi hicho na wana-Kilosa kuridhika na utendaji wake.

Katika salamu zake za mwaka 2020 Mkulo, alisema anafurahishwa na utendaji kazi mzuri wa Rais wa awamu ya tano, John Magufuli na anaungwa mkono na wana-CCM wengi.

Alisema wataendelea kumuunga mkono katika uchaguzi wa kipindi cha pili ya miaka mitano ijayo wa mwaka 2020 hadi 2025, ili aweze kutekeleza kwa ufasaha mipango ya kimaendeleo aliyoiacha katika awamu ya kwanza.

"Huu ni utaratibu wangu wa kila mwaka kutoa salamu za mwaka mpya tangu nikiwa mbunge na sasa ni wakati wa kusema ukweli Rais Magufuli kwa miaka minne amefanya mengi mazuri, na anahitaji pongezi kutoka kwa Watanzania hasa katika kupandisha uchumi na kuboresha miundombinu ya nchi hii," alisema Mkulo.

Mkulo amekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 10, amewahi kuwa Waziri wa Fedha na mwaka 2015 aliamua kutogombea nafasi hiyo.

# Vikundi vya ujasiriamali vyahimizwa utawala bora

**Na Sabato Kasika**

VIKUNDI vinavyojishughulisha na ujasiriamali vimetakiwa kufanya kazi kwa kufuata mwongozo wa usimamizi shirikishi unaozingatia utawala bora, ili viweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Hayo yalisemwa Dar es Salaam juzi, na mlezi wa Kinondoni Women Development Association (KIWODEA), Thomas Ngawaiya, wakati akizungumza katika hafla ya kuuga na kukaribisha mwaka mpya wa 2020.

Ngawaiya ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo iliandaliwa na kikundi hicho cha Vicoba, alisema, utawala bora ni wa muhimu katika nyanja zote hivyo ni muhimu uzingatiwe.

"Taasisi ninayoiongoza, inajishughulisha na mambo ya utawala bora, hivyo kila ninapopata nafasi, ni lazima niuzungumzie, kwani ndiyo msingi unaoimarisha umoja na mshikamano," alisema. Alisema utawala bora unawafanya wanakikundi waheshimiane bila ubaguzi wa aina yoyote ile, kwa vile maamuzi yanayofanywa ndani ya kikundi yatafuate sera, sheria na kanuni zilizowekwa na kupitishwa na wanakikundi wenyewe," alisema.

Ngawaiya ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA), alikubali ombi la kikundi hicho la kukitafutia eneo la eka 10, ili kiboreshe shughuli za ujasiriamali.

Katibu wa KIWODEA, Salome Damian, alisema, kikundi hicho kilianzishwa mwaka 2013 kutokana na mawazo yaliyotolewa na wanawake wa Kinondoni na kuwashirikisha wanawake wajasiriamali.

Alisema, walikubaliana kwa kila mwanachama kununua hisa moja hadi tano kwa wiki, huku hisa ikiwa na thamani Sh. 2,000, na kwamba wanachama walinunua kwa muda wa miezi mitatu. "Baada ya hapo wanachama walianza kukopeshana kulingana na wingi wa hisa za mwanachama kwa riba nafuu ambayo ni asilimi tano tu. Mfano akikopa Sh. 200,000 kwa miezi sita, riba yake ni asilimia 10," alisema.

Alisema, kikundi hicho kinazidi kukua na kwamba kimefikia idadi ya wanachama 90, na pia kimeongeza thamani ya hisa kutoka Sh. 2,000 hadi 3,000 na mikopo inazidi kuongezeka.

Aidha, alitaja changamoto zinazokikabili kikundi hicho kuwa ni ukosefu wa eneo kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo na pia ukosefu wa wafadhili kwa ajili ya kuwapa nguvu zaidi katika uanzishwaji wa miradi.

## HABARI KIMATAIFA

### Korea Kaskazini yaijadili Marekani

**PYOYANG, Korea Kaskazini**

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, ameendesha mkutano na maofisa wa ngazi ya juu kujadili masuala muhimu ya sera.

Chombo cha habari cha taifa kimeripoti jana kuwa mkutano huo umekuja wakati wa muda wa mwisho wa mwaka uliowekwa na Kim kwa Marekani kutoa unafuu wa vikwazo ukikaribia.

Kikao hicho kilifanyika huku hali ya wasi wasi ikiendelea kuwa juu kati ya nchi hizo mbili kuhusiana na mpango wa Korea Kaskazini wa nyuklia pamoja na majaribio ya mara kwa mara ya makombora.

Kim aliongoza kikao hicho ikiwa na mada kuu ya ulinzi wa taifa, na maendeleo katika ujenzi wa chama na taifa.

Shirika la habari la Korea Kaskazini (KCNA) limesema katika taarifa. Uongozi wa Korea Kaskazini umeweka wazi kuwa haina nia ya kuingia katika mazungumzo mapya na Marekani kama nchi hiyo inakataa kuondoa vikwazo.

**DW**

### Uturuki yaonya wimbi wakimbizi kutoka Syria

**ANKARA, Uturuki**

RAIS wa Uturuki, Tayyip Erdogan, ameonya kuwa makubaliano na Umoja wa Ulaya (EU) kuhusu wakimbizi yamo hatarini.

Kwa wiki kadhaa Jimbo la Idlib nchini Syria , ngome ya mwisho iliyobaki ya waasi wa jihadi, limekuwa likishambuliwa kutoka majeshi ya serikali ya Syria na Urusi. Mashambulizi ya makombora , maroketi na mashambulizi ya angani yamesababisha miji mingi kuharibika.

Kutokana na mashambulizi yanayoendelea, chama cha madaktari wa Marekani (SAMS), shirika linalotoa msaada wa matibabu, limefunga operesheni zake katika hospitali mbili za jimbo hilo.

Shirika la Medico International, la kutoa misaada ya kiutu pamoja na haki za binadamu, limeripoti kuwa katika muda wa wiki kadhaa zilizopita, kiasi cha hospitali 100 zimeshambuliwa kwa makusudi kwa mabomu.

Rais Erdogan ameonya mapigano hayo yameleta wimbi jipya la watu kukimbilia nchini humo kwa wingi, kama ilivyokuwa mwaka 2015.

**DW**

# Mlipuko wa bomu waua 76 Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

WATU 73 wamedaiwa kufariki kufuatia mlipuko wa bomu lililokuwa limetegwa ndani ya gari katika eneo lenye shughuli nyingi jijini Mogadishu.

Mlipuko huo, ulitokea katika kituo kimoja cha kukagua magari katika eneo la makutano ya barabara kuu mjini humo.

''Mlipuko huo ulikuwa mbaya mno, naweza kuthibitisha kwamba zaidi ya raia 20 waliuawa, huku wengine wengi wakijeruhiwa," ofisa wa polisi Ibrahim Mohamed alinukuliwa na kituo cha habari cha AFP.

Dk. Mohamed Yusuf, Mkurugenzi wa Hospitali ya Madina, alisema wamepokea miili 73 ya watu waliofariki inatarajiwa idadi ikaongezeka.

Hakuna kundi ambalo limekiri kutekeleza kitendo hicho, lakini wapiganaji wa kundi la Al-Shabab wamekuwa wakitekeleza mashambulizi ya mara kwa mara katika taifa hilo.

Mashuhuda watatu waliiambia Reuters, kwamba mlipuko huo ulitokea karibu na kundi moja la wahandisi wa Uturuki ambao walikuwa wakijenga barabara.

Waziri wa Masuala ya Kigeni Somalia, Ahmed Awad, alituma ujumbe wa twitter kwamba wahandisi hao wa Uturuki walifariki.

Wengi ya waliofariki ni wanafunzi wa kiume kwa wakike aliandika.

Uturuki imekuwa mfadhili mkuu wa Somali tangu kiangazi kilichokumba taifa hilo.

Al-Shabab linaloshirikiana na kundi la kigaidi la Al-Qaeda, limekuwa likitekeleza mashambulizi kwa zaidi ya miaka 10. Licha ya kufurushwa kutoka mji mkuu wa Mogadishu mwaka 2011, lakini linadhibiti maeneo ya taifa hilo.

''Kile ambacho niliweza kuona ni watu waliofariki... wakati wa mlipuko huo huku baadhi yao wakichomeka hali ya kutoweza kutambulika," alisema Sakariye Abdulkadir, ambaye alikuwa karibu na mlipuko huo.

Mbunge mmoja wa Somalia, Mohamed Abdirizak, alisema kuwa idadi ya watu waliofariki ni zaidi ya 90, ijapokuwa habari hiyo aliyopata anasema kwamba haijathibitishwa.

Wengi ya waliouawa wanadaiwa kuwa wanafunzi wa chuo kikuu waliokuwa wakipita katika eneo hilo wakisubiri basi lao.

''Mungu awarehemu waathiriwa wa shambulio hili la kikatili," aliongezea waziri huyo wa zamani.


Rais wa Somalia, Mohamed Abdullahi Farmaajo, alishutumu shambulio hilo.

''Adui huyu anafanyakazi ili kutimiza uharibifu wa ugaidi wa kimataifa, hawajafanyia lolote zuri taifa hili, hawajajenga hata barabara moja, hospitali na vituo vyovyote vya elimu," alinukuliwa akisema na kitengo cha habari cha Somalia (SONNA).

''Kile wanachofanya ni uharibifu na mauaji, raia wa Somalia wana habari zote kuhusu vitendo vyao."

Watu watano waliuawa mwezi huu wakati wapiganaji wa Al Shabab waliposhambulia hoteli moja ya Mogadishu inayopendwa sana na wanasiasa, wanadiplomasia na wanajeshi.

***BBC***



Picha ya Wizara ya Ulinzi nchini Urusi, ikionyesha kichwa cha kombora la Avangard. **PICHA: BBC**

# Urusi yazindua kombora kasi mara 12 zaidi ya sauti

**MOSCOW, Urusi**

HATIMAYE Urusi imetangaza kuunda kombora la kwanza lenye teknolojia ya kisasa la 'Avangard Hypersonic' ambalo limeanza kufanya kazi.

Wizara ya Ulinzi ya Taifa hilo ilitoa tangazi hilo jana, lakini haikusema ni wapi kombora hilo lilifanyiwa majaribio, lakini maofisa walisema kwamba litarushwa katika milima ya Urals.

Rais Vladimir Putin, amesema kuwa kombora hilo lenye uwezo wa kinyuklia lina kasi ya mara 20 ya sauti na linaiweka nchi hiyo mbele ya mataifa mengine hasa Marekani.

Kombora hilo lina mfumo maalum wa 'glide' ambao unarahisisha usafiri wake na linaweza kuwa vigumu kutunguliwa.

Waziri wa Ulinzi, Sergei Shoigu, alithibitisha kuundwa kwa kombora la 'avangard hypersonic glide' na lilianza kufanyakazi saa 10:00 za Moscow Desemba 27 na kuliita kama tukio muhimu.

Rais Putin, Jumanne iliyopita alisema mfumo wa Avangard unaweza kupenya mifumo ya ulinzi ya makombora ya kisasa na ile ya baadaye.

"Hakuna hata nchi moja inayomiliki silaha kama hiyo mbali na ile ya masafa marefu inayoweza kurushwa kutoka bara moja hadi jingine," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kwamba mataifa ya magharibi na mataifa mengine yalikuwa yakicheza nao.

Putin alizindua silaha hiyo ya Avangard na mifumo mingine ya silaha katika hotuba yake ya kitaifa mnamo mwezi Machi mwaka 2018.

Desemba 2018, silaha hiyo iligonga lengo la mazoezi ya umbali wa kilomita 6,000 (maili 3,700) katika uzinduzi wa jaribio lililofanyika katika kambi ya makombora kusini mwa milima ya Urals.

Silaha hiyo haiwezi kutunguliwa na mfumo wowote wa ulinzi wa adui, alisema Putin baada ya jaribio hilo.

Likiwa juu ya kombora la masafa marefu linaloweza kurushwa kutoka bara moja hadi jingine, silaha ya Avangard inaweza kubeba silaha ya kinyuklia ilio na uzani wa hadi megatani mbili.

Wizara ya Ulinzi ya Urusi imetoa video ya mfumo wa Avangard, lakini wataalamu wa silaha wameelezea kutilia shaka ufanisi wake.

Marekani ilisema haitapinga madai ya Urusi juu ya uwezo wa Avangard, bali na wao wana mpango wake wa kombora la mfumo wa Hypersonic, kama ilivyo China, ambayo mnamo 2014 ilisema ilifanya majaribio ya silaha kama hiyo.

Novemba 26, mwaka huu, Urusi iliruhusu wataalamu wa Marekani kukagua kombora hilo la Avangard chini ya sheria za makubaliano mapya ya 2010, azimio linalolenga kupunguza idadi ya silaha za kimkakati za kinyuklia.

Makubaliano hayo ambayo yataisha mnamo Februari 2021, ni makubaliano makubwa ya mwisho ya kudhibiti silaha za nyuklia kati ya Urusi na Marekani.

Agosti mwaka huu, Marekani ilijitoa katika Mkataba wa Vikosi vya Nyuklia (INF), ambao ulitiwa saini na Rais wa Marekani, Ronald Reagan na aliyekuwa kiongozi wa Soviet, Mikhail Gorbachev mnamo 1987.

***BBC***

# Udhibiti ugonjwa miguu, midomo ng'ombe waanza

**Na Beatrice Philemon**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi inakusanya sampuli kutoka kwa ng'ombe na wanyamapori wanaoumwa ugonjwa wa midomo na miguu (FMD) ili kupata vyanzo za virusi vinavyosababisha ugonjwa huo.

Lengo ni kuiweze kupata chanjo maalum kwa ajili ya matumizi ya mifugo ya Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania kutoka Wizara hiyo, Prof. Hezron Nonga, alisema kuwa sampuli zote zitakazokusanywa kutoka kwa ng'ombe na wanyamapori wanaoumwa ugonjwa huo, zitapelekwa kwenye viwanda vinavyozalisha chanjo katika nchi ya Botswana, Kenya na Afrika Kusini ili watengeneze chanjo maalumu yenye kabila tano za virusi vinavyosababisha ugonjwa wa miguu na midomo kwa ng'ombe.

"Chanjo itakayozalishwa itakuwa maalumu kwa matumizi ya mifugo ya Tanzania na tunategemea kupeleka sampuli hizo mwaka kesho 2020 na hapo ndiyo tutakapokuwa na uhakika wa chanjo na ulinzi wa mifugo yetu dhidi ya ugonjwa wa midomo na miguu," alisema.

Alisema wizara imeamua kutafuta chanjo maalum kwa ajili ya matumizi ya mifugo ya Tanzania kwa sababu chanjo zilizopo ni zile zinazokinga ng'ombe dhidi ya virusi aina moja, mbili au tatu na hakuna chanjo zinazokinga dhidi ya virusi vyote vitano.

Alisema mpaka sasa Tanzania hakuna kiwanda cha kuzalisha chanjo za ugonjwa wa FMD, chanjo zote zinaagizwa kutoka Kenya, Botswana, Ubelgiji na Afrika Kusini ili kudhibiti ugonjwa huo.

Mpaka sasa Tanzania kuna aina (kabila) tano ya virusi vya ugonjwa wa FMD ambavyo ni SAT1, SAT2, SAT3, O na A na virusi hawa wamesambaa nchi nzima.

Kwa mujibu wa Prof. Nonga, chanjo zilizopo nchini siyo feki kwa sababu zote zikiingia nchini lazima zithibitishwe ubora wake na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania kabla ya kuingia sokoni kwa ajili ya matumizi ya mifugo.

Pia mamlaka hizi hufuatilia chanjo hizo kila zinapokuwa kwenye maduka ya wauzaji ili kujiridhisha na ubora wake.

Alifafanua kuwa wizara imeamua kutafuta suluhisho la ugonjwa huu baada ya kuona wafugaji wengi wanapata changamoto katika shughuli zao za ufugaji ikiwamo vifo vya wanyama, upungufu wa uzalishaji wa mazao ya mifugo, gharama kubwa ya matibabu na Tanzania kushindwa kuuza nyama katika masoko ya nje.

Alisema ugonjwa wa midomo na miguu huathiri mifugo na wanyamapori wenye kwato na husababishwa na virusi aina ya "FMD virus".

"Kwa upande wa wanyama wa kufugwa virusi vya FMD huathiri zaidi ng'ombe na kidogo mbuzi, kondoo na nguruwe, na kwa wanyamapori huathiri zaidi nyati, nyumbu na nguruwe pori," anasema.

Anaainisha zaidi kuwa ugonjwa wa FMD ndiyo ugonjwa pekee ambao umeifanya Tanzania isiweze kuuza nyama ya ng'ombe nje ya nchi licha ya kuwa na ng'ombe takribani milioni 32.5 na juhudi hizi za kuutokomeza zitakuwa ni mkombozi mkubwa wa biashara ya nyama Tanzania.

Akizungumzia jinsi ugonjwa huu unavyoenea, Prof. Nonga alisema ng'ombe hupata maambukizi kwa njia ya kugusana na wanyama wenye maambukizi, na wakati mwingine kula majani, kunywa maji, kuvuta hewa yenye vimelea wa FMD au kuguswa na wadudu kama inzi waliotoka kwa mnyama mwenye maambukizi.

"Ng'ombe akishaambukizwa ugonjwa huu hupata vidonda kwenye miguu, midomo, ulimi na kinywa na pia hupata homa kali na wakati mwingine kushindwa kutembea na kula," alieleza.

Pia hutokwa mate mengi na huwa anatafuna na kusaga meno saa zote na ugonjwa huu ukiingia shambani, asilimia 90 ya ng'ombe huugua.

Vifo mara nyingi hutokea kwa ndama na ng'ombe wazee au wenye matatizo mengine na hakuna tiba bali kuna kinga tu. Kinga ya ugonjwa wa FMD ni chanjo.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA) na mlezi wa Kinondoni Women Development Association (KIWODEA), akisalimiana na viongozi na wanachama wa taasisi hiyo, juzi katika hafla ya kuuga na kuukaribisha mwaka mpya wa 2020, ambapo alikuwa mgeni rasmi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Uchunguzi kubaini ukweli pamba kuzalishwa Lindi

**Na Said Hamdani, LINDI**

SERIKALI imesema itawatuma wataalamu mkoani Lindi kubaini kama ilikuwa inazalisha pamba.

Lengo ni kubaini kama inaweza kuzalisha zao hilo, baada ya kuwekewa zuio kwa madai ya uwapo wa mdudu mharibifu wa zao hilo miaka iliyopita.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipokuwa anajibu baadhi ya maswali aliyoulizwa na wanahabari wakati wa ziara yake mkoani Lindi.

Wanahabari hao walitaka kufahamu iwapo serikali ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kwa kuruhusu kulimwa Lindi ambalo miaka ya nyuma serikali ilizuia kwa madai ya uwapo kwa wadudu hao kutokea Msumbiji.

Akijibu swali hilo mbele ya viongozi wa serikali Mkoa wa Lindi, Hasunga alisema kimsingi hakuwa na taarifa ya aina hiyo, kama mkoa huo wananchi wake walikuwa wakijihusisha na kilimo cha pamba.

Hata hivyo, aliisema kwa vile hakuwa anatambua Lindi na Mtwara wananchi wake walikuwa walimaji pamba, atawatuma wataalamu kwenda kufanya uchunguzi, na ukweli utakapobainika serikali haitasita kuwaruhusu wananchi wa mikoa hiyo kuendelea kulima zao hilo.

"Sifahamu kama Lindi pamba ilikuwa inalimwa, lakini kwa vile umeniambia, nitatuma wataalamu waje kuchunguza kwanza," alisema Hasunga.

Alisema baada ya wataalamu kumaliza kazi ya uchunguzi, na kumwasilishia taarifa iliyo sahihi, serikali haitasita kuondoa zuio hilo, ili kuwapa nafasi wananchi kuendeleza kilimo hicho, kwa ajili ya kuongeza bidhaa kulisha viwanda vinavyohusika na utengenezaji wa nguo nchini.

Waziri huyo alisema kwa kutambua Taifa linaelekea kwenye uchumi wa viwanda, hakutakuwa na sababu kwa serikali kuendelea kuweka zuio hilo, badala yake italiondoa ili kuruhusu wananchi kuongeza uzalishaji.

"Baada ya wiki tatu nipigie nitakupa majibu ya kuwaruhusu wataalamu kuja kufanya uchunguzi katika Mkoa wa Lindi," alisema Waziri Hasunga.

## Kichanga chakutwa kimekufa ndani ya shimo

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MWANAMKE ambaye hajafahamika wilayani hapa, amejifungua mtoto na kumtupa kwa kuchimba shimo na kumfukia huku akiwa amemvilingisha kwenye mfuko wa plastiki.

Akizungumza na gazeti hili jana eneo la tukio hilo, Mtendaji wa Mtaa huo, Bashiri Kitambi, alisema tukio hilo limetokea jana majira saa 1:45 asubuhi katika mtaa wa Sababa, wilayani hapo.

Alisema kichanga hicho kilikutwa kimefukiwa ndani ya shimo na kuvilingishwa kwenye mfuko wa plastiki na kusababisha kichanga hicho kupoteza maisha.

Kadhalika alisema mtu aliyejifungua kichanga hiko na kukitupa kwenye shimo alilolichimba na kukifukia.

Mtendaji huyo alisema walipata taarifa za kuwapo kwa tukio hilo kutoka kwa wananchi wasamaria wema.

Hata hivyo, alisema aliyefanya tukio hilo hajafahamika na huenda aliyefanya kitendo hicho anatoka mbali na mtaa huo.

Kitambi alisema uongozi wa serikali ya mtaa na kata ulifika katika eneo hilo na kuamuru wananchi kufukua shimo hilo kukutana na kichanga hicho kikiwa kimeviligwa kwenye mfuko wa plastiki kikiwa tayari kimekufa.

Alisema uongozi wa serikali ya mtaa huo kwa kushirikiana na mtendaji kata, Jamadi Kasimba, waliamuru wananchi wafukue shimo hilo na kutoa taarifa polisi.

Alisema Jeshi la Polisi walipofika kwenye eneo hilo na kuthibitisha walieleza kuwa watafuatilia ili kujua aliyefanya tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, alipopigiwa simu kupata ufafanuzi wa suala hilo, alisema yupo katika kikao. Mmoja wa ofisa wa Jeshi la Polisi mkoani humo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini alithibitisha tukio hilo na kueleza kuwa uchunguzi unaendelea.

## DC awatwishwa madiwani kazi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, amewaagiza madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza wanaanza masomo yao katika shule walizopangiwa katika kata zote za manispaa hiyo.

Alitahadharisha kuwa mwanafunzi yeyote atakayekosa kuingia kidato cha kwanza, diwani wa kata husika bila kujali ni wa chama gani atachukuliwa hatua kwa kuzembea agizo hilo la serikali.

Chonjo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, ambacho kilikuwa pia kikijadili taarifa ya elimu kwa manispaa hiyo.

"Kila diwani wa kata ya manispaa ya Morogoro ahakikishe wanafunzi hao wanaingia kidato cha kwanza bila kukosa, vinginevyo mtawajibishwa," alisema.

Mbunge wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, aliitaka Manispaa ya Morogoro kuhakikisha inasimamia walimu na kuwafuatilia kwa karibu ili waweze kufundisha wanafunzi kwa madai baadhi ya shule za msingi katika manispaa hiyo, amesaidia kuzimaliza changamoto zilizokuwa zikiwakabili ikiwamo madarasa na madawati.

Kwa upende wake Diwani wa Kata ya Sultani, Peter Dhahabu, alisema ipo haja kwa halmashauri hiyo kutenga fedha kwa ajili ya mitihani ya majaribio ya kuwapima watoto hao kabla ya kufanya mitihani ya kitaifa.

"Shule yangu ya Kikundi iliyopo kata ya Sultani ilikuwa ya mwisho katika matokeo ya mitihani iliyopita, lakini baada ya kukaa na walimu na kuona umuhimu wa mitihani hiyo na nikachangia sasa imefanya vizuri," alisema Diwani Dhahabu.

Naye Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Morogoro, Christine Ishengoma (CCM), alisema ipo haja kuongeza nguvu pamoja na kuwapa vivutio walimu wanaofundisha shule za pembezoni ili kusaidia kuongeza ufaulu.

"Walimu wa shule ya Luhungo manispaa hii wanapita nyumbani kwangu saa nne asubuhi wakitokea shuleni, ina maana hawafundishi ipasavyo," alidai mbunge huyo.

# Mfanyabiashara alalamika mali zake kuhujumiwa

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

MFANYABIASHARA maarufu wa Jiji la Arusha, Philemon Mollel (Monaban), amelalamikia hatua ya baadhi ya mali zake zilizopo katika kiwanda cha kusaga nafaka cha NMC, kuhujumiwa na kuuzwa mitaani kinyume na utaratibu.

Mollel alitoa kilio hicho wakati akizungumza na Nipashe, baada ya kufanikiwa kukamata mifuko zaidi ya 1,000 ikiwa inauzwa mitaani na wamachinga, aliyokuwa amezalisha katika kiwanda hicho kabla ya serikali kumpokonya.

"Nimesikitishwa kuona mali zangu zikihujumiwa na sielewi nani anahusika kuzitoa kiwandani hapo, huu ni uonevu mkubwa na unania mbaya ya kunidhoofisha kibiashara," alisema Mollel.

Alidai hatua hiyo ilimlazimu kuingia mtaani na kwenye masoko akiwa na askari polisi na kufanikiwa kuwakamata vijana wapatao 13 wanaoisambaza mtaani wakiwamo wauza chipsi wanaoitumia kufungashia chips wateja wao.

Mfanyabiashara huyo alidai baada ya serikali kumpokonya kiwanda hicho na kuikabidhi Bodi ya Nafaka na mazao mchanganyiko, aliacha mali nyingi alizokuwa amezalisha ambazo kimsingi hazihusiani na mgogoro

wake na bodi hiyo, lakini ameshangaa kuona mali hizo zikizagaa mtaani.

Alidai shauri la mgogoro huo bado lipo mahakamani na wanasubiri uamuzi wa mahakama kuhusu mkataba wake wa upangaji katika kiwanda hicho pamoja na mali zake, lakini ameshangazwa kuona mali hizo zikiuzwa na wamachinga mtaani.

"Nasikitika kuona mali zangu zikihujumiwa wakati jambo hili bado lipo mahakamani, naiomba serikali isaidie mali zangu zisije zikapotea," alidai Mollel.

Aliiomba serikali kupitia vyombo vya dola kuchunguza kwa makini jambo hilo na kuwachukulia hatua waliohusika kutoa mali hizo kiwandani na kuziuza nje kinyume na utaratibu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akizungumzia madai hayo, alisema jambo hilo lipo katika hatua za uchunguzi ili kubaini wahusika halisi wa tukio hilo na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akionyesha mfano kwa vitendo kwa wanakijiji wa Ibambo wilayani Kaliua, juu ya palizi bora ya mimea wakati wa ziara yake ya kuhamasisha kilimo bora hivi karibuni. **PICHA: VINCENT TIGANYA**

# Maajabu vivutio Msitu Taware majoka yabadili hali ya hewa

**Na Dege Masoli, HANDENI**

MSITU wa Taware uliopo wilayani Handeni mkoani Tanga, una maajabu ya vivutio vya utalii yakiwamo mapango yenye vichwa vinavyofanana na binadamu na majoka makubwa yasiyokuwa na madhara kwa binadamu.

Msitu huo wenye miti mikubwa na uoto wa asili, unawezesha chemchemu za maji kufanyakazi misimu yote ya mwaka.

Wakizungumza na waandishi wa habari waliotembelea Msitu wa Taware, Tarafa ya Mazingara unaosimamiwa na Mradi wa Mpango wa Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu nchini (Forvac), kwa kushirikiana na Serikali ya Finland, wananchi wanaoishi tarafa hiyo walisema, wamekuwa na changamoto kubwa ya kutunza mazingira katika msitu huo kutokana na baadhi yao kutokuwa na elimu.

Wananchi hao walisema mpango wa elimu unaotolewa na mradi huo ni ukombozi kwao na misitu kwa ujumla kwa kuwa vitendo vya uharibifu huo vinachangiwa na wakazi wa maeneo husika kutokuwa na ufahamu wa namna ya kutunza mazingira yao.

Juma Mohammed, mkazi wa Mazingara alisema, msitu huo una vivutio vingi vya utalii ikiwamo jiwe kubwa lenye pua mbili mfano wa binadamu, lakini katika miamba hiyo kuna majoka makubwa ambayo hayana madhara kwa binadamu na hata yanapopita njiani hali ya hewa hubadilika na kuwa mawingu na ubaridi mkali unaovuma eneo husika.

Juma alisema msitu huo wenye miti mikubwa, uoto wa asili, unawezesha chemchemu za maji kufanyakazi misimu yote ya mwaka. "Ndugu waandishi tunawashukuru sana kwa kutembelea leo huenda ukawa mwanzo wa kuja kwa watalii wa ndani na nje katika eneo letu ambalo lina vivutio vingi vya utalii, lakini halitangazwi," alisema Juma.

Naye Shabani Mlanguzi, alisema Kamati ya Mazingara ilianzishwa mwaka 2011 ikiwa na lengo la kusimamia utunzaji wa mazingira yanayouzunguka Msitu wa Tarawe ambao una vivutio vingi yakiwamo mapango yanayoitwa 'kungwi' na 'mwari' ambayo yana vichwa vinavyofanana na kichwa cha binadamu.

"Zamani kwenye mapango haya kuliletwa mwari na kungwi wake wakakosea masharti wakapotea moja kwa moja... Nawaomba sana Watanzania waje kutembelea maajabu haya, miundombinu ni mizuri barabara ipo safi ya lami," alisisitiza Mwanahawa Ramadhan. Kwa upande wake Katibu Tawala, Tarafa ya Mazingara, Hashimu Msagati, alisema Msitu wa Tarawe una maajabu mengi ambayo yakitangazwa kupitia vyombo vya habari watalii wengi wataenda kutembelea na kusaidia kuongeza mapato.

Msagati aeleza kuwa baada ya kuona msitu huo una vivutio vingi vya utalii, wananchi waliamua kuunda kamati maalumu inayosimamia ulinzi na utunzaji wa mazingara ili msitu huo mkubwa usiharibiwe, na tangu Forvac ishirikiane na wakazi hao imesaidia kwenye utoaji wa elimu kwa watu wanaozunguka msitu huo.

Mratibu wa kitaifa wa mpango wa mnyororo wa thamani ya mazao ya msitu nchini, Emmanuel Msofe, alisema Wilaya ya Handeni ni miongoni mwa halmashauri 10 nchini zinazonufaika na mradi wa Forvac.

Alieleza kuwa wilaya hiyo imenufaika na mradi huo ambao unatoa elimu kwa wananchi wanaozunguka msitu huo na misitu mingine namna ya kuitunza ili isipoteze uoto wake na kwamba elimu hiyo itaendelea kutolewa iliwamo kutangaza utalii wilayani Handeni.



# PELLEGRINI AFUKUZWA WEST HAM

**LONDON, Englad**

KOCHA Manuel Pellegrini amefukuzwa na West Ham baada ya matokeo mabaya ya timu hiyo msimu huu.

Kichapo cha mabao 2-1 nyumbani kutoka kwa Leicester City juzi Jumamosi kilihitimisha ajira ya Pellegrini.

West Ham wapo pointi moja tu juu ya mstari wa kushuka daraja na Mwenyekiti mwenza wa klabu hiyo, David Sullivan, alisema wamelazimika kufanya uamuzi huo.

"Tulikuwa na wakati mgumu kufanya uamuzi huu. Manuel ni mtu mzuri na tulikuwa na nafasi nzuri kufanya kazi na mtu mwenye hadhi kama yeye," alisema Sullivan.

"Hata hivyo, ni wazi kwamba ilitulazimu kufanya uamuzi huu na mabadiliko yalihitajika haraka inavyowezekana, hasa kutokana na kiwango cha timu yetu msimu huu.

"Tulihisi ilikuwa ni muhimu kufanya maamuzi sasa kwa ajili ya kumpa nafasi kocha mpya kujaribu inavyowezekana kufanikisha malengo ya klabu yetu."

Pellegrini aliwasili hapo kwenye dimba la London, Mei mwaka 2018 kwa mkataba wa miaka mitatu na aliiongoza timu hiyo kumaliza kwenye nafasi 10 bora msimu uliopita.

Hata hivyo, raia huyo wa Chile ambaye aliiongoza Manchester City kutwaa taji la Ligi Kuu msimu wa 2013-14 - ameshuhudia West Ham ikipoteza mechi 10 kati ya 19 msimu huu, licha ya kusajili wachezaji wenye majina makubwa kama Sebastien Haller na Pablo Fornals msimu huu.

## ALEXANDER-ARNOLD: NATAKA KUWA GWIJI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

TRENT Alexander-Arnold anataka kubakia Liverpool kwa kipindi chote cha maisha yake ya uchezaji akiwa na matumaini ya kuwa gwiji wa klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha kwanza cha Liverpool kwa misimu miwili iliyopita na alishika nafasi ya 19 kwenye kura za tuzo ya Ballon d'Or.

Zaidi alionyesha kufurahishwa na bao lake na 'asisti' zake mbili alizozitoa wakati wekundu hao wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Leicester City, matokeo ambayo yaliiacha Liverpool kuendelea kuukaribia ubingwa wa ligi hiyo.

Na mzaliwa huyo wa jijini Liverpool akiwa ametokea kwenye akademi ya klabu hiyo sasa anataka kubakia hapo kwenye dimba la Anfield kwa maisha yake yote ya soka.

"Mara zote nimekata kuwa gwiji wa klabu hii," alisema akiliambia gazeti la Sportbladet la nchini Sweden.

"Kushinda mataji, na kucheza mechi nyingi kadili inavyowezekana na siku moja kuwa nahodha wa klabu hii.

"Bila shaka, naweza kama nikiondoka hapa sitaweza kuwa gwiji wa klabu hii. Mimi nataka kuwa na mafanikio na klabu hii."




## VIDAL: AISHUTUMU BARCELONA KUTOMLIPA BONASI YAKE


**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO Arturo Vidal ameishutumu Barcelona kwa kutofanya "haki" akidai kwamba hajalipwa bonasi yake ya euro milioni 2.4.

Kwa mujibu wa gazeti la nchini Hispania la ABC, Vidal amefungua malalamiko kwa klabu yake hiyo ya Ligi Kuu Hispania, La Liga na chama na wachezaji wakulipwa wa Hispania.

Inadaiwa kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile amelipwa euro milioni 1.7 tu kati ya euro milioni 4.1 ambazo anatakiwa kulipwa.

Vidal, amekuwa akihusishwa na uhamisho kipindi cha Januari kwenda kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kutokana na kutolipwa madai yake hayo, lakini sasa suala hilo ameliacha kwa wawakilishi wake.



"Sio jukumu langu kufuatilia hilo, ndio maana nina wakala na mwanasheria ambao ndio wanafuatilia mambo yangu," alisema Vidal akiiambia redio ya nchini Chile ya ADN.

"Inaonekana sio haki kwangu mimi kama fedha zinakosekana, lakini ni jambo la wawakilishi wangu."

Vidal ameanza katika mechi nne tu za LaLiga kwa Barcelona msimu huu na mapema wiki hii alikanusha uwezekano wa kuhamia Inter Milan wakati wa dirisha lijalo la Januari.

HABARI MICHEZO



# MOURINHO

## ASIFIA KIWANGO CHA NDOMBELE SPURS IKIBANWA

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, amemsifia kiungo, Tanguy Ndombele kwa kiwango kizuri alichokionesha dhidi ya Norwich City kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Ndombele alikuwa nyota wakati akiwa amerudi kwenye kikosi hicho cha Mourinho, wakati Tottenham ikitoka sare ya 2-2 na Norwich Jumamosi.

Ndombele, ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo, Lyon aliachwa kwenye kikosi cha Tottenham kilichocheza dhidi ya Brighton and Hove Albion siku ya Alhamisi.

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 23, alirudi kikosini humo huku Harry Winks na Moussa Sissoko wakiwa nje, na Mourinho alisifia kiwango chake.

"Alicheza vizuri," Mourinho aliwaambia waandishi wa habari. "Tulicheza bila ya wachezaji wengi wa kati, hakuwapo Winks, wala (Eric) Dier na (Christian) Eriksen na Ndombele alicheza vizuri sana.

"Aliweza kutawala mpira kwa kupiga pasi nzuri na alikuwa na haraka kuuwahi mpira na kwa hakika alicheza vizuri mno.

Tottenham ililazimika kutoka nyuma kwa bao moja na kuweza kupata pointi moja kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Carrow Road.

Mario Vrancic alifunga la kwanza dakika ya 18 kabla ya Tottenham kusawazisha kupitia Christian Eriksen dakika 10 kabla ya mapumziko.

Bao la kujifunga la Serge Aurier likawafanya Norwich wawe mbele kabla ya Harry Kane kusawazisha dakika ya 83.

# Guardiola ataendelea kubakia City

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola atabakia Manchester City na wataangalia mkataba wake utakapomalizika, kwa mujibu wa ofisa mtendaji, Ferran Soriano.

Mkataba wa sasa wa Guardiola na City unamalizika mwaka 2021, hata hivyo, kumekuwa na mashaka juu ya majaliwa ya Mhispania huyo, baada ya kushinda mfululizo taji la Ligi Kuu England.

Ripoti ambazo Guardiola mwenyewe alikanusha zilidai kwamba, kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Hata hivyo, Soriano ana imani kwamba Guardiola atabakia na kuheshimu mkataba wake licha ya kwamba uvumi kuzagaa kwamba anarudi Barcelona.

"Pep hajasema mara nyingi kuhusu mkataba wake," alisema Soriano wakati akiwa Dubai kwenye mkutano wa michezo wa kimataifa.

"Hakuna majadiliano kuhusu hilo.

"Pep atabakia na ataondoka muda muafaka utakapofika siku moja na klabu ina nguvu ya kutosha kuweza kushawishi mabadiliko yoyote. Lakini Pep ameshasema mara nyingi, haondoki."

Guardiola alihamia City mwaka 2016 na kikosi chake kilitawala soka la Uingereza hadi msimu huu.

City imeshinda mataji saba tangu msimu wa 2017-18, lakini sasa kikosi hicho cha Guardiola kipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi kikipitwa pointi 14 na vinara Liverpool kabla ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Sheffield United kwenye dimba la Etihad.

# Ajax yahitaji huduma ya Hag

**AMSTERDAM, Uholanzi**



KOCHA Erik ten Hag hataruhusiwa kuondoka Ajax mwakani kwa namna yoyote, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo, Marc Overmars.

Hag mwenye umri wa miaka 49 amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa kubwa, tangu alipoiongoza Ajax kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na kutwaa taji la Ligi Kuu ya nchi hiyo.

Miongoni mwa klabu zinazotajwa kumuwania Hag ni mabingwa wa Ujerumani, Bayern Munich, ambao wanaongozwa na Hansi Flick kwa muda hadi mwishoni mwa msimu.

Bayern imetajwa kwamba inamwania Mholanzi huyo msimu ujao, lakini Overmars ana imani kwamba haendi kokote.

"Ten Hag kwa urahisi tu anaweza kuendelea na msimu mwingine wa kipindi kijacho cha majira ya joto," amesema Overmars akiliambia gazeti la De Telegraaf.

"Kwa uhakika sitamwachia aondoke, ingawa najua kwamba yupo kwenye orodha ya kutakiwa na klabu kubwa Ulaya. Mlango utakuwa umeendelea kufungwa.

"Bado tuna mkataba nae, hivyo kwa sasa sio jambo jema kuzungumzia kuhusu yeye kuondoka, maana yupo na sisi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AFURAHIA UNITED KUZINDUKA

●●●Awataka wachezaji wake kuendelea na kasi hiyo watakapoikabili Arsenal...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesifia uwezo wa kikosi chake "kulazimisha matokeo" baada ya Mashetani Wekundu hao kuifumua Burnley mabao 2-0 katika mchezo wa Ligi Kuu England, uliochezwa juzi Jumamosi usiku.

Anthony Martial alifunga bao lake la tatu katika mechi mbili zilizopita dakika moja kabla ya mapumziko kuwaweka mbele United kwenye mchezo ambao walitawala kwa kipindi kirefu, lakini wenyeji Burnley walipeleka presha nyingi kwa golikipa, David De Gea, dakika 15 za mwisho kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Turf Moor.

Dakika za majeruhi United walicheza kwa nguvu na kupatikana kwa bao la pili wakati Daniel James alipomchezesha vizuri Marcus Rashford aliyefunga bao lake la 12 la Ligi Kuu msimu huu na kuifanya timu hiyo kujivuta hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi, wakiwa wamezidiwa pointi moja tu na Chelsea iliyopo nafasi ya nne.

Solskjaer alikubali kwamba wachezaji wangeweza kupata matokeo hayo mapema, lakini aliwasifia kwa kupata ushindi mfululizo, akijielezea yeye mwenyewe kwamba "ana furaha kubwa".

"Kipindi cha kwanza nilifikiri tulikuwa vizuri zaidi," alisema Solskjaer. "Tulitawala mchezo, tukafunga bao, na tulifunga bao zuri zaidi.

"Kipindi cha pili bila shaka kulikuwa na ugumu kwa lango letu kushambuliwa mara kwa mara, lakini tuliweza kusukuma mashambulizi mbele na kufanikiwa kupata bao la pili.

"Tungeweza kumaliza mchezo kwa ushindi wa mapema, tulikuwa na nafasi nyingi za kufanya mashambulizi ya kushtukiza.

"Tulitakiwa kupata bao la pili mapema, lakini waliweza kulinda vizuri lango lao na kutupa wakati mgumu.

"Ni muhimu kwa upande wetu kujua kwamba tunaweza kuchimba na kulazimisha matokeo kama ilivyotokea, ingawa wakati ukifunga moja mara zote huwezi kushinda.

"Kama hatujafungwa bao lolote, tumepata nafasi ya kujivuta kwenye msimamo wa ligi."

Sasa United itasafiri kwenda uwanja wa Emirates kucheza na Arsenal siku ya mwaka mpya na Solskjaer amewataka wachezaji wake kuendelea na kasi hiyo hiyo iliyowafanya wacheze mechi tisa na kupoteza moja tu kwenye mashindano yote, baada ya kufungwa mabao 2-0 na Watford Desemba 22, mwaka huu.

Huku Martial na Rashford wakiendelea kuwa kwenye kiwango kizuri, United itakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kupata matokeo dhidi ya Arsenal ambayo kwa sasa inajaribu kuzoea maisha mapya chini ya kocha mpya, Mikel Arteta.

Kuelekea mchezo huo, Solskjaer alisema washambuliaji wake watatakiwa kutopoteza muda zaidi kama ilivyokuwa kwa Burnley.

"Unajiweka kwenye nafasi mbaya kama hutumia nafasi unazopata vizuri. Tulifanya mashambulizi mengi ya kushtukiza na tulikuwa na nafasi ya kufunga kwa urahisi, lakini tulifanya maamuzi mabaya au tulikuwa taratibu mno kwenye kumalizia, lakini tulikuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

"Ngoja tuangalie nini tutafanya dhidi ya Arsenal. Tunataka kuendelea na kasi hii hii. Ushindi mara mbili baada ya kufungwa na Watford. Nina furaha na hilo. Vijana wamejibu vizuri na wamejifunza."

## KWA UFUPI

**UNITED YAMSUBIRI ERIKSEN**

MANCHESTER United inajiandaa hadi msimu utakapomalizika ndiyo ianze tena mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), akiwa mchezaji huru. ***(Sunday Telegraph)***

**VALVERDE AMZUIA POGBA**

REAL Madrid wamemweleza Kocha Zinedine Zidane, asahau mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Manchester United, Paul Pogba (26), kwa sababu Mfaransa huyo atazuia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Federico Valverde, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(AS)***

**ANCELOTTI AIBANIA UNITED**

KOCHA mpya wa Everton, Carlo Ancelotti, anatarajia kuweka ngumu ya kukubali ofa yoyote kutoka kwa Manchester United kwa ajili ya kumnasa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Richarlison (22). United imepanga kutoa dau la pauni milioni 70 ili kufanikisha usajili huo. ***(Sun on Sunday)***

**MOYES KUMRITHI PELLEGRINI**

MAKOCHA David Moyes na Tony Pulis wanaongoza katika mchakato wa kurithi mikoba iliyoachwa na Manuel Pellegrini ambaye alitimuliwa mwishoni mwa wiki baada ya West Ham kuwa na matokeo mabaya. ***(Sunday Telegraph)***

**TRENT KUSTAAFIA LIVERPOOL**

BEKI wa kulia wa Timu ya Taifa ya England, Trent Alexander-Arnold (21), amesema kwamba anataka kuendelea kubakia Liverpool katika muda wote wa kucheza soka ili aweze kuja kuwa mmoja wa wachezaji wakongwe wa klabu hiyo. ***(Sportbladet, via Independent)***

**SARRI AMTAKA GIROUD**

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, anajiandaa kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 33 akitokea katika timu yake ya zamani ya Chelsea. ***(La Stampa - in Italian)***

**BAYERN, JUVE, PSG VITANI**

BAYERN Munich, Juventus na Paris St-Germain zimeonyesha nia ya kuwania saini ya golikipa wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Marc-Andre Ter Stegen (27), kutokea Barcelona. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**EZE ANUKIA SHEFFIELD**

MABOSI wa Sheffield United wamejitosa kuwania saini ya mshambuliaji wa QPR, raia wa England, Eberechi Eze, ambaye ana umri wa miaka 21 na thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 12. ***(Sun on Sunday)***

**BARCA YAMSHUSHUA VIDAL**

BARCELONA imesema kuwa mashtaka ya kutolipwa bonasi yanayotolewa na Arturo Vidal (32), ni moja ya sababu anazojaribu kuziweka wazi ili kurahisisha uhamisho wake wa kujiunga na Inter Milan katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(ESPN)***

**ROJO KUTUA FIORENTINA**

FIORENTINA inajiandaa kumsajili beki wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Argentina, Marcos Rojo, ambaye ana umri wa miaka 29 katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(La Nazione, via Football Italia)***

**INIESTA AIKATAA MLS**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona, Andres Iniesta (35), amekataa ofa za kujiunga na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Marekani ambazo ni LA Galaxy, Inter Miami na Montreal Sounders na kuweka wazi kwamba anafurahia kubaki kwenye kikosi cha Vissel Kobe cha Japan. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# GOLIKIPA KMC ABAINISHA UZOEFU UMEIBEBA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA wa KMC FC, Jonathan Nahimana, amesema kuwa kilichowasaidia mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kupata ushindi katika mchezo uliowakutanisha hapo juzi ni uzoefu wa wachezaji wake.

Simba iliendeleza kasi yake ya ushindi baada ya juzi kuwafunga KMC FC mabao 2-0, na kufikisha pointi 31 baada ya kucheza mechi 12.

Nahimana aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wa Simba walitumia vema uzoefu waliokuwa nao, licha ya nyota wa KMC kupambana kuwabana.

Kipa huyo alisema kuwa pia maandalizi waliyofanya kuelekea mchezo huo yalisaidia kuwapa wakati mgumu mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mechi ilikuwa 50-50, wenzetu walipata nafasi wakazitumia vizuri, ila sisi wametuharibia malengo yetu, kupitia uzoefu walionao wametuharibia mipango yetu," alisema Nahimana, kipa huyo raia wa Burundi.

Aliongeza kuwa licha ya kukaa nje kwa muda mrefu kutokana na maumivu ya bega yaliyokuwa yanamsumbua, anaahidi kuendeleza kucheza vema ili arejee katika kiwango chake cha kawaida.

"Nawapongeza sana, wameonyesha uwezo wao, wametuheshimu, hawajatudharau, kulikuwa na tofauti kubwa katika timu hizi mbili, ukiangalia hata walivyokuwa wakishambulia, walionekana ni wachezaji wenye uzoefu zaidi," Nahimana alisema.

Naye nahodha wa Simba katika mchezo wa juzi, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr", amesema siri ya wao kupata ushindi ilitokana na kuwaheshimu wapinzani wao ambao mara zote wamekuwa na kiwango kizuri wanapokutana.

Beki huyo alisema kuwa katika kipindi cha kwanza idara ya kiungo haikucheza vema, jambo ambalo kocha wao alilibaini na walipoingia kwenye dakika 45 za pili waliimarika na hatimaye walipata ushindi.

Vinara na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba watashuka tena uwanjani kesho kuwakaribisha Ndanda FC kutoka mkoani Mtwara huku Januari 4, mwakani watavaana na watani zao, Yanga.




Kiungo wa Newcastle United, Jonjo Shelvey (kushoto), akijaribu kumiliki mpira mbele ya beki wa Everton, Moise Kean, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi. Everton ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Waendesha mitumbwi kuchuana Musoma

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya timu 11 zinatarajia kushiriki katika mashindano ya mitumbwi yatakayofanyika leo katika kijiji cha Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara, maalumu kwa ajili ya kuuaga mwaka huu na kuukaribisha mwaka mpya wa 2020.

Timu hizo ni kutoka katika kata za Bugwema, Bukima, Bukumi, Bwasi, Etaro, Mugango, Murangi, Musanja, Nyakatende, Rusoli na Suguti, ambazo kila moja itakuwa na wapiga kasia watano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa mashindano hayo, Fedison Masawa, alisema kuwa maandalizi ambayo yanasimamiwa na ofisi ya mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, yamekamilika.

"Kwa upande wa zawadi tumejiandaa vizuri pia, mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni moja na kikombe, mshindi wa pili Sh. 700,000 na kikombe na mshindi wa tatu atazawadiwa Sh. 400,00 na kikombe," alisema Masawa.

Aliongeza kuwa zawadi ya kifuta jasho kwa timu nyingine zilizobakia ambazo hazikufanya vema, itakuwa ni Sh. 50,000.

"Timu zitazoshiriki mashindano haya zinatakiwa kuwapo kwenye ufukwe wa Ziwa Victoria eneo la Bukima kuanzia saa 2:30 asubuhi bila kuchelewa na taratibu za usalama majini zitazingatiwa," alisema mratibu huyo.

Aliweka wazi kuwa suala la michezo na utamaduni ni miongoni mwa vipaumbele vya jimbo hilo na wamekuwa wakiandaa pia mashindano ya kwaya, ngoma za asili na mpira wa miguu.

# Shime afurahia mazoezi Algeria

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kufanya vibaya katika mashindano maalumu ya UNAF yanayoendelea nchini Algeria, Kocha Mkuu wa Timu ya Vijana wa umri chini ya miaka 20 ya wanawake, Bakari Shime, amesema kuwa nafasi waliyopata wachezaji wake imewasaidia kujiandaa na mashindano ya Afrika.

Timu hiyo ilitarajiwa kurejea nchini jana, baada ya kucheza mechi mbili, imefungwa mabao 3-0 dhidi ya Algeria na ilianza kwa sare ya goli 1-1 na wenzao wa Misri.

Shime, alisema kuwa wachezaji wake wamepata nafasi nyingine ya kujiimarisha na atatumia makosa yaliyojitokeza kwenda kukinoa zaidi kikosi chake.

Kocha huyo alisema kuwa kupata nafasi ya kucheza mechi za kirafiki huwa ni ngumu, na inapotokea, benchi la ufundi hutumia kukipima kikosi, na wamerejea nyumbani na faida.

"Kimsingi tumepata mengi mazuri ambayo yatatusaidia katika safari yetu ya mashindano ya Afrika yaliyoko mbele yetu kuanzia Januari, kikubwa kuna vitu tumejifunza kupitia ziara hii," Shime alisema.

Timu hiyo ya Tanzania itaifuata Uganda kati ya Desemba 31 na Januari 12, mwakani kucheza mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Afrika kwa vijana, huku wakitarajia kurudiana kati ya Januari 17 na 19, mwakani.

# POLISI TANZANIA KUMBANA NCHIMBI

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umesema kuwa bado unaamini mshambuliaji mpya wa Yanga, Ditram Nchimbi, ni mchezaji wao halali, imeelezwa.

Kiongozi mmoja wa Polisi Tanzania (jina tunalihifadhi), alisema kuwa Nchimbi aliingia makubaliano binafsi na klabu hiyo na endapo atafanikiwa kuyavunja, ndiyo itakuwa amekamilisha uhamisho wake.

"Sisi tunajua ni mchezaji wetu, ni mali yetu, aliingia makubaliano rasmi na ya kisheria na Jeshi la Polisi, fedha za serikali haziwezi kupotea hivi hivi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa anaamini nyota huyo hataweza kuitumikia Yanga mpaka pale atakapomalizana na klabu hiyo iliyomsajili akitokea Azam FC kwa mkopo.

# Michezo

Jumatatu Desemba 30, 2019

Nipashe




Solskjaer afurahia United kuzinduka

HABARI UK 30




Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (katikati), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Burnley, Jack Cork (kulia) katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. United ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN AKAMILISHA "DOZI" YA YANGA

## Ni baada ya kukamilisha uchunguzi wake wa kikosi hicho cha Jangwani huku akitoa...

**Na Somoe Ng'itu**

ZIKIWA zimebakia siku tano kuelekea mchezo wa watani wa jadi Tanzania, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amewataka mashabiki wa timu hiyo kutokuwa na wasiwasi kwa sababu ameshapata "dawa" ya kuimaliza Yanga.

Mechi hiyo ya Januari 4, mwakani, ambayo ni ya kwanza kwa vigogo hao kukutana msimu huu wa 2019/20, itakuwa ni ya tano kwa Mbelgiji huyo anayesaidiana na Selemani Matola baada ya kuchukua mikoba ya Patrick Aussems.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sven, alisema kuwa ameshaipeleleza Yanga kupitia mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea, pamoja na kwa kuangalia picha za video za michezo yake mingine iliyopita.

Kocha huyo alisema kuwa anahafamu "joto" la mechi za watani wa jadi zinavyokuwa katika nchi mbalimbali na anajua umuhimu wa timu yake kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo.

Alisema kuwa kila siku kikosi chake kinaimarika na ataendelea kukijenga kwa sababu wanataka kutimiza malengo ya kutetea ubingwa na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ninajua mechi za watani zinavyokuwa, ninajua presha yake na umuhimu wake wa kushinda, kama kocha na kwa timu pia, nimewaangalia kupitia mechi zao zinazoendelea, pia kupitia video zao mbalimbali, ninaamini "dawa" yao itapatikana," alisema kocha huyo.

Kuhusu ubora wa kikosi chake katika mechi zinazoendelea, Sven, alisema kuwa bado anaendelea kukiimarisha kwa kutoa nafasi kwa kila mchezaji kucheza na kabla ya dirisha dogo la usajili halijafungwa hapo Januari 15, mwakani, atakuwa ameshajua wachezaji atakaowaongeza kikosini.

"Bado hatujapata muda mzuri wa kufanya mazoezi, tumekuwa na mechi mbili katika siku sita, kila mchezaji ataendelea kucheza, bado ninakiangalia kikosi baada ya mechi ya Jumanne, nitakuwa na tathmini yangu kuhusu usajili," alisema kocha huyo.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Ndanda FC kutoka Mtwara katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Simba yenye pointi 31, imecheza mechi 12, imeshinda michezo 10, sare mechi moja na ilipoteza mchezo mmoja wa ugenini dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga.

## Yanga, Biashara United kibaruani

**Na Mwandishi Wetu**

KINYANG'ANYIRO cha kuwania ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajia kuendelea tena leo kwa Yanga kuwakaribisha Biashara United kutoka mkoani Mara kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Said Maulidi "SMG", alisema kuwa mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu, hivyo timu yake imejiandaa kupambana ili kuondoka na pointi tatu muhimu.

Maulidi alisema kuwa hakuna timu ndogo kwenye ligi hiyo na msimu huu kila klabu imejiimarisha kusaka ushindi.

Alisema kuwa mzunguko wa kwanza ni mgumu zaidi kufuatia kila timu kutaka kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi kabla ya kuanza kwa hatua ya lala salama.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mechi yetu ya kesho (leo), wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo, ingawa hakutupata muda mrefu wa mapumziko, lakini tunaahidi kupambana katika mechi hiyo ili tupate ushindi," alisema Maulidi.

Francis Baraza, Kocha Mkuu wa Biashara United, amesema kuwa wachezaji wake wako tayari kwa mchezo wa leo ambao kwake ni muhimu kuweka historia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Yanga ni timu kubwa, malengo yetu ni kupambana ili kupata pointi, tumejiandaa kwa changamoto zote, tutacheza kwa tahadhari kutokana na ubora na uzoefu wa wapinzani wetu, ni mchezo ambao ninahitaji kupata matokeo mazuri ili kuweka rekodi," alisema Mkenya huyo.

Naye Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema kuwa wanawatambua vema Yanga na kwa sababu hiyo, wachezaji wake watapambana kwa muda wote wa mchezo ili kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Tunatambua Yanga walishinda mechi yao dhidi ya Tanzania Prisons, hiyo haiwapi nafasi kututisha, nasi kwenye mchezo wetu lazima tutawapa taabu na hesabu zetu ni kupata pointi tatu muhimu," alisema Mataso.

Yanga ina pointi 21 na katika msimamo wa ligi iko katika nafasi ya tatu wakati Biashara United yenye pointi 15, wako katika nafasi ya 15.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >